**17 JUNI, 2025**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Arobaini na Saba – Tarehe 17 Juni, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Priscus.

Na. 598

**Makato ya Malipo ya Wastaafu**

**MHE. PRISCUS J. TARIMO** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali inakata hela kwenye malipo ya wastaafu, na je, makato hayo ni kodi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo, Mbunge wa Moshi Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria zinazosimamia mifuko ya hifadhi ya jamii zinakataza makato yoyote, ikiwemo kodi katika malipo ya mafao ya wastaafu. Hata hivyo, pale inapobainika kuwa mstaafu ana deni la mkopo kutoka Serikalini ambalo halijalipwa kikamilifu hadi anapostaafu, sehemu ya mafao yake hukatwa kwa ajili ya kufidia deni la mkopo huo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Priscus.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mara kadhaa nimepata malalamiko kutoka kwa wastaafu, kwamba kuna makato ambayo wanakuwa hawayaelewi, tena ambao wamestaafu muda mrefu, kana kwamba hakuna deni, je, wako tayari kufuatilia ili kujua makato hayo yanatokana na kitu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa wastaafu mbalimbali waliostaafu wakiwa na mshahara mdogo wameendelea kupata pensheni kiasi kidogo sana, je, wako tayari kurekebisha ili wapate pensheni ya kuendana na hawa wanaostaafu kipindi hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Priscus Tarimo kwa kuwa mfuatiliaji mzuri wa masuala ya wananchi wake pale Moshi, na hususan Kitaifa. Pili, haya masuala ya makato ambayo ameyasema yasiyoeleweka ambayo yanafanywa; katika upande upande wa mifuko *PSSSF* ambao unahusika na wastaafu wa watumishi wa umma na NSSF ambayo inahusika na wastaafu hasa katika sekta binafsi, yote hii tumeshafanya maboresho ya

sheria. Mojawapo ni hiyo ya kukataza fedha hizi kukopewa au kukatwa kwa sababu nyingine zozote isipokuwa kwa deni ambalo ni la Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, katika makato ambayo wanafanya, inawezekana wakawa na makubaliano nje ya utaratibu wa kisheria, lakini nje ya utaratibu wa mifuko. Katika mifuko mpaka sasa haturuhusu na ni marufuku na ni katazo kisheria kutumia pensheni ya mstaafu kwenye kufanyia kazi nyingine yoyote tofauti na kusudio tarajiwa la pensheni.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili linalohusu kima cha wastaafu, ni kweli Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ililiona hilo na ikaanza na hatua ya wafanyakazi walio kazini kuwapandishia madaraja ya mishahara pamoja na stahiki zao na kulipa madeni yaliyokuwepo muda mrefu. Hatua ya pili tulifanya *actuarial evaluation*, na kufanya pia utafiti kuhusiana na kima cha chini cha mishahara na tukaongeza hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo ilikwenda pia kuwagusa wastaafu. Tuliongeza kima cha chini kutoka shilingi 100,000/= ya pensheni kwenda shilingi 150,000/= kwa sasa. Kwa hiyo, hakuna anayepata chini ya hapo. Malipo haya tumeyaweka kidigitali. Tumesha-*advance* hii mifuko, tunatumia zaidi TEHAMA sasa, na taarifa ya mstaafu anaipata kwenye kiganja chake kupitia simu ya mkononi….

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante …

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, kama kuna mtu ana changamoto tunaweza kuwasiliana naye au kuonana naye, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Munira Mustapha.

Na. 599

**Kupunguza Tatizo la Ajira kwa Vijana**

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza tatizo la ajira kwa vijana hasa wanaomaliza Vyuo Vikuu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEM AVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Munira Mustapha Khatib, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ya kuwawezesha vijana, hususan waliohitimu vyuo vikuu ili kupunguza tatizo la ajira kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Mafunzo ya Uzoefu Kazini kwa Wahitimu wa Mwaka 2017;

(ii) Kubuni na kutekeleza programu maalum zinazowawezesha vijana kujifunza kwa vitendo kupitia sekta zinazozalisha ajira kwa wingi; na

(iii) Kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa vijana kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na Mfuko wa Maendeleo ya Vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa wito kwa waajiri wote nchini kuendelea kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa programu ya mafunzo ya vitendo mahala pa kazi kwa wahitimu kwa kutoa fursa kwa vijana wahitimu kuendelea kujifunza katika maeneo yao ya kazi. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munira.

**MHE. MUNIRA MUSTAPHA KHATIB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Nina maswali mawili ya nyongeza. Je, kuna mpango gani endelevu wa kuwawezesha vijana kiuchumi walio wasomi na wasio wasomi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Mikopo ya vijana ya asilimia nne inayopatikana kwenye halmashauri, imekuwa na changamoto sana. Je, Serikali ina mpango gani, kwamba badala ya kuwawezesha vijana watano watano wakopeshe kwa kijana mmoja mmoja kama ilivyo taasisi nyingine za kifedha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Moja, ni kweli kwamba Serikali hii mikopo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imekuwa rafiki sana kwa vijana, na ni kundi la kwanza alilokutana nalo alipoingia madarakani. Alisikiliza changamoto zao na kuziwekea mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya mpango wa kuwawezesha vijana waliosoma na wasiosoma, ni pamoja na kuendeleza kutengeneza mifumo ya utoaji wa mikopo. Moja ya mikopo inayotolewa ni hii maarufu inaitwa 4:4:2, ambayo ni 10% ya pato ghafi la halmashauri. Katika halmashauri zote 115 hapa nchini ni mkopo kwa vijana ambao hutolewa kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna programu za mafunzo na uwezeshaji wa vijana na ukuzaji ujuzi. Moja ya programu ambayo tunayo ni *Building Better Tomorrow* ili chini ya Wizara ya Kilimo, lakini pia tunayo *BBT Life* kupitia Wizara ya Mifugo ambapo zaidi ya shilingi bilioni 10.3 zimetumika kwa ajili ya vijana. Vilevile tuna *Mining for Brighter Tomorrow* ambayo iko chini ya Wizara ya Madini, na tumekuwa tukiweka mpango wa kuwapa vijana vitalu vya uchimbaji, vifaa pamoja na mafunzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *program* nyingine ni kwenye michezo. Kwenye michezo kuna zaidi ya shilingi bilioni tano ambazo Mheshimiwa Rais alizitoa kwa ajili ya kuwasaidia vijana ambao wako kwenye masuala hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, wale ambao wako kwenye kusoma, kwa upande wa vyuo vikuu tu ni shilingi bilioni 788 kwa ajili ya Bodi ya Mikopo ya wanafunzi. Pia, kuanzia huku chini; *kindergarten,* darasa la awali hadi kidato cha sita, tunafahamu kuhusu Mpango wa Elimu Bila Malipo ambapo zaidi ya shilingi bilioni 28 inalipwa kila mwezi kwa ajili ya kusaidia programu hiyo, ikiwa ni sambamba na *Samia Scholarships* pamoja na programu nyingine ambazo ni wezeshi kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ile ya mafunzo kazini ambapo zaidi ya vijana 27,471 walipata fursa ya kupewa mafunzo, na wengine 161,000 ambao wapo kwenye programu mbalimbali zinazowasaidia. Kwa hiyo, hili jambo tumeliona kama Serikali na tunaendelea kuliboresha kila wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na lile suala la vijana watano kuchukua mkopo, tumebadilisha mwongozo wa utoaji mikopo kwenye halmashauri. Sasa hivi hata kijana mmoja anaweza kukopa shilingi milioni 10 hadi milioni 50. Hii ni kwa kijana ambaye *ame-graduate* na ambayo ameonekana anafanya vizuri zaidi katika mikopo ambayo imetolewa kwenye ule mpango wa 4:4:2 pamoja na Mfuko wa Maendeleo wa Vijana. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Kyombo, kwa niaba Mheshimiwa Oliver.

Na. 600

**Barabara ya Bulembo Kona Hadi Hospitali ya Wilaya Missenyi**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA K.n.y. MHE. DKT. FLORENT L. KYOMBO** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itajenga barabara ya lami, kutoka Bulembo kona hadi Hospitali ya Wilaya ya Missenyi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na usanifu wa Barabara ya Bulembo Kona hadi Hospitali ya Wilaya ya Missenyi kwa lengo la kubaini gharama halisi za utekelezaji wa ujenzi kwa tabaka la lami. Gharama halisi za utekelezaji wa ujenzi wa barabara hiyo zitakapobainika, Serikali itaitengea fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa tabaka la lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja ya Wilaya ya Misenyi kwa kujenga, kukarabati na kuifanyia matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana na ninaipongeza sana Serikali kwa majibu mazuri. Pia, ninaipongeza Serikali kwa kazi nzuri iliyofanyika katika Jimbo la Misenyi kwa ujenzi wa miundombinu ya barabara. Je, ni lini usanifu wa barabara hiyo utafanyika ili kazi ya ujenzi ianze?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili. Mji wetu wa Benako uliopo Jimbo la Ngara unakua kwa haraka sana na unaunganisha nchi jirani. Je, Serikali haioni haja ya kuanza kujenga barabara za mitaa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba barabara hii ya lami ya Bulembo Kona kwenda Hospitali ya Halmashauri ya Misenyi ni barabara muhimu; na Mheshimiwa Mbunge Oliver Semuguruka amekuwa akifuatilia mara kwa mara ili kuona inajengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali imeshaandaa mpango wa kufanya usanifu wa kina mwaka ujao wa fedha

kuanzia Julai, 2025/2026. Baada ya kubainika gharama zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi kwa tabaka la lami, tutatenga fedha mwaka wa fedha 2026/2027 kwa ajili ya kuanza kujenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali la pili kuhusiana na Mji wa Benako; ipo miji mingi ambayo inaendelea kukua, mojawapo ni eneo la Benako katika Halmashauri ya Ngara, na lina wananchi wengi na shughuli nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilishaweka mpango kwamba, maeneo yote ambayo yanakua, kwanza kunakuwa na mpango endelevu kwa kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha changarawe, kiwango cha lami, lakini pia kwa kuweka taa za barabarani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunalichukua hilo, tutafanyia tathmini na kuona kwa kadri ya fedha zinavyopatikana, tutaendelea kutenga kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami katika eneo la Benako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, mwaka 2024 Septemba, niliomba ukarabati wa barabara za Ifakara Mjini, hasa zile za lami na Serikali ikatupatia mkandarasi tangu Septemba mwaka 2024. Hadi ninavyozungumza hivi, yule Mkandarasi hajafanya kazi ile. Je, Serikali ina kauli gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefanya ziara katika Mji wa Ifakara hivi karibuni na nimpongeze sana Mheshimiwa Asenga kwa ufuatiliaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan

ilisikia kilio cha wananchi wa Mji wa Ifakara, ilitafuta fedha na mkandarasi alipewa kazi ya kujenga na kukarabati barabara za Mji wa Ifakara. Tunafahamu kwamba hapa katikati kulikuwa na changamoto ya utekelezaji kutoka kwa mkandarasi. Tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI imechukua hatua za kumrejesha mara moja *site* mkandarasi ili aendelee na ujenzi wa barabara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza nichukukue nafasi hii nimsisitize Meneja wa *TARURA* wa Wilaya na Mkoa wa Morogoro wamfuatilie mkandarasi haraka iwezekanavyo ili arejee *site* kuanza na ujenzi kama tulivyokubaliana ili barabara zile ziweze kukarabatiwa kama mpango ulivyoainishwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaka kujua, ni lini barabara inayotoka Wilaya ya Manyoni inayounganisha Wilaya nne za Chemba – Mpendo – Sanzawa - Kwa Mtoro – Lahoda hadi Hanang', itajengwa kwa kiwango cha lami kwa sababu ni barabara inayounganisha mikoa mitatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ziko barabara ambazo ni za muhimu sana na za kimkakati kwa uchumi wa maendeleo mbalimbali ikiwemo barabara ambayo Mheshimiwa Monni ameitaja. Ninaomba tu nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mohamed Monni na wananchi wa Jimbo la Chemba kwamba Serikali inatambua uhitaji wa ujenzi wa barabara hiyo. Hatua ambayo inaendelea ni kutenga bajeti kwa awamu baada ya kufanya usanifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie tu kwamba, tutaendelea kuijenga barabara hiyo kwa awamu kwa sababu tumeshaiingiza kwenye mchoro wa barabara za kimkakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Barabara za Mtaa wa Kwa Mwarabu na Mtaa wa Kwa Mzungu zilizopo katika Kata ya Kilungule hazipitiki kwa uharibifu uliotokana na Mvua. Je, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati barabara hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ziko barabara ambazo zimeharibiwa kutokana na neema ya mvua ambayo imekuja na changamoto, ikiwemo na barabara hiyo ya Kwa Mwarabu na Kwa Mzungu katika Jimbo la Mbagala, Manispaa ya Temeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari kupitia *TARURA,* lakini pia hata *DMDP* tulishakubaliana kwamba wataalamu waainishe barabara zote zilizoathirika na mafuriko ya mvua na kuzitengea fedha kwenye Mpango wa dharura ili kuzifanyia marekebisho angalau ziweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI nimsisitize Meneja wa *TARURA* wa Temeke na Mkoa wa Dar es Salaam wazipitie barabara hizo mapema iwezekanavyo, wafanye tathmini ya maeneo korofi kwa ajili ya utengenezaji na ziweze kupitika na kuwa na ubora zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika Jimbo la Rungwe, Barabara ya Ilima - Masukulu na Matwebe ni korofi, ambayo tunaomba Serikali angalau iweke kiwango cha changarawe. Je, ni lini watapeleka fedha kuisaidia *TARURA* ili iweze kutengeza barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeongeza sana bajeti ya barabara kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, Halmashauri ya Rungwe ni moja ya halmashauri ambazo zimeongezewa sana bajeti kwa zaidi ya mara nne ya bajeti ukilinganisha na miaka minne iliyopita na sasa. Kwa hiyo, ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunaishukua barabara hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tutawasiliana na Menejimenti ya *TARURA* ngazi ya Mkoa wa Mbeya na Wilaya ya Rungwe ili tuweze kuona kama imeingizwa kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha itafanyiwa matengenezo, na ikiwa haijaingizwa, tutaona utaratibu mzuri wa kupata fedha ili twende kuitengeneza na iweze kupitika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo hiyo. Mheshimiwa Dkt. Kimea.

Na. 601

**Ujenzi wa Daraja la Kitifu – *Korogwe TC***

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Kitifu linalounganisha Kata za Mgombezi na Msambiazi katika Halmashauri ya *Korogwe TC*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza azma wa ujenzi wa Daraja la Kitifu, Serikali imepanga kufanya usanifu wa kina katika mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kutumia wataalam wa *TARURA*. Baada ya kukamilisha usanifu huo na kupata gharama

halisi za mradi, Serikali itatafuta fedha ili kuwezesha ujenzi wa Daraja la Kitifu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimea.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa majibu ya Serikali. Ni miaka mingi sana daraja hili limekatika na linaleta changamoto kubwa kuvuka kati ya sehemu hizi mbili; na nimekwishajibiwa hivi mara nyingi. Je, Waziri ananihakikishia vipi kwamba ni kweli huu mwaka wa fedha unafuata usanifu utafanyika na daraja litajengwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, daraja hili la Kitifu ni muhimu linalounganisha Kata ya Mgombezi na Kata ya Msambiazi katika Halmashauri ya Mji wa Korogwe na vijiji kadhaa ambako kuna shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana baada ya Mheshimiwa Mbunge Kimea kuleta hoja hiyo, Serikali imeiwekea bajeti kwa ajili ya usanifu wa kina mwaka ujao wa fedha ili tuweze kujua gharama halisi zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka ujao wa fedha tumelitengea bajeti. Kwa hiyo, ni uhakika kwamba litafanyiwa usanifu wa kina, lakini pia tutatengea fedha baada ya kujua gharama ambazo zinahitajika. Kwa hiyo, nimhakikishie yeye pamoja na wananchi wa Mji wa Korogwe kwamba daraja hili litajengwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa nafasi. Zipo barabara na madaraja ambayo yametangazwa na TAMISEMI kupitia miradi ya *DJP*

ikiwemo na Daraja la Nyatharogo linalotuunganisha Tarime na Rorya. Je, ni lini mradi huu utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama ambavyo amesema Mheshimiwa Wambura Chege, Mbunge wa Rorya kwamba ziko barabara, madaraja na ma-*culvert* ambayo yanahitaji ujenzi. Yako ambayo yametangazwa na zabuni zimepatikana na wakandarasi wamepatikana. Hatua zinazoendelea ziko katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hatua ambazo ni *mobilization,* ziko hatua ambazo ujenzi umeanza na ziko hatua ambazo zinaendelea na usanifu. Nikuhakikishie tu, madaraja yote ambayo ni muhimu na yanahitaji ujenzi wa dharura, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele ili kuhakikisha kwamba yanajengwa na yanapitika vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Daraja la Mashine ya Maji pale Kipatimu limesimama kwa muda mrefu sana kujengwa. Je, ni lini Serikali itakamilisha kulijenga daraja hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli daraja hilo lishapewa mkandarasi, na alikuwa ameanza kazi, lakini kutokana na mazingira tofauti na hasa hali ya hewa ya mvua, na pia baadhi ya masuala, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tumelichukua hilo na tutatoa maelekezo kwa Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Kilwa pamoja na Mkoa wa Lindi ili waweze kukaa na mkandarasi kuona wapi kuna changamoto ili tuweze kuona namna ya kuzitatua mapema iwezekanavyo na daraja hilo liweze kujengwa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma.

Na. 602

**Mji Mdogo Muleba Kupatiwa Hadhi ya Halmashauri ya Mji**

**MHE DKT. OSCAR I. KIKOYO** aliuliza: -

Je, lini Mji Mdogo wa Muleba utapatiwa hadhi ya Halmashauri ya Mji wa Muleba?

**NAIBBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri huanzishwa au kupandishwa hadhi kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa Uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa mwongozo, uanzishaji wa halmashauri mpya huanza na kusudio ambalo hupaswa kujadiliwa katika vikao vya ngazi za vijiji/mitaa, kata, Halmashauri, Wilaya na Mkoa na kuwasilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kupitia Katibu Tawala Mkoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Muleba inashauriwa na kuendelea na hatua ikizingatia Sheria na Mwongozo wa uanzishaji wa maeneo ya utawala, na utaratibu utakapofika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tathmini na uchambuzi wa vigezo utafanyika kwa hatua zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeshaweka vigezo vya kupandisha hadhi hizi halmashauri zetu, je, Serikali haioni

kutokana na vile vigezo miji inabidi ipande *automatically* hata bila kuleta maombi pale ambapo mji mdogo unakidhi vile vigezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, miji inapanda kwanza kutokana na bajeti za Serikali. Ipo miji ambayo inakidhi vigezo, lakini pia tunaendelea kuboresha maeneo ya utawala yaliyopo kwanza. Kuna halmashauri na kuna miji haina majengo ya Wakurugenzi, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya, ofisi za kata na kadhalika. Kwa hiyo, pamoja na kwamba ipo miji ambayo inakidhi vigezo, lakini tumeona kipaumbele kwanza tukamilishe miundombinu muhimu katika halmashauri zilizopo kabla ya kuanza kuongeza halmashauri nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Kikoyo kwamba Mji wa Muleba ni miongoni mwa miji ambayo tunawashauri wafuate utaratibu huo. Tunajua tunahitaji kuwa na vigezo, uwezo wa mapato kwa angalau 50% kujitegemea kama halmashauri, lakini pia idadi ya wananchi pamoja na vigezo vingine. Kwa hiyo, pale ambapo watawasilisha maombi hayo, Serikali itafanya tathmini na kuona uwezekano wa kupandisha Mji wa Muleba kuwa halmashauri ya mji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea ni zaidi ya miaka 15 sasa, na kwa sasa Mji wa Nachingwea umeendelea sana ukilinganisha na miaka 15 iliyopita na taratibu zote tumefuata. Je, ni lini Serikali itapandisha Mamlaka ya Mji Mdogo Nachingwea kuwa Mamlaka ya Mji kamili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Amandus Chinguile, Halmashauri ya Nachingwea iliwasilisha maombi ya Mji

Mdogo wa Nachingwea kuwa Halmashauri ya Mji wa Nachingwea, lakini niwapongeze kwamba kuna baadhi ya vigezo wamekidhi, lakini kuna baadhi ya vigezo bado havijafikiwa ikiwemo uwezo wa mapato ya ndani kujitegemea kwa 50%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Nachingwea tuendelee kuwa na subira wakati Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vigezo, na pale ambapo tutakidhi vigezo hivyo, tunaamini kabisa tutapata fursa ya kupata halmashauri ya mji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Asia, kwa niaba Mheshimiwa Dkt. Kabati.

Na. 603

**Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Katika Mji wa Babati**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI K.n.y. MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Mji wa Babati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi katika Halmashauri ya Mji wa Babati unatekelezwa kupitia Mradi wa Tanzania *Cities Transforming Infrastructures and Competitiveness (TACTIC)*. Aidha, mkandarasi ameshapatikana na mradi utatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 19.99. Taratibu za kukamilisha mkataba zinaendelea ili uweze kusainiwa na ujenzi unatarajiwa kutumia muda wa miezi 15 mpaka kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ujenzi wa stendi ya mabasi, mitaro ya maji na barabara za lami katika Mji wa Babati unatarajiwa kuanza mwezi Julai, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, nishukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri kwa Wananchi hawa wa Babati. Je, ni lini sasa Serikali itamalizia ujenzi wa stendi ya mabasi katika Mji Mdogo wa Ilula katika Wilaya ya Kilolo? Kwa sababu ni muda mrefu sana zaidi ya miaka 15 ile stendi imekuwa ikijengwa na pale ni mji wa kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, kuna mradi mwingine umeanzishwa katika Makao Makuu ya Kilolo Stendi ya Mabasi, ni lini sasa mtamaliza ule mradi pia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Spika Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati kwa pamoja kwamba tunatambua kuwa kuna uhitaji wa stendi ya mabasi katika Mji wa Ilula na katika Mji wa Kilolo, lakini nikuhakikishie tu kwamba Serikali imeendelea kutenga fedha kwa awamu katika bajeti zake na kutekeleza ujenzi wa stendi hizo kwa awamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi hili litaendelea katika kila mwaka wa bajeti, na tutatenga fedha kutoka mapato ya ndani ya halmashauri, lakini pia Serikali Kuu itaona namna ya kuongezea fedha ili kujenga stendi hizo katika maeneo hayo mawili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime iliandika kuomba miradi mitatu; soko kuu, stendi ya mabasi pale Kemange na barabara ya kuzunguka Mji wa Tarime. Tunashukuru soko kuu mmeshajenga. Ni lini sasa hii miradi ya stendi pamoja na barabara ya kuzunguka Mji wa Tarime itaenda kujengwa ambayo ni ya kimkakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Mji wa Tarime ni moja ya miji ambayo ipo kwenye Mradi wa *TACTIC,* miji 45, na ni kweli kwamba Serikali imeanza ujenzi wa baadhi ya miundombinu iliyoko kwenye hiyo *package*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu kwamba mpango wa Serikali ni kuhakikisha kwamba *Tier One, Two* na *Three* zote zinakamilika angalau tunapofika mwaka wa fedha ujao wa 2025/2026. Kwa hiyo, nikuhakikishie tu kwamba miundombinu mingine yote ambayo haijajengwa katika Mji wa Tarime pia tutahakikisha inajengwa kwenye *package* hiyo ya *TACTIC* ili tuweze kuboresha Halmashauri ya Mji wa Tarime.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Muharami Mkenge, kwa niaba Mheshimiwa Dkt. Kabati, swali namba 604.

Mheshimiwa Dkt. Kabati simama uliza swali kwa niaba.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo hapa.

**NAIBU SPIKA:** Kwa niaba Mheshimiwa Asenga.

Na. 604

**Kujenga Ukuta Fukwe za Bagamoyo**

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA K.n.y. MHE. MUHARAMI S. MKENGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga ukuta katika Fukwe za Bagamoyo ili kuzuia maji ya bahari kumega sehemu ya ardhi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fukwe za Bagamoyo ni miongoni mwa fukwe zenye changamoto ya kumomonyoka kuta za ufukwe kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na kuongezeka kwa kina cha bahari. Hali hii husababisha maji chumvi kuingia katika maeneo ya makazi na mashamba ya wananchi. Maeneo yalioathirika zaidi ni pamoja na eneo la *Livingstone*, Hoteli ya Stella Maris, *Travella lodge*, Kaole, Changwahel, Razaba, Kitame, Mlingotini, na Kondo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kufanya tathmini ya uharibifu wa Fukwe za Bagamoyo na kutafuta fedha kupitia Mifuko ya Usimamizi wa Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ikiwemo *Adaptation Fund, GEF, GCF,* na washirika wa maendeleo. Kwa muktadha huo, shughuli za ujenzi wa ukuta katika fukwe za Bagamoyo utafanyika baada ya fedha kupatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini Mheshimiwa Muharami anaomba kwamba tutafute kikosi cha dharura au timu ya wataalamu wa dharura wa mazingira waende wakaone athari zilizopatikana. Je, Serikali ina majibu gani katika mpango huo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, katika nchi nzima kuna baadhi ya mito ambayo imeathiriwa sana na athari za kimazingira na mafuriko ikiwemo Mto Rumemo wa Halmashauri ya Mji wa Ifakara ambapo Serikali imekuwa ikiboresha kwa kuweka tuta mara kwa mara. Je, kwa msimu wa mwaka huu wa fedha, Serikali ina mpango gani wa kuboresha tuta la Mto Rumemo katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na wazo lake na tuna kikosi kazi kabisa kwenye Wizara hii kinachotembelea maeneo ambayo yanaathirika na ujazo wa maji unaozidi kiwango.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye swali la pili la Mto Ifakara pamoja na mwendelezo ambao tunaendelea kuuangalia kwanza. Ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi ambazo unaendelea kufanya. Nipokee hilo jambo na tutatuma timu kwa ajili ya kwenda kuangalia uhalisia, lakini kwa mwaka wa fedha huu ambao tayari tumeshapitisha bajeti yetu, fedha zimetengwa kwa ajili ya shughuli hizi za ukarabati wa kuta zinazoleta shida.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASYA MWADINI MOHAMMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, Serikali haioni haja ya kutembelea fukwe zote nchini kwa sababu changamoto hii ya maji ya bahari kuingia kwa wananchi imekuwa ni kubwa na tatizo ni kubwa sana kwa jamii? Hawaoni haja sasa ya kutembelea na kuweka mpango maalumu ili kuweza kuwasaidia wananchi na kunusuru kadhia hii inayowakumba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**N NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,**

**MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, cha kwanza kabisa ni mabadiliko ya tabianchi ambayo yameleta mambo mapya kwenye maeneo yetu. Fukwe hizi zimekuwa zikidumu kwa muda mrefu sana, lakini kwa sasa ninaona kabisa baada ya mazingira haya kuwa katika changamoto hiyo, maji yanajaa kwenye fukwe mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikubaliane na ushauri wa Mheshimiwa Asya kwamba tutafanya hilo zoezi na tunaomba taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kila mnapopata eneo ambalo linaleta kadhia hizo, tujulishwe ili tuweze kuchukua hatua za haraka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Madini. Mheshimiwa Ally Jumbe; kwa niaba yake, swali hilo litaulizwa na Mheshimiwa Suma.

Na. 605

**Malipo ya Waliokuwa Wafanyakazi**
***Mgodi wa Kiwira Coal Mine***

**MHE. SUMA I. FYANDOMO K.n.y. MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza: -

Je, nini hatma ya malipo ya waliokuwa Wafanyakazi wa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, deni la wafanyakazi wa Kiwira lilitokana na malalamiko ya mapunjo ya mafao kwa waliokuwa wafanyakazi wa mgodi huo kabla ya ubinafsishaji. Baada ya kuwasilishwa kwa malalamiko ya mapunjo hayo na Chama cha Wafanyakazi Mgodini *(TAMICO)*, Serikali ilifanya ukaguzi maalum kupitia Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* Mwezi Novemba, 2008 na baadaye iliyokuwa Wizara ya Nishati na

Madini iliunda timu ambayo ilihakiki madeni hayo mwezi Desemba, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakiki wa madeni hayo ulibaini kuwa madai halali ya wafanyakazi yalikuwa shilingi 1,000,240,000.00 kwa wafanyakazi 893 na madeni ya wazabuni ikiwemo huduma ya ulinzi ilikuwa shilingi milioni 496 na hivyo kufanya deni kuwa jumla ya shilingi 1,520,000,000.00.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhakiki, madeni hayo yalijumuishwa katika madeni ya Serikali na Wizara inaendelea kufuatilia Wizara ya Fedha ili madeni hayo yaweze kulipwa. Aidha, Wizara ya Fedha ilituma wataalamu wake mwezi Februari, 2025 kufanya tena uhakiki wa madeni hayo ili kujiridhisha na taarifa iliyotokana na uhakiki uliofanyika Desemba, 2015 ili kujiridhisha kabla ya kulipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa, timu ya wataalamu inakamilisha taarifa ya uhakiki ili madeni hayo yaweze kulipwa haraka. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza ambayo anauliza Mheshimiwa Mbunge wa Kyela Ally Mlaghila Jumbe. Je, kwa nini baada ya uhakiki hawajalipwa mpaka sasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Wafanyakazi hao wa Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Kiwira wanataka kujua ni lini sasa watalipwa fedha hizo, kwa sababu ni muda mrefu sana madeni hayo hayajalipwa pamoja na uhakiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, madeni hayo hayajalipwa hadi sasa, inawezekana ni kutokana na sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza ni upatikanaji wa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya pili, kwa kuwa ni suala la fedha na linahitaji uhakiki wa kuondoa uwezekanao wa watu wasiohusika kudai, ndiyo maana baada ya *CAG* kutoa maelekezo kwamba watu hao walipwe, Wizara wakati ule Nishati na Madini walifanya uhakiki wakaja na hesabu yao na wakapeleka hesabu Serikalini na ili Serikali nayo iweze kulipa kupitia Hazina, yaani Wizara ya Fedha na wao wana hatua zao za kuhakiki kujiridhisha kabla hawajalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninadhani ni kwa sababu hizo ndiyo maana mpaka sasa hivi ndugu hawa hawajaweza kulipwa. kuhusu ni lini? Hili kwa sababu sasa limechukuliwa mwaka huu na kuwekwa kwenye orodha ya madeni ambayo ni lazima Serikali iyalipe, mara baada ya uhakiki huu wa mwisho kukamilika, ninaamini kabisa kwamba wadai wote watapata haki yao, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Mheshimiwa Asha Juma.

Na. 606

**Watoto Wanaozaliwa Kabla ya Wakati**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kushughulikia watoto wanaozaliwa kabla ya wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejenga wodi maalumu 151 kwa ajili ya watoto wachanga wanaozaliwa kabla, ambazo zimeongezeka kutoka wodi 14 hadi 165 mwaka 2024, ambapo lengo ni kufikia hospitali 280 ifikapo Desemba, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepeleka Bohari ya Dawa takribani shilingi za Kitanzania bilioni 2.2 kwa ajili ya ununuzi wa

vifaatiba muhimu kwa watoto wachanga ikiwemo watoto wanaozaliwa kabla ya wakati ili kuimarisha huduma zinazotolewa kwa watoto wanaozaliwa kabla ya wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asha Juma.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu yenye weledi ya Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa watoto hawa wanaozaliwa kabla ya wakati mara nyingi wanakuwa na matatizo hasa ya kupumua na uzoefu uliokuwepo ni kulea watoto hawa kwa *Kangaroo Style,* je, Serikali imejipanga vipi kuimarisha *special care nurseries,* vitengo maalumu kwa ajili ya kuweka *incubators* za kisasa, na mitambo ya *Oxygen* kuwasaidia watoto hawa katika wodi za wazazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine ni je, Serikali imefanya utafiti wa kugundua visababishi vinavyofanya watoto kuzaliwa mapema? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, Mama yangu, kwa maswali haya ya msingi sana na amekuwa akiwafuatilia wakati wote. Hata matokeo mazuri tuliyoyapata hapo kwa maana ya ujenzi huu uliofanyika ni mojawapo ya mawazo yake ambayo amekuwa akitupa kila wakati na kuhakikisha tunafikia haya malengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa swali lake hili, moja, ukisikia tumefikia hospitali 165, maana yake yote uliyoyasema yako pale kuhakikisha wale watoto wanapata joto, na wanaweza kupumua kwa sababu wengine wanazaliwa kabla ya mapafu hayajakua vizuri na kuna vitu vingine ambavyo vinatakiwa visaidie mapafu

kupanuka na kusinyaa, bado havijajengeka. Kwa hiyo, hivyo vitu vyote vinajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana unaona tunasema ni wodi maalumu zinakuwa na hayo mambo yote ambayo Mheshimiwa Mbunge ana wasiwasi nayo, kuwa yanaweza kuwa ndani ya hiyo wodi na kuzuia hata matatizo yanayoweza kutokea baadaye kwenye maisha wanapokuwa watu wazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili. Je, Serikali imegundua visababishi? *Yes,* visababishi vingine vinajulikana, vingine havijulikani, ndiyo maana unaona Rais wetu anatoa fedha nyingi sana kupeleka huduma karibu na jamii. Kwa nini tunapeleka?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ili pia akina mama waweze kuhudhuria kliniki ili waweze kupimwa wakati wote na kufuatiliwa wakati wote kwa sababu kuna sababu nyingine ni maambukizi, kuna sababu nyingine ni *stress,* kuna sababu nyingine ni *hormone* ambazo sasa zinaweza zikajulikana wakati huo, na zikijulikana mapema zinafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wengine kwenye mlango wa kizazi unakuwa mfupi kuna namna ya kufanya pia. Kwa hiyo, kujua hayo mapema wakati mama anahudhuria kliniki yakigundulika mwisho wa siku yanapatiwa tiba yake na kufuatiliwa kwa karibu na kufanya huyu mama asiweze akafikia mahali pakumzaa huyu mtoto kabla ya wiki zake zinazotakiwa kutimia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa Serikali imeboresha miundombinu ya kutunza hawa watoto waliozalizaliwa kabla ya wakati, lakini gharama za kuwatunza hawa watoto ambazo wanazipata wazazi ni kubwa sana. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mwafaka wa kuwa na ruzuku mahsusi kwa ajili ya wakina mama ambao wanazaa watoto njiti? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa ni zuri sana na ninakumbuka kwa kweli tulishirikiana naye kwenye Kamati kuweza kuja na bajeti ya kuona namna gani tunafanya kwenye eneo hili na hasa kwenye eneo la akina mama, na ninafikiri anakumbuka yalipokuja yale mahesabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, Serikali ina namna ya kufanya, ndiyo maana wale wasiojiweza kuna namna ya kuwasaidia. Pia tuna sera yetu ile ya akina mama na hawa wanaojifungua kwa namna hiyo kuhakikisha hawaingii kwenye hizo gharama kulingana na hospitali *level* yake ilivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba bado kuna changamoto, pamoja na Serikali kuwasaidia hao akina mama bila kulipia, lakini kwa kweli wote hawajaweza kusaidiwa kwa 100% kama ambavyo wanapatikana. Imewezekana kusaidia kuanzia 68% ya akina mama wote wanaopata matatizo hayo, kwa maana hiyo 32% bado wamebaki, hawajata huo msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, *solution* kwa kweli ambayo inaweza ikaja kutusaidia ili tuwafikie wote kwa 100% ni Bima ya Afya kwa Wote. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana, na ninajua unarudi Bunge lijalo, tushirikiane vizuri tuhakikishe Bima ya Afya kwa Wote inaenda kutokea ili tufanye mambo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

Na. 607

**Kuimarisha Huduma za Matibabu ya Kibingwa**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, hospitali gani zinatoa huduma za Matibabu Bingwa na kwa magonjwa yapi kwa kiwango cha Kimataifa hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hospitali sita za kanda na Taifa zinatoa huduma kwa kiwango cha Kimataifa, ambapo hospitali nne zikiwa ni za Serikali na mbili ni za binafsi ambazo ni kama ifuatavyo: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Taasisi ya Mifupa ya Muhimbili, Taasisi ya Saratani ya *Ocean Road,* Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Hospitali ya *SAIFEE* na Hospitali ya AGAKHAN.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya huduma za kibingwa bobezi zinazotolewa ni upandikizaji wa figo, upandikizaji wa vifaa vya usikivu, upandikizaji wa uroto, matibabu ya magonjwa ya moyo kwa tundu dogo na mishipa, upandikizaji meno, huduma za kupunguza uzito, matibabu ya magonjwa ya mifupa na mishipa ya fahamu na huduma za tiba ya magonjwa ya saratani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa kutoa majibu mazuri na elimu kwa umma kuhusu hospitali hizi za matibabu ya kibingwa ambazo ziko kwenye kanda moja. Nikiwa na maana ya hospitali zote alizozitaja Mheshimiwa Naibu Waziri ziko Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza. Kwa kuwa Hospitali ya *KCMC* ambayo iko kwenye kanda nyingine, ni Kaskazini, imekuwa ikitoa matibabu mazuri sana. Sasa hivi katika yale matibabu nane aliyoyataja, mawili tayari *KCMC* inaenda kumudu, ikiwepo matibabu ya kansa na matibabu ya ugonjwa wa moyo. Je, Serikali iko tayari sasa kuendelea kuisaidia *KCMC* ili iweze kukidhi kutoa matibabu hayo mengine na kupunguza ile shida ya kuleta mlundikano Dar es Salaam tu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kwa kuwa kutoa matibabu hayo ya kibingwa ni pamoja na wafanyakazi hao kuwa na mishahara mizuri, utulivu wa akili na kuacha kufungua hospitali

zao pembeni, mathalani wanaofanya *KCMC* kwenda kutoa matibabu Arusha, Serikali iko tayari sasa kusaidia *KCMC* kuboresha mishahara ya wafanyakazi wa pale ili wafanye kazi kwa utulivu na kutoa matibabu hayo vizuri? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Shally Raymond. Hili nasema kwa niaba ya Wabunge wenzangu wa Mkoa wa Kilimanjaro, amekuwa ni tunu kubwa sana kwa maana ya sisi Wabunge wa Mkoa wa Kilimanjaro wa Majimbo, lakini na wanawake wa Mkoa wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa, mama yangu tuna hakika anaenda kurudi tena akina mama wa Mkoa wa Kilimanjaro wanamrudisha, nafikiri ataona haya mafanikio makubwa anayoyafanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye tiba kwa Mkoa huo wa Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Juni, hiyo Idara ya Kansa, na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu alishatoa shilingi bilioni saba kwenye hospitali hiyo kwa ajili ya kutengeneza hilo eneo la kansa analosema, lakini anajua kuna eneo lingine kwa ajili ya *center* ya matatizo ya moyo nayo inaendelea pale *KCMC*. Maana yake, baada ya muda mfupi nayo tiba za moyo zitaanza kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama unavyojua, japo hatujalisemea hapa sana, *KCMC* nayo kwenye matibabu ya Kimataifa inafanya vizuri sana kwenye eneo la ngozi na kwenye eneo la macho. Kwa hiyo, kwa kweli ina-*perform* vizuri sana kwenye eneo hilo. Ukiangalia utaona wagonjwa kutoka Mataifa mbalimbali wakija kwenye eneo hilo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili hebu naomba mama yangu kama anaweza akarudia swali, maana sikulisikia vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond, swali la pili lirudie.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa matibabu haya ya kibingwa yanahitaji utulivu wa akili na utulivu wa akili kwa mfanyakazi yeyote wakiwemo madaktari ni pamoja na kulipwa vizuri madaktari, wauguzi na wote ambao wapo kwenye hii sekta ya afya, je, Serikali iko tayari sasa kuisaidia *KCMC* kwenye eneo hilo ili madaktari wa *KCMC* watulie kazini kwenye vituo vyao pale *KCMC* na siyo kwenda tena kufungua hospitali huko Arusha, Moshi na kwingineko? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilimsikia tu, nilitaka Wanakilimanjaro na wana-*KCMC* wasikie vizuri alichokisema. Nimwambie tu mama yangu kwamba, moja, Serikali ilianza mchakato huo, kwa sababu ilikuwa inatakiwa *KCMC* iwe sasa taasisi ili iweze kupata hiyo mishahara anayoisema na mchakato ulifanyika mpaka ilipofika hatua ya kuwa yanachakatwa hayo maamuzi eneo la utumishi, lakini baadaye likatoka suala la kufanya upembuzi yakinifu kuona taasisi gani zipunguzwe na taasisi gani ziongezwe na huo mchakato uliendelea, ndiyo uliochelewesha hiyo hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado tunaendelea kuwasiliana ndani ya Serikali ili kuona ni namna gani sasa *KCMC* inaweza kusaidia kufikia hatua hiyo aliyoisema. Pia tusisahau, 98% ya mishahara ya *KCMC* inalipwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Utumishi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imetujengea kiwanda cha madawa pale Makambako, na kwa kuwa mitambo ya kutengeneza vidonge na kadhalika mashine hizo zipo, je, Serikali sasa itaanzisha lini kufunga mitambo hiyo ya kutengeneza vidonge, na *syrup* watu wa Makambako wanasubiri kwa hamu sana, na kwa sababu Makamu wa Rais alikuja akatoa maelekezo, ni lini sasa mitambo hiyo itaanza kufanya kazi? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli Mbunge wa Makambako sio tu amepigania kiwanda hicho toka ikiwa ni ardhi, ni pori ambalo lilikuwa halina kitu chochote. Leo ndani mle tuna kiwanda ambacho majengo zaidi ya matatu yaliyopo pale, na tayari kiwanda cha kuzalisha mipira kwa maana ya *glove* na vitu vingine, imeshaanza kufanya kazi na imeanza kutoa *products* ambazo zina-*supply* kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kweli, kama Mheshimiwa Mbunge anaposema kwamba kuna jengo lingine, lakini kuna mitambo tayari iko pale kwa ajili ya kuzalisha vidonge na *syrup,* kwa hiyo, kulikuwa na mchakato unaofanywa ndani ya Serikali kuona masuala ya nishati kwa sababu inahitaji nishati kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya kibiashara ili tutakapochukua vidonge kule Makambako tunapoingiza kwenye soko la kawaida tuweze kuwa *competitive,* namwomba Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo amekuwa akifuatilia na akija Wizarani, wiki ijayo Mheshimiwa Waziri atakuwepo hapa, tukutane mimi na yeye ili tuweze kuangalia kwa pamoja tunawezaje kujinasua pale, kwa kuwa tunataka tukizalisha vilevile mzunguko uwe mzuri au tuzalishe kwa ajili ya kusambaza tu kwenye hiyo kanda yake kama ambavyo alishauri siku ile tulipokuwepo na Makamu wa Rais pale. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Kassinge. *(Makofi)*

Na. 608

**Ujenzi wa Masoko ya Samaki – Kilwa Kusini**

**MHE. ALLY M. KASSINGE** aliuliza:-

Je, Serikali imefikia hatua gani katika ujenzi wa Masoko ya Samaki ya Kivinje na Somanga – Kilwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2025/2026, Serikali kupitia Halmashauri ya Kilwa ina mpango wa kujenga Soko la Samaki katika eneo la Kilwa Kivinje lenye thamani ya shilingi milioni 200.3 kwa kutumia fedha zake za ndani. Soko hilo litajumuisha ujenzi wa jengo la soko, chumba cha ubaridi, vizimba vya kuuzia samaki, ofisi, vyoo na stoo za kuhifadhia mazao ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka fedha 2024/2025 Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa kwa kushirikiana na Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani *(WWF)* inaendelea na ujenzi wa soko la samaki katika Mji Mdogo wa Somanga, ambapo, awamu ya kwanza ya ujenzi wa soko hilo liligharimu jumla ya shilingi milioni 44.4 na ujenzi huo ulijumuisha jengo la soko, vizimba vya kuuzia samaki na vyoo. Awamu hiyo ilikamilika na soko hilo lilianza kutumika kuanzia mwezi Februari mwaka 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili ya ujenzi wa soko hilo inatarajiwa kuanza muda wowote kuanzia sasa na utagharimu jumla ya shilingi milioni 232.9. Ujenzi huo utajumuisha ukamilishwaji wa chumba cha ubaridi, usimikaji wa mashine ya barafu, ujenzi wa ofisi, uwekaji wa marumaru na uwekaji wa umeme. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu. Nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni kuhusu ujenzi wa masoko ya samaki ya Kilwa Kivinje na Kilwa Somanga ambayo ni ahadi ya Serikali kupitia Wizara hii, iliahidi hapa Bungeni mwaka juzi 2023 wakati wa bajeti Mheshimiwa Ulega akiwa anawasilisha hapa. Hizo ambazo zimefanyika ni juhudi za halmashauri baada ya kuona uhitaji wa masoko upo, lakini fedha kutoka Serikali Kuu bado hazijafika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muktadha huo, je, Serikali sasa kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi iko tayari kushirikiana na

halmashauri ili kuwezesha fedha hizi kupatikana na hatimaye masoko haya ya samaki ya Kilwa Kivinje na Kilwa Somanga kujengwa kwa ukamilifu wake? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Tunaishukuru Serikali kwa ugawaji wa maboti kwa wavuvi wetu, lakini kulikuwa na awamu ya pili ya ugawaji wa maboti haya. Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi ya ugawaji wa maboti awamu ya pili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nimpongeze Mheshimiwa Ally Kassinge kwa kazi nzuri ambayo ameifanya kwa wananchi wake wa Jimbo la Kilwa Kusini, na vilevile kwa kufuatilia masuala yanayohusu uvuvi katika jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo moja tu nikiri kwamba Serikali tuko tayari kufanya kazi na Halmashauri na kuhakikisha fedha hizi zinatoka na ndiyo maana katika jibu la msingi tumesema tunatarajia kutoa shilingi milioni 232.9 muda wowote kuanzia sasa kwa ajili ya kuhakikisha Soko la Somanga linaanza kujengwa, lakini vilevile tunatafuta fedha kwa ajili ya soko hilo kwa hiyo ile ahadi itatekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuhusu suala la ugawaji wa maboti awamu ya pili, uko katika hatua za mwisho za utekelezaji. Muda wowote tutatangaza kama Wizara kutoa huo muda rasmi baada ya wale wakandarasi waliopewa kwa ajili ya ujenzi wa boti hizi kuzikamilisha, ili tuweze kuleta kwa wananchi na waweze kunufaika na mradi huo. Kwa hiyo, liko katika hatua za mwisho. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Bidya.

Na. 609

**Kutengeneza Skimu ya Nyanganga - Uvinza**

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kutengeneza Skimu ya Umwagiliaji iliyopo Kijiji cha Nyanganga Kazuramimba – Uvinza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali nchini ikiwemo miradi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa miradi ya Mgambazi, Kashangului, Nkonkwa na Ilagala iliyopo katika Wilaya ya Uvinza.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 imetenga bajeti kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu ya umwagiliaji ya Nyanganga Kazuramimba yenye ukubwa wa hekta takribani 600. Baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu wa skimu hiyo, Serikali itaanza taratibu za manunuzi ili kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bidyanguze.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu hii ya Nyanganga ilipelekewa fedha na kujengwa miaka kumi na saba iliyopita na haijatumika mpaka sasa. Je, ni lini sasa fedha zitapelekwa ili kukamilisha skimu hiyo ili wananchi waweze kuitumia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nimpongeze Mheshimiwa Bidyanguze, Mbunge wa Kigoma Kusini kwa kazi nzuri aliyoifanya katika jimbo lake na

kufuatilia hii miradi. Nikuondoe shaka, tunatambua kwamba miradi hii awali miaka ya nyuma ilikuwa inajengwa bila kufanya zile *study* za kina, na ndiyo maana unaona fedha zilikuwa zinakwenda na miradi haikamiliki kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alituelekeza tufanye usanifu wa kina kwenye miradi yote ili tuwe na gharama halisi ya ujenzi ili mradi unapoanza ukamilike, na ndiyo maana sisi tunachotaka ni kujenga skimu hii kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumeahidi hapa kwamba katika mwaka wa fedha huu 2025/2026 tutakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza kumpata mkandarasi ili aanze kujenga kisasa hiyo skimu ikamilike kwa wakati na ianze kunufaisha wananchi katika jimbo lake. Kwa hiyo, tupo katika hatua za mwisho za utekelezaji, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri kwa kutembelea Skimu za Umwagiliaji pale kwenye Jimbo la Vunjo. Tarehe 24 mwezi Julai, mwaka 2024 na katika ahadi alizotoa ni kwamba wangetuma wataalam kufanya usanifu kwa Skimu ya Soko iliyo kwenye Kata ya Kahe Mashariki. Naomba kujua suala hili limefikia wapi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo kwa kufuatilia mradi huu kwa muda mrefu, na ni kweli nilifika kule tarehe 24 mwezi wa Saba mwaka 2024 na moja ya ahadi ambayo tulitoa ni kupeleka wataalamu na wataalam walishafika kule. Sasa hivi wanachofanya ni kuandaa *paper* kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu ili sasa tuje kuujenga kama ambavyo Serikali imeahidi. Kwa hiyo, hiyo ndiyo hatua ambayo tuko sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo la Hai kumekuwa na skimu kubwa na mifereji ambayo inahudumia mashamba ya ushirika kwa wawekezaji, lakini kuwaacha wananchi wale ambao wanapitiwa na mifereji hiyo bila maji. Je, Serikali itatoa tamko gani kuhakikisha mifereji na skimu hizi zinazoenda kwa wawekezaji zinahudumia pia wananchi ambao wanabaki bila maji ya kumwagilia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nami ninampongeza tena Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai kwa kazi nzuri aliyoifanya katika jimbo lake kwa miaka mitano. Tunaamini kwa kazi nzuri aliyoifanya, basi atarejea tena katika hili Bunge Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, kabisa kwamba katika jimbo lake kuna hii miradi ambayo ameainisha hapa ambayo imekuwa ikipeleka maji asilimia kubwa kwa wawekezaji wakubwa na maeneo mengine kuwaacha wale wakulima wadogo ambao mifereji ile inapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli ya Serikali ni kwamba, miradi yote ya mashamba ya ushirika na ile ambayo inatokana na uwekezaji wa Serikali Kuu, inatakiwa yale maji yatumike kwa usawa kwa watu wote. Kwa hiyo, tunawaelekeza tu Maafisa Ugani wanaosimamia katika maeneo husika kuhakikisha wanasimamia hiyo haki ya mgawanyo wa maji kwa usawa kwa wananchi wote. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Festo.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wilaya ya Makete ina skimu moja ya Mwamlenge, ipo Kijiji cha Ruaha, Kata ya Mfumbi na tumeleta barua Wizarani ya kuomba shilingi 1,400,000,000.00 kwa ajili ya ukarabati wa skimu hii ili iweze kuleta tija kwa sababu ina hekta 520 ambazo zipo tayari kwa ajili ya kutumika. Je, ni lini Serikali italeta fedha ili wananchi wa Jimbo la Makete waweze kunufaika hususan Kata ya Mfumbi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea tena kumpongeza Mheshimiwa Festo Sanga Mbunge wa Jimbo la Makete, mmoja wa Wabunge mahiri ambao wamefanya kazi nzuri katika Bunge na kuwatetea wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu Mheshimiwa Festo kwamba tumepokea barua hiyo ya Skimu ya Mwamlenge ambayo inahitaji fedha takribani shilingi bilioni 1.4 na sisi kama Wizara tunatafuta fedha hiyo. Tutakapoipata, tunaamini ipo ndani ya uwezo wetu na tutaitekeleza. Kwa hiyo, niwathibitishie tu wananchi kwamba Wizara imepokea na fedha hiyo itatoka kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, skimu ya Minepa pamoja na Lupiro ni skimu ambazo zipo kwenye mpango wa kujengwa kwa muda mrefu, lakini mpaka sasa hivi hazijajengwa. Je, ni lini skimu hizi za Lupiro pamoja na Minepa zitaanza ujenzi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Morogoro ambaye amekuwa akipigania wanawake katika Mkoa wake. Nimthibitishie kwamba kweli ilikuwa katika mpango. Hatua tuliyopo sasa kwa skimu za Minepa na Lupiro tumeshamaliza usanifu wa kina, sasa tunasubiri kuanza kuitangaza tupate mkandraasi kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tupo katika hatua hiyo na tukishakamilisha, tutaanza ujenzi huo, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa na tunaendelea Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Makoa.

Na. 610

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi – Kondoa.**

**MHE. ALLY J. MAKOA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kondoa chenye hadhi ya Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa imeshatoa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 20,300 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi Wilaya ya Kondoa. Serikali inatarajia kujenga kituo kipya cha Polisi cha Daraja *"B"* kitakachogharimu kiasi cha shilingi 802,926,788.00 na fedha kwa ajili ya ujenzi zimetengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Makoa.

**MHE. ALLY J. MAKOA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa majibu mazuri na hatua Serikali waliyoifikia ya kukubali kutujengea Kituo cha Polisi katika Wilaya yetu, kwa sababu majengo yale yanayotumika ni kama makumbusho. Sasa, nina swali moja la nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo jengo wanalolitumia la ofisi lilivyo chakavu, pia makazi ya Askari wetu Kondoa ni chakavu sana na hayana hadhi ya kuishi binadamu. Sasa, Serikali ina mpango gani pia wa kuboresha makazi ya Polisi wetu pale Wilayani Kondoa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ina mpango wa ukarabati, pamoja na kuendelea na ujenzi wa vituo vya Polisi, inakwenda

sambamba na ujenzi wa makazi ya Askari wetu. Pia kwa yale maeneo ambayo majengo yake yamechakaa, Serikali ina mkakati wa kuanza ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Makoa, ni suala la kuingia kwenye bajeti mpya ya mwaka unaokuja, tutakwenda kuliangalia hilo suala la uchakavu wa nyumba hizo na ambazo baadhi ya maeneo, mpango kazi ni kuzivunja na kujenga nyumba nyingine mpya ambazo ni bora zaidi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mahakama ya Mwanzo Kumbululu ni Mahakama ambayo imechoka kabisa kwa uchakavu, maana yake ni ya muda mrefu sana. Je, ni lini Serikali itafikiria kuijenga upya Mahakama hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninalipokea suala la Mheshimiwa Mchungahela ili nifikishe sasa kwenye Mamlaka za Mahakama kuona mpango kazi waliouweka. Kimsingi swali la msingi lilikuwa linahusu ujenzi wa vituo vya Polisi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariki.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi. Tunaishukuru Serikali kwa kutuletea shilingi milioni 400 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Halmashauri ya Mpimbwe. Je, ni lini Serikali sasa itatuletea fedha ili tuweze kumalizia ujenzi huo, kwa sababu Kituo cha Polisi kinahitajika sana na hatuna kabisa? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mariki Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Katavi. Kituo cha Polisi Halmashauri ya Mpimbwe ndiyo Jimboni kwangu, ni Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kipolisi cha Mpimbwe. Kwa kweli tunamshukuru sana Mama Samia kwa kutuleta fedha zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katibu Mkuu analielewa suala hili na atapeleka fedha hizo haraka sana kwa ajili ya umaliziaji kwa sababu kituo kile kinahitajika hasa kabla ya uchaguzi wa mwaka huu, kuwe na Kituo cha Polisi chenye ngazi na hadhi ya Wilaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kutukumbusha kwenye eneo hili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza. Kwa niaba yake, Mheshimiwa Jesca.

Na. 611

**Uboreshaji wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU K.n.y. MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza: -

Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaongezewa uwezo wa kiteknolojia ili kumfikia kila mwananchi kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuliimarisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kulipatia vitendea kazi, ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, Serikali itatekeleza mradi wa ununuzi wa magari na vifaa vya kuzima moto na

uokoaji vyenye thamani ya Dola za Marekani milioni 100 kutoka kampuni ya *NAFFCO FZCO* iliyopo Dubai.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huo utawezesha kupatikana kwa vitendea kazi vya kisasa, ikiwemo vifaa vya mawasiliano, magari 150 ya zimamoto na uokoaji, magari ya kubebea wagonjwa 40, boti za kuzima moto na uokoaji 23 na *helicopter* moja ambavyo vitawezesha kuwafikia wananchi kwa wakati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jesca.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Katika wiki Mheshimiwa Pondeza katika Jimbo lake, moja ya changamoto kubwa aliyokutana nayo ni teknolojia duni na vifaa vinavyotumika katika uokozi katika Jimbo lake la Chumbwini. Je, mpo tayari katika vifaa hivyo kupeleka pia kwenye Jimbo hili kule Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Iringa Mjini pia ina uchakavu mkubwa wa magari katika Kikosi cha Zimamoto. Je, mpo tayari kutupatia katika sehemu ya vifaa hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, vifaa hivi mara vitakapofika lazima vitasambazwa mpaka Jimboni kwa Mheshimiwa Pondeza kule Chumbwini, na ni hakika kabisa vitalenga Makao Makuu ya Mikoa yote hapa nchini, ikiwemo Iringa ambayo vifaa vyake vimechakaa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malleko.

**MHE. ESTHER E. MALLEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Tunaishukuru sana Serikali kwa kutupatia gari la Zimamoto Moshi Mjini. Je, ni lini sasa Serikali itaweza kutujengea Jengo la Zimamoto kwa sababu lililopo sasa limechakaa sana? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango ambao Serikali imetoa kwa maana ya kupeleka gari jipya, bado sambamba na kupeleka vifaa, Serikali ina mpango wa kuanza kuweka miundombinu bora katika maeneo haya. Kwa hiyo, jengo la Zimamoto Mkoa wa Kilimanjaro ni moja kati ya mikakati ambayo Serikali imejiwekea kwenye kipindi kijacho cha fedha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea Wizara ya Maji. Mheshimiwa Malima.

Na. 612

**Kukamilika Miradi ya Maji Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Miradi ya Maji ya Kikombo - Ving'hawe hadi Mang'hangu na Idiro - Kisoka hadi Mazae itakamilika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima – Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji Kisokwe - Idilo - Mazae uliopo Wilaya ya Mpwapwa Mkoa wa Dodoma. Kazi zinazofanyika katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio la maji *(intake),* ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 200,000, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 35.5 sanjari na ujenzi wa vituo 20 vya kuchotea maji. Kukamilika kwa mradi huo kumewezesha wananchi zaidi ya 11,905 waishio kwenye vijiji

vitatu Kisoka, Idiro na Mazae kuanza kunufaika na huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua nyingine, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/2026 itaanza utekelezaji wa mradi wa maji Ving'hawe - Mang'hangu ambapo utahusisha ujenzi wa nyumba ya mitambo *(pump house),* ujenzi wa tanki lenye ujazo wa lita 200,000 sambamba na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 11.5. Mradi huo unatarajiwa kutekelezwa ndani ya miezi 12 ambapo unalenga kunufaisha zaidi ya wananchi 5,000 waishio Mji wa Mpwapwa, ninakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi huu wa Kisoka – Mazae – Idiro, lakini kuna mradi wa kupeleka maji katika maeneo kuanzia Idiro kwenda Chamnye mpaka Visele.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu utekelezaji wake unasuasua sana. Hapa tunapoongea ni 14% ya utekelezaji wake imekamilika. Je, ni lini Serikali itakamilisha mradi huu ili wananchi wa maeneo haya niliyoyataja waweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza sana Mheshimiwa George Malima kwa mradi ule wa kwanza ambao yeye pamoja na Ofisi ya Mheshimiwa Waziri hasa Mheshimiwa Aweso pamoja na Mheshimiwa Kundo walifanya kwa pamoja na kuweza kuhakikisha walau mradi unatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu huu Mradi wa Idiro – Chamnye pamoja na Isele kumekuwa na mtekelezaji wa mradi huu ambaye ni Mkandarasi, ameanza kufanya kazi hiyo. Ninatambua eneo hili lina pande mbili. Upande wa Serikali ni kuingia mkataba na Mkandarasi ili kazi hiyo iweze kufanyika. Pia

tunao wajibu wa kuweza kumlipa Mkandarasi kwa wakati. Hatua ya pili ni Mkandarasi kutekeleza wajibu wa kimkataba kwa mujibu wa tarehe zilizopangwa za kimkataba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa suala hili nimwambie tu Mheshimiwa George Malima nimhakikishie kwamba, tutalisimamia, na Katibu Mkuu amelisikia, na hivyo tutaenda kufanya ufuatiliaji ili kila mmoja katika upande wa mkataba atekeleze wajibu wake, wananchi waweze kunufaika na huduma ya maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtaturu.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika Jimbo la Singida Mashariki tumechimbiwa maji katika maeneo mbalimbali, tuna visima na vyanzo vya maji katika maeneo mbalimbali, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo bado hayajawekewa miundombinu ikiwemo Kijiji cha Ujaire ambacho tayari tuliambiwa Mkandarasi ameshapatikana, lakini bado hajaanza kazi. Je, ni lini sasa, Mkandarasi huyu ataanza kazi katika Kijiji kile cha Ujaire?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lini Mkandarasi ataanza kufanya kazi, hilo ni jambo la ufuatiliaji na Katibu Mkuu Wizara ya Maji atalifanyia kazi. Mara baada ya swali hili, tutakuwa tumempatia *specific date* ya Mkandarasi kuanza kufanya kazi, kwa sababu jambo zuri ni kwamba tayari Mkandarasi amepatikana. Kwa hiyo, ni suala la kuanza kutekeleza mkataba mahsusi kulingana na tarehe zilizopangwa za utekelezaji wa mradi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi. Nianze kwa kuishukuru Serikali kwa kupeleka shilingi milioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa

zahanati pale Kisaula, lakini wananchi hawa wana adha kubwa sana ya maji. Je, kwa kuwa Serikali tayari ina mtambo kila Mkoa, nini maelekezo yako kwa *RUWASA* ili waweze kutafuta mafuta na wananchi wale waweze kuchimbiwa kisima? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwanza mpango ulivyo na sera ya utekelezaji wa miradi ya maji, tunaangalia sana kwenye maeneo na vipaumbele tunaviweka kwenye maeneo ambayo yanagusa wananchi wengi au maeneo ya *public,* ambapo zahanati ni sehemu mojawapo ya sehemu muhimu ya utoaji huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia suala hilo, na kwa sababu mitambo imeendelea kuwepo na kuendelea kuchimba visima ambavyo Mheshimiwa Rais alinunua mashine hizi kuwasaidia wananchi, suala hili la Mheshimiwa Kamonga, nikitoka hapa nitawasiliana na Katibu Mkuu ili tuweze kuona ni namna gani haraka sana wananchi waweze kupewa huduma ya maji katika zahanati hususan wananchi wote katika eneo hilo alilolitaja, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipatia fursa. Kata ya Kimochi hasa eneo la Sango lina uhaba mkubwa wa maji. Je, Serikali ina mkakati gani kutupelekea maji katika Kata hii? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwa kazi nzuri anayofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili ambalo amelisema kwenye Kata ya Kimochi, tutatuma wataalam kupitia Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Maji, *Engineer* Mwajuma, ananisikia, ninatoa tu maelekezo kwamba atume wataalam kwa ajili ya kwenda kufanya *study* ili kujua katika kipindi cha mwaka wa fedha walau ujao wa bajeti tuweze kutoa huduma hii muhimu kwa wananchi wa Kata ya Kimochi katika Jimbo la Moshi Vijijini kwa Mzee wangu Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mpakate.

**MHE. DAIMU I. MPATAKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru. Mradi wa Mchoteka, mradi wa Msinji na mradi wa Tuwemacho imesimama kutokana na tatizo la fedha. Ni lini Serikali itawalipa Wakandarasi hawa ili miradi ile iweze kuendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCHAL P. KATAMBI) K.n.y. WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna maeneo ambayo Wakandarasi wamekuwa wakifanya kazi, jambo la kwanza ni kumshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa sababu miradi hiyo tayari imeshaanza kufanyiwa kazi. Changamoto iliyokuwepo ni hayo malipo ya wakandarasi ambayo tayari tumeshasikia kwa mpango mzuri wa Serikali kwenye bajeti hii ya Serikali ambayo tunaenda kuipitisha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameshasema maeneo mengi ambayo yalikuwa hayajalipwa fedha kwa wakandarasi imewekewa mpango maalum na bajeti hiyo itawekwa kwa ajili ya kuweza kulipa ili waweze kukamilisha kazi ambazo zimekusudiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha. Nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge, ninaona kipindi hiki maswali ya nyongeza yamekuwa ni machache sana na uchache wake unakuja kwa sababu Majimbo mengi miradi imekamilika. Hii ni kazi ya Serikali ya Mama Samia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hivyo siyo vibaya Mbunge ukisimama kwenye maswali ya nyongeza ukapongeza Serikali

kwa namna miradi ilivyokamilika. Vilevile, ukasimama ukasema bado kuna changamoto kwenye eneo lako ili Serikali ikuletee huduma hiyo, na wananchi wako wafurahi. Sasa ukikaa tu, unakaa tu, "hatuchezi, hatuchezi!" Ulizeni maswali ya msingi ya wananchi. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ambao wapiga kura wake kutoka Jimbo la Kibakwe, Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 22 wa Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Afya ambao ni wanafunzi wa mwaka wa Nne wanaosomea Udaktari Chuo cha Mt. Francis kutoka Ifakara, Mkoani Morogoro. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni watatu wa Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga ambao ni jamaa zake aliosomanao Shule ya Msingi Ludewa Mkoani Njombe. *(Makofi)*

Wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka ambao ni familia yake kutoka Chunya Mkoani Mbeya, wakiongozwa na mke wake, Ndugu Agness Mgongo. *(Makofi)*

Wapo wageni 46 wa Mheshimiwa Mussa Ramadhani Sima ambao ni wachezaji na viongozi wa Timu ya Mpira wa Miguu ya *Singida Big Stars.* Timu hii imeshika nafasi ya nne Ligi Kuu na inatarajia kucheza Fainali ya *CRDB Federation Cup* na Timu ya Klabu ya *Young Africans*. Timu hizi nyingine kuzitajataja nazo! Haya. *(Vicheko/Makofi)*

Tunao wageni 11 wa Mheshimiwa Tumaini Magessa ambao ni Waenezi Kata wa CCM kutoka Jimbo la Busanda Mkoani Geita. *(Makofi)*

Wageni 15 wa Mheshimiwa Miraji Mtaturu na Mheshimiwa Elibariki Kingu ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Siasa kutoka Wilaya ya Ikungi Mkoani Singida wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya, Ndugu Mika Likapakapa, karibuni. Ninaona mmekuja, basi pamoja na timu yenu, hongereni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 48 wa Mheshimiwa Mpakate ambao ni wanafunzi na walimu wa Klabu ya Watoto Wasomaji wa Vitabu na Kujifunza kwa Matendo, kutoka Mkoani Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Wanakwaya ya Vijana wa Kanisa la KKKT Usharika wa Kisasa kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wapo wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Upendo Moreto kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania, Makao Makuu Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 45 na walimu sita wa Shule ya Msingi *Marangu Hills* kutoka Marangu Mkoani Kilimanjaro. *(Makofi)*

Tunao pia wanafunzi 53 na walimu nane wa Shule ya Msingi *Blessed* kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Katibu.

**17 JUNI, 2025**

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, majadiliano yanaendelea. Tunaanza na Mheshimiwa Kakunda, wajiandae Mheshimiwa Neema na Mheshimiwa Gambo.

Mheshimiwa Kakunda hayupo. Tunaendelea na Mheshimiwa Neema, wajiandae Mheshimiwa Gambo na Mheshimiwa Suma.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia katika Bajeti Kuu ya Serikali. Ninapenda nianze kwa kuipongeza sana Serikali chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo inaendelea kufanywa kuhakikisha kwamba uchumi wa Tanzania unaendelea kukua, hali kadhalika sisi kama Watanzania tunaendelea kupata maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nijielekeze kwenye mchango wangu na moja kwa moja nitaanza na eneo la kwanza la kutanua wigo wa walipakodi. Tunapoongelea kutanua wigo wa walipakodi, hapa tunaongelea maeneo mawili; eneo la kwanza ni kuongeza idadi ya walipakodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapenda kurejea kuikumbusha Serikali kwamba, katika kila shilingi 10 ambayo inazunguka kwenye uchumi wa Tanzania, shilingi sita ipo kwenye sekta isiyo rasmi. Hivyo ni muhimu sana Serikali iweke jitihada thabiti kuhakikisha tunarasimisha biashara ambazo zipo kwenye sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninaiomba sana Serikali, pamoja na kwamba iliweka miezi sita ya likizo ya kulipa kodi kwa biashara ndogo ambazo zinaanzishwa, naomba sana Serikali ione namna ya kubadilisha sheria ili biashara zinazoanzishwa na vijana, wanawake, na watu wenye ulemavu wapate likizo ya kulipa kodi kwa angalau miaka mitatu, kwa sababu wawekezaji kutoka nje wanapata likizo ya kulipa kodi mpaka miaka mitano. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kutanua wigo wa walipakodi kwa kuingiza kundi kubwa la walipakodi ambao hivi sasa hawamo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kujielekeza kwenye aina ya pili ya kutanua wigo wa walipakodi. Aina ya pili ni kutambulisha aina mpya za kodi ambazo zilikuwa hazitozwi hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninarejea mfano mwaka 2021, mimi nilipendekeza hapa Bungeni kwamba Serikali ianze kutoza Kodi ya Huduma za kidijiti, *(Digital Service Tax)*. Baada ya Serikali kufanya uamuzi huo, tokea Februari mwaka 2022 mpaka Machi mwaka 2025, Serikali imeweza kukusanya kodi takribani shilingi bilioni 48, kodi ambayo Serikali ilikuwa haiipati hapo awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa msingi huo huo Serikali imetambulisha kutoza kodi ya *Withholding Tax* 10% kwenye *retained earnings*. Ninaomba nitoe darasa kidogo, pale ambapo biashara inakuwa imepata faida, tuseme mathalani faida shilingi 1,000,000.00, Serikali itatoza kodi ya 30% ya hiyo faida ambayo itakuwa ni shilingi 300,000.00. Kampuni itabaki na shilingi 700,000.00 ambayo inakwenda kwa wanahisa kwa maana ya *dividends*. Sasa, kinachotokea na pale ambapo mwanahisa atapokea *dividend,* anapaswa kisheria alipe *Withholding Tax* ya 10%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachofanyika hivi sasa ni kwamba, baadhi ya kampuni badala ya kupeleka ile shilingi 700,000.00 nzima kwa wanahisa, inachofanya ni labda inapeleka shilingi 300,000.00 tu, halafu kampuni inasema kwamba shilingi 400,000.00 inabaki kwenye kampuni kwa ajili ya *reinvestment*, kitu ambacho kinaruhusiwa kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu nao ni mwanya wa kukwepa kodi kwa sababu, ile shilingi 400,000.00 ambayo inakuwa imebaki kwenye kampuni kama *retained earnings* hairejeshwi katika kampuni katika minajili ya *reinvestment*. Badala yake zipo kampuni ambazo wanairejesha fedha ile kwa wanahisa, *(shareholders)* lakini kwa njia mbadala kama vile kununua magari ya kifahari, kulipia ada za watoto shule, au kuwapa posho za safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya hivyo ni kutumia mwanya katika sheria kukwepa kodi, kwa sababu lazima ukweli usemwe, pale ambapo unaamua kubakiza kiasi cha faida ili uendelee kukuza biashara na kukuza mtaji, zipo gharama ambazo zinapaswa zikubalike kama *reinvestment,* na zipo gharama ambazo haziwezi kukubalika kama *reinvestment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaamini ni katika minajili hiyo ndiyo maana Serikali imeamua kupendekeza kwamba pale ambapo kampuni itakaa na hii *retained earnings* kwa zaidi ya miezi sita na haijafanya hiyo *reinvestment*, basi itatozwa kodi hiyo ya 10% ya *Withholding Tax*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niishauri Serikali kwamba, badala ya kufanya hivyo, Serikali kwanza iongeze muda iwe ni takribani mwaka mmoja. Pia, Serikali iainishe ni aina gani ya gharama ambazo zinakubalika kama *reinvestments*. Hiyo itasaidia kuondoa hii mianya mingine na kiwango hicho ama aina hizo za gharama zinazokubalika, ziwe ni kwa kibali cha Kamishna wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo itasaidia kuhakikisha kwamba kampuni ambazo zinabakiza kiwango kile cha faida kama *retained earnings,* zitatumia fedha hizo kwa ajili ya *reinvestment* kwa maeneo yanayokubalika, na siyo maeneo ambayo yanatumika kama mwanya wa kukwepa kodi.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la pili, ninaipongeza sana Serikali kwa jitihada kubwa ya kuandaa bajeti ambayo imezingatia namna ambavyo Serikali itaweza kuhimili mabadiliko ya fedha kutokana na wahisani wetu kutoka nje ya nchi kupunguza misaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba, pia kutokana na taswira na mabadiliko ya fedha za wahisani kutoka nje ya nchi kuja hapa Tanzania pamoja na Mataifa mengine, ni lazima Serikali ifunge mkanda ipunguze gharama zisizo za lazima katika bajeti yake *(Non-Essential Costs)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ningependa kuishauri Serikali ione namna ya kufanya tathmini ya gharama zake zote ili iweze kuondoa gharama ambazo siyo za lazima. Nitatoa kwa mfano, mathalani, tukiacha viongozi wetu wakuu wa nchi, hata jambo hili Mheshimiwa Spika, Dkt. Tulia Ackson alishawahi kulisemea Bungeni; utakuta magari ya Serikali yanaweza yakakaa yananguruma hata saa zaidi ya nne mpaka tano. Serikali inaingia gharama ya mafuta pasipo ulazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali ikafanye tathmini ya gharama zake za uendeshaji na iweze kuondoa *Non-Essential Costs* ili fedha hiyo iweze kwenda kuelekezwa kufidia katika maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa kutokana na mabadiliko ya fedha za misaada kutoka kwa wahisani wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, halikadhalika Serikali ikishafanya hiyo tathmini, itueleze Watanzania ni wapi ambapo inakwenda kupunguza hizo gharama za *Non-Essential Costs* na hizo fedha zinaelekezwa kwenye kufidia katika eneo gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la tatu, ninapenda kurejea kidogo. Hapa Bunge lako Tukufu, katika wiki zilizopita tumepitisha bajeti za Wizara kadhaa kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ninarejea tu, Wizara ya Maendeleo ya Jamii tumepitisha shilingi bilioni 76, Wizara ya Afya tumepitisha shilingi trilioni 1.6, na Wizara ya Elimu tumepitisha shilingi trilioni 2.4. Nimefanya rejea hii kwa sababu sekta ya *NGOs* tunachangia kwa

kiwango kikubwa sana kutekeleza afua mbalimbali katika sekta tofauti ikiwemo sekta hizi, jambo ambalo linachangia kwa kiasi kikubwa kwenye maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikifanya rejea ya mwaka 2024 tu, sekta ya *NGOs* imeweza kuingiza nchini takribani shilingi trilioni 2.61 ambazo zimeelekezwa kwenye afua mbalimbali katika sekta tofauti, ikiwemo sekta hizi nilizozitaja. Kama sekta ya *NGOs* kwa mwaka 2024 pekee imeweza kusaidia na kuingiza nchini shilingi trilioni 2.61, hii ni zaidi ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, zaidi ya bajeti ya Wizara ya Afya, na ni zaidi ya Bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya *NGOs* bado inapata changamoto kubwa sana. Katika Sheria ya Kodi ni kwa bahati mbaya sana kwamba *TRA* imeshindwa kutofautisha kati ya biashara na *NGO*. Hivi sasa *TRA* inatambua *NGOs* kama ni biashara, jambo ambalo linaleta changamoto kubwa na mkanganyiko mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naiomba sana Serikali kwa kutambua kwamba tayari Tanzania imepata mtikisiko ambao Serikali inajitahidi kuuhimili kufuatia mabadiliko ya fedha za wahisani. Sekta ya *NGO* ni lazima sasa itambulike kwa utofauti. Sekta ya *NGO* siyo biashara, *NGOs* haziingizi faida, *NGOs* zinatoa msaada.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu sasa Sheria ya Kodi ibadilishwe ili itofautishe kati ya *NGOs* na biashara. Hivi ni vitu viwili tofauti, na kuendelea kuvitambua kama ni kitu kimoja ni kuendelea kufifisha jitihada ambazo kwa wakati huu tuliopo sasa tunahitaji sana *NGOs* ziendelee kutafuta fedha kutoka kwa wahisani ili tuweze kuendelea kuchangia na kufidia yale mapengo ambayo tayari yameshaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba sekta hii ya *NGO* ina mchango mkubwa sana wa kusaidia Serikali kufidia *gap* ambalo tayari lipo. Kwa sababu nikirejea tena, mwaka 2024 pekee sekta ya *NGO* imeweza kuingiza nchini takribani shilingi trilioni 2.61, ambayo ni zaidi ya bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya

Jamii; ni zaidi ya bajeti ya Wizara ya Afya; na ni zaidi ya bajeti ya Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninaiomba sana Serikali ifanye maboresho ya sheria ili *TRA* watambue *NGOs* siyo biashara, *NGOs* haziingizi faida, hazifanyi biashara, hivyo ziwe tofauti na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo langu la tatu ni kwamba ninaendelea kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ambazo inafanya, lakini ni muhimu sana tuone namna ambavyo tutaendelea kulea na kuweka mazingira wezeshi kwa sekta ya *NGO* ili iweze kushamiri na iweze kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuhitimisha, ninaomba nirejee katika Ilani Ibara ya 34(E) na kwa kusoma kwa haraka haraka inasema kwamba, "Chama cha Mapinduzi kinakwenda kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia tafiti na huduma za lishe nchini."

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafurahi sana kwamba aliyekuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kuandaa Ilani ya Chama cha Mapinduzi alikuwa ni Waziri Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, lakini cha ajabu ni Waziri huyu huyu chini ya Wizara hii hii ambaye amekwenda kufuta Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninajiuliza, je, Serikali ambayo iko chini ya Chama cha Mapinduzi itatekeleza vipi Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi 2025 – 2030, ikiwa Serikali imeamua kufuta Taasisi ya Chakula na Lishe ilhali Chama cha Mapinduzi kinaelekeza kwenye Ilani hii ya Uchaguzi 2025 – 2030 kwamba Chama cha Mapinduzi kinakwenda kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kuimarisha tafiti na huduma za lishe nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, kwa unyenyekevu mkubwa sana nimwombe sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo afanye rejea uamuzi alioufanya na uamuzi huo aufute na kuturejeshea Taasisi ya Chakula na Lishe *(TFNC)* ili tuweze

kutekeleza maelekezo yaliyowekwa kwenye Ilani hii ya Chama cha Mapinduzi 2025 – 2030. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana kwa fursa, na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kwenye hoja yako ya Serikali kupunguza gharama katika uendeshaji wake, Chama cha Mapinduzi kimeshaielekeza Serikali kwenye Ilani yake kuwa izingatie matumizi ya *CNG* kwenye magari yote ya Serikali.

Kwa hiyo, hiyo peke yake ni hatua kubwa ambayo imefanywa na Chama cha Mapinduzi na itapunguza matumizi hayo, na fedha nyingi zitarudi kwa wananchi kuwapelekea maendeleo yao. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mheshimiwa Gambo, wajiandae Mheshimiwa Suma na Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitatumia fursa hii kuzungumza kwenye maeneo matatu. Eneo la kwanza itakuwa kuhusiana na malipo au maslahi ya Wenyeviti wa Serikali za Mitaa; eneo la pili ni madai ya wafanyakazi waliokuwa wanafanya kwenye viwanda vya *Fibreboards*, *General Tyre*, *Kilitex, TANALEC,* na *TPI*, na mwisho nitamaliza na shukrani kwa yale ambayo tumefanyiwa kwenye Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenyeviti wa Serikali za Mitaa ndiyo msingi wa uongozi katika nchi hii. Ndiyo viongozi ambao Serikali ikitoa maelekezo yoyote, iwe kukusanya Kodi ya Majengo, kama sasa hivi wanapita nyumba kwa nyumba kuhakikisha kwamba wanatambua nyumba zilizopo, wanapiga picha ili mwisho wa siku Serikali iweze kukusanya kodi kwenye sekta hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande wa Jiji letu la Arusha ambalo tunakusanya zaidi ya shilingi bilioni 45, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa anapewa shilingi 100,000.00 tu kwa mwezi. Pia, hata kazi nyingine akizifanya wakati mwingine unakuta hata posho hapati kulingana na mzigo ambao anaubeba. Mwananchi akipata changamoto sijui ya Polisi anahitaji kupitia Serikali ya

Mtaa, akiwa ana shida sijui ya ardhi anahitaji kupitia Serikali ya Mtaa, lakini anachokipata hakiendani na mzigo anaoupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kibaya zaidi, pamoja na kupewa kiasi kidogo cha shilingi 100,000.00 kwa mwezi, na chenyewe pia hawapewi kwa wakati. Kwa mfano, sasa hivi wanadai mwezi wa Nne na mwezi wa Tano, na wako wengine ambao hawajalipwa toka mwezi wa Tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa, nilidhani kwa sababu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali ambayo inawajali Watanzania, na sisi wengine wote ukiangalia Waheshimiwa Wabunge ikifika wakati tunapata mishahara yetu kwa wakati, tunapata posho kwa wakati. Pia, Waheshimiwa Madiwani wanapata mishahara kwa wakati na wanapata posho kwa wakati; watumishi wa Umma Mheshimiwa Dkt. Samia anawalipa kwa wakati, lakini changamoto ni kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba wanaohusika na kusimamia Serikali za Mitaa wahakikishe kwamba maslahi yao yanapatikana kwa wakati ili wapate morali ya kuendelea kufanya kazi, kwa sababu tayari Mheshimiwa Dkt. Samia ametafuta fedha kwa ajili ya kuwalipa hawa. Changamoto iliyopo ni kwenye usimamizi katika ngazi zetu za chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi, pia sisi ambao tunachaguliwa kama Madiwani, na Wabunge, baada ya miaka mitano tunapata *gratuity* (kiinua mgongo), lakini Wenyeviti wa Serikali za Mitaa hawapati chochote. Wakifanya kazi wakimaliza wanaenda zao, watakaorudi sawa, ambao hawajarudi sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata kwa Jiji la Arusha kwa ambao walimaliza kipindi chao kilichopita, hata posho yao ya shilingi 100,000.00 tu, hivi tunavyozungumza wako baadhi mpaka leo hawajaweza kupata. Kwa hiyo, tungependa Serikali kwa kweli itusaidie kusimamia ili Wenyeviti hawa waweze kupata maslahi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa pia kwenye bajeti hii ya Serikali, badala ya kuwalipa kwa shilingi 100,000.00 tu kwa sababu mapato tunayo mengi; kama Jiji la Arusha ukienda Mkoa kama wa Dar es Salaam majiji yote yale, ukienda Mbeya na maeneo mengine, nilikuwa ninadhani wangelipwa angalau shilingi 300,000.00 kwa mwezi, ingeweza kuwasaidia kupata nauli na masuala madogo madogo ya kupambana na changamoto nyingine kwenye maeneo kama hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, sisi tukilipa shilingi 300,000.00 tu kwenye viti 154, tutatumia kama shilingi 554,400,000.00, kitu ambacho nina uhakika kiko ndani ya uwezo wetu sisi kama Jiji la Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo pia, nadhani nilisemee ni kuhusiana na madai ya waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha *Fiberboard*, *General Tyre*, *Kili Tex*, *TANELEC* pamoja na *TPI,* wamefanya kazi kubwa na nzuri kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, hawa wafanyakazi wa Kiwanda cha *Fiberboard* wapo 353 ambao kwa tathmini yao waliyoitoa wanasema wanadai kama shilingi bilioni tisa, wanatakiwa walipwe na Serikali, lakini kila siku wanaambiwa andika hiki, lete hiki, tutakuja kuhakiki, tutafanya hivi na mwisho wa siku mpaka leo hakuna ambacho kinapatikana toka mwaka 1998.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tuna wafanyakazi wa *General Tyre* 317 ambao wameniambia mpaka sasa hivi kati ya 317 wafanyakazi 72 wamefuatilia mafao yao, haki zao, mpaka wengine wamefariki. Mwisho wa siku, mpaka leo hata hakuna ambacho kimepatikana. Pia, kuna Kiwanda cha *KILITEX*, Kiwanda cha *TANALEC* pamoja na Kiwanda cha *TPI*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninapenda kwa kweli, Wizara ya Fedha watusaidie kuja na majibu yanayoeleweka. Je, ni lini hawa waliofanya kazi kwenye viwanda hivi vitano nilivyovitaja watapata haki zao?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho wa siku malipo yao yapatikane, ili nao waendelee kusomesha watoto wao na pia, kuendelea na maisha yao ya kila siku. Nafahamu mara kwa mara imekuwa inatumwa timu inakwenda kwa ajili ya uhakiki, lete taarifa ya hiki, lete habari hizi; wakati Serikali inabinafsisha hivi viwanda au viwanda vinapokuwa vinaondoka naamini wanazo taarifa za kutosha za watu hawa na unakuta mishahara ya kipindi kile ilikuwa ni midogo. Sasa mpaka hivi tunavyozungumza, ukitaka kuwalipa, je, utawalipa kwa mshahara gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, mshahara wa mwaka 1998, mshahara wa mwaka wa nyuma zaidi kwa sababu, hela ingekuwa benki ingekuwa hata na riba. Kwa hiyo, tunadhani kwamba, hata kuja kuwalipa, pamoja na kuangalia mishahara ya kipindi kile, basi Serikali iangalie na hali halisi ya maisha ya sasa, ili wanapokwenda kuwalipa, basi wapate kitu ambacho kitaweza kuwasaidia kupambana na hali yao ya maisha, na mwisho wa siku waendelee kuwa na furaha na nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi namfahamu Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni mtu mwenye upendo na mapenzi kwa Watanzania. Mambo yote yaliyokuwa magumu kipindi cha Dkt. Samia Suluhu Hassan yameweza kutekelezeka, hata madai mengine ambayo kipindi cha nyuma yalikuwa hayawezekani, kipindi cha Dkt. Samia Suluhu Hassan, yametekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na madai hapa, hata wale wenye vyeti *fake* yalionekana ni mambo ambayo hayawezekani, lakini kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hoja zilikuja hapa ndani ya Bunge na tumeona yamefanyiwa kazi na wameweza kulipwa. Huko waliko sasa hivi wana furaha na mambo yanakwenda vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nawaomba Wizara ya Fedha tunapokuja kuhitimisha kwenye Bajeti Kuu hii ya Serikali, tuhakikishe kwamba, tunalifanyia kazi suala hili na wapate majibu kwamba, je, ni lini watalipwa? Wameitwa kila siku, taarifa zimechukuliwa na timu zimetumwa zimeenda. Wanachotaka wao, baada ya kazi yote hiyo, wapate haki yao na masuala mengine yaweze kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwa muda wa miaka mitano tumekaa ndani ya Bunge hili, tumejenga hoja kwenye masuala mbalimbali ya maendeleo. Nataka nitumie fursa hii kwa kweli, kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa sababu, kila hoja yenye masilahi kwa wananchi tumeona namna ambavyo ameifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na hoja hapa ya *bureau;* karibuni zote zilikuwa zimefungwa. Tukasema sisi watu wa utalii kule Arusha unapofunga *bureau* na ile biashara ni ya dola, changamoto inakuwa ni kubwa zaidi. *Bureau* zilifungwa, kuna baadhi ambao hela zao zilichukuliwa, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipewa kilio kile, akaweza kusimamia jambo hilo na hivi tunavyozungumza zile *bureau* zimefunguliwa. Gharama za kuchukua leseni zilipandishwa, zile gharama zimeshushwa na wale ambao walichukuliwa fedha zao Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alielekeza zenyewe pia, zimeweza kurudishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao hela zao bado hazijarudishwa zote. Wengine walipewa nusu na wengine robo. Tunaomba Wizara ya Fedha, sababu tunajua hata Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa maelekezo hayo, waende wakasimamie basi na wale wachache waliobaki wamaliziwe hela zao, mambo yaende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili kwa kweli naomba nimpongeze sana Waziri wa Fedha, ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba; pia, nampongeza Naibu Waziri wake wa Fedha kwa kazi kubwa na nzuri walioifanya ya kusimamia ipasavyo maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninashukuru, tumezungumza kila siku hapa kuhusiana na malipo ya fidia kwa wenzetu waliopo Moshono kule. Kila tukizungumza, wanasema yatafanyiwa kazi, lakini tunashukuru sana kwa kweli, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameweza kuielekeza Wizara ya Fedha ikashirikiana na Wizara ya Ulinzi, zimetolewa zaidi ya shilingi bilioni mbili, kwa ajili ya

kuwalipa wananchi ambao walikuwa wana mgogoro na Jeshi kule kwenye Kata ya Moshono.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ninavyozungumza, fedha zimeshafika tayari Jiji la Arusha na wananchi wapo pale, kwa ajili ya utaratibu wa kuweza kupata fedha zao, mpaka *vendor form* wameshajaza tayari, wanasubiri taratibu za kawaida tu kupata fedha zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba msimamie halmashauri hela zitoke kabla mfumo haujafungwa. Wasije wakachelewa ikafika tarehe 30 mfumo ukafungwa, halafu wananchi wakakosa haki yao wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshafanya kazi na wasaidizi wake mmemsaidia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru pia, katika hili eneo mmetulipa Moshono, Jiji la Arusha, sawa, lakini mmesahau Kata ya Mlangarini na Kata ya Nduruma. Tunaomba na wenyewe pia, japokuwa ni wilaya au jimbo lingine kwa sababu, ulikuwa ni mgogoro mmoja, naomba na wenyewe pia, jambo hili likafanyiwe kazi mambo yaende vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru pia, Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametupatia shilingi bilioni 48, kwa ajili ya Chuo cha Uhasibu Arusha kupitia Mradi wa *HEET* ambao unakwenda kuboresha kile chuo. Wanajenga chuo kingine Songea, lakini pia, wanaboresha chuo kingine cha kule Babati. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi hiyo na tunampongeza Mkuu wa Chuo, Prof. Sedoyeka kwa kweli, kwa usimamizi mzuri wa fedha hizo. Ukienda pale chuo kimebadilika kabisa kwa sababu, na mimi nilisoma pale, nafahamu chuo kilivyokuwa siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pia kwa ajili ya mradi wa *TACTIC*. Tulikuwa na kilio cha muda mrefu, hatuna stendi ya kisasa, hatuna masoko mazuri, hatuna barabara nzuri, lakini kupitia mradi wa *TACTIC,* Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anakwenda kutujengea stendi ya kisasa Jiji la Arusha, anatujengea soko jipya Kwamrombo, pamoja na soko lingine pale Kilombero. Hivi

tunavyoongea, tenda imetangazwa, mkandarasi amepatikana, na tayari amekabidhiwa *site* kwa ajili ya kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Katika miaka hii mitano, wema aliotutendea tutakwenda kumlipa kwa kumpa kura za kutosha kwa sababu matendo yanaongea zaidi kuliko maneno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi wa *TACTIC* unakwenda kujenga barabara za lami; Barabara ya Engosheraton, kilometa 4.8 na Barabara ya Olasiti, kilometa nne. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye mambo hayo. Pia, tunamshukuru kwa kutujengea Uwanja wa *AFCON,* shilingi bilioni 286.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kujengewa tu ule Uwanja wa *AFCON,* tayari kule viwanja eka moja ilikuwa pengine ni shilingi milioni 15 au 20, leo chini ya shilingi milioni 60 haupati eka moja pale. Kwa hiyo, hata thamani pia imeongezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anakwenda kutujengea barabara ya lami pia ya Njoro; kutoka pale Njoro kwenda kwenye uwanja wa mpira hadi kufika kule kwenye eneo la stendi. Naomba tumshukuru sana na tumpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kazi kubwa ambayo anatufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia hiyo pia, tunaenda kujengewa viwanja vidogo vidogo vingine. Leo kwa mfano, kuna mkataba utasainiwa pale kujenga Uwanja wa Mpira wa *Arusha Sports and Games Academy*. Huu uwanja ni matokeo ya Dkt. Samia Suluhu Hassan kuleta mashindano ya *AFCON* na bado kupitia wenzetu wa *TFF* tumependekeza maeneo ya kujenga viwanja vingine vidogo vidogo; kuna Uwanja wa Gymkhana, Uwanja wa Soweto, Uwanja wa *General Tyre*, Uwanja wa ESAMI na pia, Uwanja ule wa Polisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, tumejengewa shule mpya za sekondari, mpya kabisa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga Shule ya Sekondari *Unga Limited*, amejenga kule Muriet Mlimani, amejenga kule Moshono, amejenga kule Olmoti,

kule Mirongoine, amejenga Sekei na anajenga nyingine eneo la Bondeni. Katujengea shule mpya za msingi, tena za ghorofa; amejenga *NAFCO* kule Kata ya Olmoti, kule Msasani A na B na nyingine kule Lemala. Kwa hiyo, ukiangalia hata sekta ya elimu ameiona.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda sekta ya afya ndiyo usiseme. Mount Meru, zamani kabla ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ilikuwa mtu akienda hospitali *X-Ray* peke yake anaambiwa nenda hospitali ya *private* ka-*check* halafu njoo hapa. Leo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kapeleka *X-Ray* mbili, ya *digital* na *analogy,* watu wanapata huduma pale na amewapelekea *CT-Scanner,* kaibadilisha ile hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anajenga vituo vya afya vipya. Nenda sokoni Ywami, nenda kule kwenye Kata ya Olmoti, sasa hivi kuna vya mkakati kingine Sinoni, tutajenga kituo kuboresha pale Kaloleni na ukienda kule Levolosi ameboresha. Nenda Elerai kajenga kituo kingine kipya pale; ukienda Olasiti, unaona kabisa mambo yaliyofanyika katika Jiji la Arusha kwa kweli, haijawahi kutokea. Ndiyo maana sisi tunasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mitano tena. Tunasema kwa sababu, tuna ushahidi na mambo tunayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan kabla hajaingia madarakani, utalii ulikuwa ni changamoto. Vijana walikosa ajira kwenye magari ya utalii waliyokuwa wanafanya hiyo kazi. Kwenye hoteli zetu watu walifukuzwa kazi. Ameleta *Royal Tour,* leo watalii wamejaa, vijana wamepata kazi kwenye magari ya utalii, wageni walikuwa hawaji wengi, mikutano ilihamia Dodoma hapa na Dar es Salaam, lakini toka Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuja, mikutano imejaa pale Arusha; hoteli zinapata watu; magari, bodaboda wanapata abiria; mwenye Hiace, mwenye taxi wanapata abiria na wanakula vyakula kwenye maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana tunasema, unapomwona Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan analeta fursa za mikutano kama hii, baadhi ya viongozi wawaachie fursa hizi watu wa Arusha. Maana sasa mkianza na nyie kufanya kazi ya

mama ntilie sijui, kazi ya hoteli, mwisho wa siku mnawanyima Watanzania wengine waliopewa fursa hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni nyama, waacheni waende wakale kwenye baa; kama wanataka kunywa pombe, waacheni waende wakanunue kwenye maeneo mengine ili Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan fursa aliyowatengenezea Watanzania waende kule wakatumie na mwisho wa siku waweze kulipa kodi katika nchi yetu. Maana msipofanya hivyo, watakosa biashara. Wakikosa biashara hata kulipa kodi pia, itakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Samia Suluhu Hassan analeta fursa hizi kwa ajili ya Watanzania na wala siyo kwa masuala mengine. Kwa hiyo, nimesema kwa kweli nimshukuru kwa sababu, hata nilivyoongea Bungeni hapa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa shilingi milioni 500, kwa ajili ya kujenga eneo la wa Machinga, namna anavyowajali wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, zimekaa zaidi ya miaka miwili pale hazijafanya kazi, lakini mara baada ya kuongea hapa Bungen,i wamesikiliza kilio hicho, Serikali imetoa maelekezo na hivi leo unasainiwa mkataba kwa ajili ya kujenga eneo la Wamachinga kule *Bondeni City*, ili kuwajali wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kweli, tuna deni naye kwa sababu, mambo aliyotufanyia ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Arusha ya leo, siyo Arusha iliyopita. Barabara za lami Mianzini – Ngaramtoni kulikuwepo na changamoto kubwa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anajenga lami pale kilometa 18. Pale Ilboru ukienda, anajenga lami mita 700 na imekamilika, nenda Kijenge Nguwela wanajenga barabara ya lami, nenda Boma Siara wanajenga barabara ya lami, nenda kule Moshono Konakiselia amejenga pale lami kilometa moja, nenda kule Muriet kutoka kituo cha afya kuja Kituo cha Polisi anajenga barabara ya lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda pale Kaloleni anajenga barabara ya lami, nenda Levolosi anajenga barabara ya lami na

bado umesainiwa mkataba mkubwa kabisa wa barabara ya kutoka Kona ya Mbauda kwenda mpaka kwa Mrombo, wanajenga njia nne. Anajenga pia nyingine ya kutoka pale Kona ya Kiserian kwenda mpaka Fun Retreat. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mambo anayofanya ni makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefurahi sana kuona wamekamilisha tayari upembuzi yakinifu wa kutoka pale *Airport* ya Kisongo kwenda mpaka Kilombero. Tumeambiwa tayari fidia, zaidi ya shilingi bilioni 10, wakati wowote italipwa. Ni imani yangu kwamba, baada ya kulipa fidia watatangaza tenda ili njia nne itengenezwe, watu waweze kunufaika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, hiki ni kipindi cha kuhesabu faida. Kama bado kuna mambo mazuri ya Mheshimiwa Rais, endelea kuyasema. Siyo wewe tu, Mbunge yeyote namwongezea dakika kwa kuzungumza faida ya nchi. *(Makofi)*

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wakati wote, sisi kama watu wa Arusha, tumekuwa tunahangaika sana na mradi wa Arusha – Kibaya – Kongwa. Ni awamu zote umezungumzwa, lakini ule mradi haujawahi kutekelezwa. Leo kupitia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari mkataba umesainiwa, unakwenda kuanza na kilometa 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilometa 70 zile, kama nilivyosema, tunajenga njia nne kutoka pale Kona ya Mbauda tunakwenda mpaka *round about* ya Kwamrombo; baada ya *round about* ya Kwamrombo mbele yake kidogo ndiyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pale anajenga stendi ya kisasa ili watu wakitaka kwenda stendi wasipate changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, bado tunajenga barabara ya lami kutoka Kona ya Kiserian, pale Moshono, inakwenda mpaka kule *Fun Retreat* ambako wapo baadhi ya wawekezaji kama *TANFOAM,* wanajenga kiwanda kipya cha kisasa pale. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameona kazi hiyo wanayoifanya, ameamua kuwapelekea barabara ya lami ili mambo yaendelee vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wale ambao wanasimamia mradi huu, kwa maana ya *TANROADS* na Wizara ya Ujenzi kwa sababu mkataba umeshasainiwa, naomba mkandarasi afike *site* mapema ili Watanzania waendelee kula matunda ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuujali utalii, amekwenda kuubadilisha kabisa uwanja mdogo wa ndege wa Kisongo, uwanja ambao siku za nyuma palikuwa hakuna mabanda ya abiria, lakini sasa hivi yamejengwa. Ule uwanja ulikuwa hauna taa, sasa hivi ameweka taa, ndege zitakuwa zinatua hata usiku. Kwa hiyo, ni kazi kubwa ambayo ameifanya ya ku-*boost* utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Arusha hatuna mashamba. Pale hatulimi, tunategemea utalii, maana mtalii akija, akilala kwenye hoteli, faida ni nyingi sana. Akiamka tu asubuhi, akinywa supu ya kuku, mama kule au kijana anayefuga kuku atauza mayai, atauza kuku; Mmasai unayeuza kule ng'ombe utauza maziwa, utauza nyama ya ng'ombe; wewe unayeuza mbuzi ni hivyo hivyo; unayeuza mbogamboga utauza vitu vyako na unayeuza mchele, unauza. Kwa hiyo, inaongeza mzunguko kwenye uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata wageni wanaokuja kulala pale Arusha wana faida kubwa; wakilala kwenye hoteli ajira zinapatikana, lakini wakila kwenye hoteli, chochote kile wewe unayefanya biashara ndogondogo unapata hiyo fursa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kitendo cha kutuletea *Royal Tour* ametuokoa watu wa Arusha na ameondoa changamoto. Hivyo utaona namna anavyoijali Arusha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mwaka huu, 2025, tumeona amepitisha mapato yale yanayotokana na Ngorongoro pamoja na *TANAPA,* sasa hivi watabaki nayo wenyewe ili waendelee kurekebisha miundombinu ya ndani, barabara zikae vizuri ili watalii wakija mambo yawe mazuri zaidi pamoja na masuala mengine yanayohusiana na maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa kweli, pia namshukuru sana Waziri wa Fedha, ndugu na rafiki yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Waziri wake pamoja na Katibu Mkuu kwa sababu, kama wasingekuwa na Waziri mwenye kuweza kumsoma Dkt. Samia Suluhu Hassan, anataka nini, haya tunayoyasema yote yasingewezekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu pamoja na wasaidizi wake, wamemsoma Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakuna mfanyabiashara yeyote anayeonewa. Tumemsikia Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kwenye ziara yake, watu wasifunge *account* za wafanyabiashara na wasiwaonee, lakini wafanyabiashara pia, wasikwepe kulipa kodi kwa sababu kuna haya maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, watimize wajibu wao, walipe kodi na Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo tayari kuwalinda, ili mambo yaweze kwenda. Kwa hiyo, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa kazi hiyo aliyoifanya iliyotukuka. Tumeona hata wale ambao wanasema kuhusu changamoto ya mikopo, sisi ni wanufaika wa mikopo katika nchi hii. Hii miradi ninayoisema hapa inatokana na mikopo ya *World Bank*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunajenga stendi, ni mkopo wa *World Bank*, tunajenga yale Masoko ya Kilombero, tunajenga Soko la Morombo, ni mkopo wa *World Bank*. Tunaweka lami Engosheraton, lami ya Olasiti na Oljoro kwenda stendi, ni mkopo wa *World Bank*. Kwa hiyo, kama kuna mtu haoni mikopo inavyotumika huko kwake aje kwenye Jimbo la Arusha, tumwoneshe mfano wa namna ambavyo mikopo hii ina manufaa katika nchi na Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sisi tunamwambia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alale usingizi, Arusha Mjini ana kura za kutosha, tutamtetea asubuhi, tutamtetea mchana na tutamtetea jioni kwa sababu, kazi alizofanya zinamuuza. Wanasema Waswahili, "kizuri chajiuza." Mheshimiwa Dkt. Samia hana mpinzani, tutahangaika naye mpaka aweze kupata kura za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, nakutakia kila la heri kwenye jimbo lako. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na kwenye mkoa wenu mkipendana zaidi mtakwenda mbali zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Suma, jiandae Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia bajeti hii ya Serikali Kuu. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya njema tangu kipindi cha mwaka 2020. Mara tu baada ya kuapishwa nilianza michango yangu hapa, lakini pia, nimeuliza maswali ya kutosha. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuwa, alikuwa pamoja nami wakati wote. Alinishika mkono hakuniacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza sana Wizara hii ya Fedha na Mpango wa Serikali kwa namna ambavyo inafanya kazi nzuri na njema sana. Ni Wizara ambayo ni sikivu. Ninawapongeza sana kwa namna ambavyo mnachapa kazi vizuri. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, kaka yangu Kalumbu hapo, Naibu Waziri, pamoja na kaka yangu Waziri wa Mipango, wanafanya jambo jema sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Mbeya na wilaya zake zote kwa jinsi ambavyo walinichagua mimi, walikuwa wana imani na mimi. Ninawashukuru kwa upendo wao mkubwa, Wilaya ya Kyela, Rungwe, Mbeya Mjini kwa Mheshimiwa Spika, Mbeya Vijijini, Mbarali, Chunya na Busokelo. Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, ninaishukuru Kamati Kuu ambayo ilikaa ikawa na imani na mimi, wakapendekeza ama waliteua jina langu kuwa niwe Mbunge wa Viti Maalum wa Mkoa wa Mbeya. Ninaishukuru sana Kamati Kuu, Mwenyezi Mungu asiwapungukie, awe pamoja nanyi wakati wote ambapo

mnafanya majukumu yenu, akawape kila mahitaji ya mioyo yenu pamoja na familia zenu, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee sana namshukuru Mwenyezi Mungu kwa namna ambavyo ameendelea kutulinda na kuwalinda ninyi viongozi wetu ambao mnatuongoza hapa. Ninampongeza sana Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, namna ambavyo alikuwa anaongoza Bunge hili ambalo tunakwenda kumalizia. Mheshimiwa wetu Dkt. Tulia Ackson, ambaye anakwenda kuwa Mbunge wa Jimbo jipya la Uyole ninampongeza maana hana mpinzani yeyote kulingana na majukumu yake anayoyafanya, Mbeya tuna imani naye sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakupongeza sana Naibu Spika, Mheshimiwa Azzan Zungu, kwa kazi unayoifanya hapa Bungeni. Umekuwa unatuongoza vizuri sana na unasimamia Bunge vizuri sana. Ninawashukuru sana wananchi wa Ilala jinsi ambavyo mlipata maono ya kumchagua Mheshimiwa Zungu kuwa Mbunge wenu, hamkufanya makosa, mlitenda haki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawaomba sana wananchi wa Ilala waendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Zungu, wamchague tena arudi hapa Bungeni ili aendelee kufanya kazi zile ambazo Mwenyezi Mungu anamwongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee, na kwa mara nyingine tena niipongeze sana Wizara hii. Mwenyezi Mungu alinipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii na kuishauri Serikali kwa namna ya ulipaji wa kodi. Nilishauri Serikali kwa sababu wananchi walio wengi hawajui ni kwa nini, wanalipa kodi? Hiyo kodi wakilipa inakwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nikashauri, Serikali hii kwenye Wizara hii nilishauri kwamba uanzishwe mpango wa elimu kuanzia shule za msingi, sekondari, vyuo na vyuo vikuu ili Mtanzania huyu kadri anavyozidi kujenga imani, anavyofundishwa kwamba ni kwa nini analipa kodi, anakuwa hana kinyongo chochote. Anavyotoa kodi anajua kodi ndiyo ambayo inaleta maendeleo ya Taifa letu hili la Tanzania, kwamba, inajenga barabara kwenye upande wa afya, kwenye upande wa elimu na miundombinu ya namna yote

na mambo mengine mengi. Ninaipongeza sana Serikali kwamba ililipokea hili kwa upana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza kwa sababu wamekwenda kuanzisha rasmi somo la biashara, wameanza mwaka huu, ambapo hilo somo litakuwepo ndani ya miaka kumi tangu mtoto anapokuwa anakwenda kuanza shule. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni Serikali ambayo ni sikivu na ni Serikali ambayo inajali. Kwa kufanya hivi, pamoja na mpango huu kwa ajili ya kufundisha, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa fedha nyingi kwa ajili ya kuwafundisha hawa walimu ambao wapo ili waweze kufundisha kisasa namna gani ya ulipaji wa kodi za Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo, Mheshimiwa Rais ameidhinisha zitangazwe ajira nyingine 4,000 kwa ajili ya kwenda kufundisha somo hili la biashara. Kwa hivyo, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo analiongoza Taifa hili la Tanzania, mama yetu hana baya. Mama yetu ni mwema sana, mama yetu ni msikivu, mwenye upendo mkubwa na anajali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna hii ambapo Serikali imelichukua hili, tunaamini kwamba miaka ya mbele kodi zitakuwa zinalipwa kwa hiari na siyo kwa kuambiwa kwamba lazima utoe kodi. Mtu akijua kwamba muda huu umefika natakiwa nikatoe kodi, atakwenda kwa hiari yake mwenyewe kwa sababu atakuwa amepata elimu yeye mwenyewe, amepata elimu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hongera sana kwa kaka yangu *ilumbu gwangu* Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, kwamba alikwenda kulisimamia hili ambapo nilimwomba sana na akalifanyia kazi. Mwenyezi Mungu aendelee kusimamia majukumu yake wakati wote, asimpungukie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nishauri jambo moja. Kabla ya kushauri, ninatamani niseme namna gani ambavyo tunakwenda kwenye Taifa hili la Tanzania. Mheshimiwa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa mstari wa mbele wa kutoa ajira mahali pengi. Iwe kwa upande wa elimu, lakini ukienda *TRA,* ukienda sekta tofauti tofauti ajira zipo. Mheshimiwa Rais wetu na Amri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anafanya mambo mema sana, mambo makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na jinsi ambavyo wahitimu wanakuwa ni wengi, unakuta nafasi zimetangazwa, inawezekana zikatangazwa aidha nafasi 9,000, wanaokwenda kuomba nafasi hizo za kazi wanafika mpaka 50,000. Kwa hiyo, wengi wanakuwa wamebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao wanaokuwa wamebaki wanajiongeza, kwa maana ya kwamba wasajili kampuni zao ili waweze kufanya kazi na taasisi za Kiserikali. Taasisi hizo za Kiserikali wanaweka masharti magumu sana. Kwa vijana wanaokwenda kuanza ama kwa mtu yeyote anayekwenda kuanza biashara na taasisi za kiserikali, anakwama kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utakuta binti ama kijana amesajili kampuni yake, anakwenda kuomba kazi. Maana kazi zote zinatangazwa kwenye *NEST,* wanafuata utaratibu huo, lakini vigezo vya kupata hiyo kazi, vinakuwa ni vigumu mno. Utakuta anaambiwa sasa hivi moja ya vigezo ili upate kazi hiyo uwe umewahi kufanya. Wanakwambia lete *bank statement* ya miaka mitatu nyuma. Huyu anayekwenda kuanza, kijana ambaye amejiongeza, anapataje hiyo *bank statement* ya biashara hiyo miaka mitatu nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, anaambiwa kigezo kigumu kwamba kwenye akaunti yako kusipungue fedha kiasi cha shilingi milioni 100 mpaka shilingi milioni 200 na kuendelea, huyo anayekwenda kuanza anapataje hiyo fedha? Huo mtaji ambao anao huko, umekaa umetulia ili aweze kuendesha biashara yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nilitamani sana kuishauri Serikali, ninaomba sana vigezo hivi kwenye taasisi hizo naomba

wavipunguze, kwa sababu hata ambao wanaendelea kufanya kazi hizo, sasa wao walianza kwa vigezo vipi wakati wanaanza? Walifanya mpaka wakafanikiwa kuvuka vigezo, kwamba wana shilingi milioni 200, wana shilingi milioni 100 kwenye akaunti zao, waliwezaje kuwa na *bank statement* ya biashara hiyo kwa miaka mitatu nyuma?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sana Serikali walitazame jambo hili, na kwamba wanatakiwa kupunguza masharti makali na magumu kwenye nafasi hizo za kazi za kitaasisi ambazo ni biashara za kwa kwenye *tender.* Sasa mwananchi huyu anashindwa kujikwamua kibiashara, kujikwamua kimsingi kwanza ili afanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Serikali haijakaa mbali sana na wanawake, imewaona wanawake upande wa *TARURA*. Vikundi vya wanawake inatoa kazi, lakini pia kule nako kuna vigezo fulani ambavyo ni vigumu kidogo. Nilitamani wanawake hawa pia wapunguziwe masharti ya kupata kazi kwenye vikundi vyao ili waweze kufanikiwa kufanya kazi wajikwamue kwenye shida mbalimbali na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachukua nafasi hii kumshukuru kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo ametuona wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuletea fedha nyingi sana kwenye barabara ya njia nne ambayo nimekuwa nikiiomba mara nyingi. Hata Wabunge wa Mkoa wa Mbeya, wapo wamekwenda kuiomba hiyo barabara, na sasa hivi, barabara hiyo inakwenda kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa juzi tumepata msiba mzito sana, kulitokea ajali mbaya sana. Ajali hiyo ilipoteza uhai wa wananchi 28 kwenye mteremko wa Mlima Iwambi kutokea pale Mbalizi. Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ule msiba tulioupata kule Mkoa wa Mbeya hatukulia peke yetu, tulilia pamoja na yeye, kwa sababu alihusika kwa sehemu mbalimbali, kama majeneza, iwe kutoa fedha za rambirambi, alikuwa anatoa kwa unyenyekevu mkubwa. Imemsikitisha sana kana kwamba

hizo rambirambi hazifanani na gharama ya uhai wa mwanadamu, alitoa kwa unyenyekevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ametujali sana wananchi wa Mbeya. Hakuishia hapo, bado akatoa fedha kwa haraka zaidi ya shilingi bilioni 3.4 ili barabara ya mchepuo kwenye Mlima Iwambi ijengwe kwa haraka sana ili kuepusha ajali hizi ambazo zinagharimu maisha mengi ya wananchi wa Mkoa wa Mbeya. Tunamshukuru sana kwa fedha hizo alizitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado, kulingana na kwamba barabara za mchepuo ni za muhimu sana, akatoa fedha shilingi bilioni saba ili barabara ya Mlima Nyoka ijengwe kwa haraka ili kuepusha ajali zisizokuwa na ulazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamshukuru sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuujali Mkoa wetu wa Mbeya na Wilaya zake zote kwenye upande wa maendeleo. Kila mahali tunakopita kuna pendeza, kunang'ara, na kila mahali tunakopita miradi inakwenda inasonga mbele. Sasa hivi hata Tukuyu Mjini pale lile tenki la maji ambalo nilikuwa nikilisema hapa limekamilika. Ni kwa sababu anatuwezesha kuleta fedha ili tukamilishe ili wananchi wasiweze kuendelea kupata shida ya maji; na sasa hivi linakwenda kujazwa maji. Pale Tukuyu Mjini na kata zake zote shida ya maji inakwenda kuwa ni historia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Waheshimiwa Mawaziri. Ninawaombea sana kwa Mwenyezi Mungu kama ninavyojiombea mimi, kwamba twende na turudi tena hapa Bungeni. Ninaamini Mwenyezi Mungu atakwenda kuturudisha ili tuweze kuwatumikia wananchi wa Tanzania na Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, ninaiunga mkono hoja hii ya Bajeti Kuu ya Serikali kwa asilimia mia moja. Ahsante sana kwa nafasi hii niliyoipata na

Mwenyezi Mungu aendelee kulibariki Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Kassinge, jiandae Mheshimiwa Festo.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja iliyopo Mezani. Nianze kwa kuishukuru sana Serikali yetu ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia kwa utekelezaji wa mpango na bajeti kadiri ambavyo hapa Bungeni tumekuwa tukipitisha mwaka mpaka mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikumbushe tu kwamba katika mpango wa miaka mitano ambao ndiyo unaishia sasa, Bunge lako lilipitisha uboreshaji na upanuzi wa viwanja vya ndege 11 nchini. Tunashukuru, tumeshuhudia katika maeneo mbalimbali ya viwanja. Uboreshaji huu ukifanyika, upanuzi ukifanyika, na kwa kweli sifa zote ziende kwa Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili nikumbushe tu kwamba kulikuwa na viwanja vitano vya kipaumbele, ikiwemo Kilwa, Nachingwea pamoja na kule Kilimanjaro ambapo wananchi wa maeneo haya bado hawajalipwa fidia; na utekelezaji wa malipo haya upo katika mwaka huu wa bajeti ambao tunamaliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, niikumbushe Serikali yangu pendwa iweze kulipa fidia kwani ukarabati umeshaanza katika maeneo haya, na kwamba baadhi ya maeneo yameshatwaliwa. Kwa hiyo, ni jukumu tu la Wizara ya Fedha ku-*allocate* fedha ili wakalipwe fidia kule Nachingwea, wakalipwe fidia kule Kilwa, lakini pia wakamalizie wenzetu Segerea ambao wameshaanza. Tunashukuru kwa hatua hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili la uchangiaji wangu kwa kiwango kikubwa sana, nitajikita katika sekta ya maji, kwa sababu Mwenyezi Mungu katika Kitabu Kitukufu cha Quran Aya ya 30 katika Sura ya 21 *Surat An Biyai* anasema, na nina nukuu:

"*Wa Ja`Alna minal ma`i kulla syai`in hayyin.*" Mwisho wa kunukuuu. Tafsiri, tumejalia kutokana na maji kuwa ni uhai wa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ambavyo tunafanya tathmini ya sekta ya maji, miaka mitano, minne iliyopita na sasa kwa kweli Mheshimiwa Rais amepiga hatua kubwa sana. Kabla ya hapo, ilikuwa maji vijijini chini ya 70%, miaka minne iliyopita; maji mijini walikuwa wanapata chini ya 80% miaka minne iliyopita. Kulikuwa na miradi mikubwa ambayo imechelewa utekelezaji wake miaka minne iliyopita, ikiwemo miradi ya kimkakati. Kulikuwa na miradi kichefuchefu katika maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya miaka minne hii, ninayo furaha na ninazungumza kwa amani kwamba Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia amesikiliza kilio cha Watanzania kwa sababu katika Mradi wa Miji 28 ambapo ulikuwa ni changamoto ya kutotekelezwa kwa muda mrefu, tayari utekelezaji wake unaendelea, na shilingi zaidi ya trilioni 1.9 zimetolewa na mradi huu inaenda kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi katika Jimbo langu la Kilwa Kusini ni sehemu ya wanufaika wa mradi huu. Ninayo heshima kutamka katika Bunge lako Tukufu kwamba mradi huu sasa umeshafikia zaidi ya 90% na unakwenda kunufaisha wakazi katika Miji ya Kilwa Kivinje, Kilwa Masoko, Nangurukuru, Mavuji, Mtanga mpaka Kilwa Kisiwani kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi ndizo kazi ambazo Rais Samia ameweza kuzifanya katika miradi hii ya Miji 28 kwenye eneo langu tu kama mfano. Ninaamini pia kwa Wabunge wenzangu katika maeneo ya utekelezaji, utekelezaji uko katika hatua nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na mradi mkubwa kama mpango wetu wa kutoa maji Ziwa Victoria na kupeleka katika maeneo kadhaa ili wananchi wa Tanzania wakanufaike. Ninayo heshima kusema tu kwamba kwa mujibu taarifa tulizonazo, tayari Miji ya Tinde na Shelui mradi huu umeanza utelelezaji wake na Mheshimiwa Rais ametoa shilingi bilioni 24. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kulikuwa na ujenzi wa chanzo cha maji Butimba kule, tayari shilingi bilioni 71 amezitoa na utekelezaji unaendelea. Pia kulikuwa na miradi 218 chini ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa ya Mapambano ya Uviko 19, mimi jimboni kwangu ni sehemu ya wanufaika wa mradi huu wa Uviko 19, na zaidi ya shilingi bilioni 78 Mheshimiwa Rais amezisambaza katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa ajili ya wananchi kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais anaposema tunakusudia kumtua mama ndoo kichwani, anazungumza kwa nadharia, lakini pia anazungumza kwa vitendo. Huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi ya 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda katika Aya ya 100 ya Ilani hii, na ninanukuu: "*Katika miaka mitano ijayo lengo la Chama cha Mapinduzi ni kuona nchi inaendelea kuwa na usalama wa maji, na kwamba huduma ya majisafi na salama inaendelea kuimarishwa na kuwafikia zaidi 85% ya kazi wa vijijini na zaidi ya 95% ya wakazi wa mijini ifikapo 2025.*"

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo heshima kusema kwamba Mheshimiwa Rais ametekeleza Ilani na amepitiliza. Mpaka kufikia Disemba mwaka 2024, wakazi wa vijijini 83% wanapata maji. Mpaka kufikia Disemba mwaka 2024 wakazi wa mijini 91.6% wanapata maji. Ni nani kama Mheshimiwa Rais Dkt. Samia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upo msemo unaosema kwamba "*Man laa yashkur nnasa laa yashkurullah.*" Asiyeweza kumshukuru mwanadamu, hata Mwenyezi Mungu hataweza kumshukuru. Sisi ni waungwana na ni lazima tutamke kwamba tunakwenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa kazi kubwa ambayo Watanzania ametufanyia; na ikifika Oktoba hivi punde ni kwamba *we are going to separate the voters and the others, so that voters are going to vote for Dr. Samia and Chama cha Mapinduzi in October and the others will be blaming each other, will be watching, will be shouting.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo utaratibu wa mfumo ulivyo. Nni lazima makundi yawepo. Kwa hiyo, hata kama ni wachache ambao watakwenda kukodoa, watakwenda kulaumu wenyewe na kuendelea kushutumu, lakini sisi ambao tunayaona matunda ya Mheshimiwa Rais, tunakwenda kupiga tiki kwa Mheshimiwa Rais kwa sababu ameweza kutekeleza Sera ya Chama cha Mapinduzi ya kupeleka maji mijini na vijijini, na ameweza kumtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikimaliza katika eneo langu, niendelee kushukuru mipango yetu ya Serikali pendwa, kwamba katika miradi hii na mipango hii ya maji kuna mpango ule wa *National Water Grid,* Mpango wa Taifa wa Gridi ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo hili niendelee tu kusisitiza kwamba wakati tunatoa maji kutoka Ziwa Victoria kupeleka maeneo mengine mpaka hapa Dodoma, wakati tunatoa maji katika Mto Ruvuma ili uweze kunufaisha wakazi wa Mikoa ya Kusini hususan Ruvuma pamoja na Mtwara, ni wakati mwafaka sasa umefika wa kutoa maji Mto Rufiji ili uweze kusambaza maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na maeneo yake yote ikiwemo Ubungo, Ilala, Segerea, Kigamboni, Temeke, Mbagala, Kinondoni na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa kusini kule pia ni wakati muafaka sasa umefika wa kutoa maji kutoka katika Mto Rufiji yaweze kusambazwa mikoa ya Kusini ya Lindi na Mtwara ili majimbo yote ya Lindi na majimbo yote ya Mtwara yaweze kunufaika na mradi huu mkubwa wa kutoa maji Mto Rufiji na hatimaye sera ya mama, Sera ya Chama Cha Mapinduzi ya kumtua mama ndoo kichwani iweze kuonekana na Watanzania na hatimaye Oktoba sisi tunasema: "sisi na Samia, sisi na Chama Cha Mapinduzi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Sanga, wajiandae Mheshimiwa Mchungahela na Mheshimiwa Kakunda.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyo mezani. Jambo la kwanza niseme ninaunga mkono hoja na ninaipongeza sana Serikali na ninaipongeza sana Wizara ya Fedha kwa hotuba yao nzuri sana, hotuba iliyojaa matumaini kwa Watanzania wengi na mamilioni ya Watanzania. Hotuba hii na bajeti hii imebeba matumaini makubwa sana. Pia, ninawashukuru na niwapongeze watendaji wa Wizara, lakini kikubwa zaidi niwashukuru Wananchi wa Jimbo la Makete kwa imani ambayo mimi wamenipa kwa muda wa miaka mitano na kwa imani ambayo wanaendelea kunipa kwa kipindi kijacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana wananchi wa Makete kwa sababu ilikuwa ni kipindi ambacho Jimbo la Makete kwa mara ya kwanza limepata Mbunge kijana na hajawahi kutokea na mimi ndiye nimekuwa Mbunge wa kwanza kijana kwenye lile jimbo na niwahakikishie kwamba kazi nimeifanya na wao wanajivunia kwamba walituma mwakilishi kwelikweli ndani ya Bunge hili. Kwa Jimbo la Makete walishafanya uchaguzi miaka mitatu iliyopita na wanaamini kabisa kwamba Mbunge wao ni mimi na nitaendelea kuwa Mbunge wa Jimbo la Makete kwa sababu nimetosha, nimetosha na nimetosha kweli kweli kwenye Jimbo la Makete kwa maana ndani ya Bunge na nje ya Bunge nimekuwa nikiwawakilisha vizuri. Ninawahakikishie wananchi wa Makete kwamba sitawaangusha na nitaendelea kuwapa ushirikiano kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais, niliingia kwenye Bunge hili tukiwa na begi kubwa sana lililobeba changamoto za wananchi wa Makete, lakini leo ninasimama hapa nikiwa ninachangia ndani ya miaka mitano leo tukiwa tunafunga Bunge letu kwa maana ya wachangiaji kwa miaka mitano mimi kama nikiwa ninachangia, ninaipongeza sana Serikali kwa kazi ambao imefanya Jimbo la Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliingia kwenye Bunge hili wakati Jimbo la Makete lina vituo vitatu vya afya, leo ninasimama hapa Mbunge wa Jimbo la Makete nikijivunia kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga vituo saba vipya ndani ya Jimbo

la Makete kitu ambacho hakijawahi kutokea. Wamepita Wabunge wengi lakini walikuwa na vituo vitatu vya afya. Leo ndani ya miaka minne; na mitano ya Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, tumejenga vituo vipya saba vya afya, ni kitu ambacho hakijawahi kutokea na katika vituo hivi hakuna mchango wa mwananchi hata shilingi 10, vimejengwa na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru vilevile kwamba katika kipindi ambacho ninaingia hapa tulikuwa na zahanati chache lakini ndani ya miaka minne, mitano hii ya Serikali tumejenga zahanati takribani 15 mpya ndani ya Jimbo la Makete. Kwa hiyo, kama Mbunge ninajivunia kwamba Serikali imefanya kazi kubwa ndani ya Jimbo la Makete achana na umeme ambao umeenda vijiji vyote, lakini kwa ripoti ya *RUWASA* ukienda kwenye sekta ya maji, Ripoti ya *RUWASA* ambayo imetoka, Jimbo la Makete tunaongoza kwa upatikanaji wa maji kwenye Taifa letu. Wakati ninaingia tulikuwa na 62% na leo tuna 98% upatikanaji wa maji kwa wananchi wa Makete. Kwa hiyo, mimi kama Mbunge kwa kweli ninajivunia na ninajisifia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda kwenye sekta ya elimu, nenda kwenye sekta ya maji, nenda kwenye sekta ya kilimo tumefanya kazi kubwa sana ndani ya Jimbo hili. Ndiyo maana ninasema wananchi wa Makete walishafanya uchaguzi wa Mbunge wao kwa miaka mitatu iliyopita, kwa hiyo tunachokifanya sasa hivi ni kuhakikisha kwamba tunafuata taratibu tu za kawaida ndani ya chama na Serikali kuhakikisha sasa wa Mbunge wa Jimbo la Jimbo la Makete ninarejea kwenye nafasi yangu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wa Makete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais; na Watanzania wafahamu kwamba, kinachozungumza kwenye Taifa hili ni takwimu, hatuzungumzi maneno, tunachokizungumza ni kwamba Taifa hili la Tanzania, sisi kama Taifa tumelijenga sisi wenyewe, hamna mtu aliyetujengea Tanzania. Barabara, afya, elimu, kila sekta wanayoizungumza, tumezijenga kwa nguvu zetu, tumejenga kwa kodi zetu,

tumejenga taifa hili kwa mikopo, tumejenga sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mataifa wamejengewa nchi zao, lakini sisi tumejenga kutoka chini hadi leo hapa tulipofikia. Niipongeze bajeti ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, ilionesha tulikotoka, ilionesha tuliko na inaonesha tunakokwenda. Kwa kweli kama Watanzania wana masikio wakumbuke tulikuwa na wataalamu bingwa wa afya 14 kwenye nchi hii, leo tunazungumzia mabingwa wa afya 2,000 ambao wamezalishwa na Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kitu kikubwa sana kwenye nchi, Watanzania lazima wajivunie kuijenga nchi yao wao wenyewe ni kitu cha kujivunia na kutembea kifua mbele na ni kusisitiza tu kwamba ni lazima tuendelee kulipa kodi ili tuendelee kuijenga nchi yetu kwa sababu hatujajengewa na mtu. Hakuna mkopo ambao unatumika kiholela, mikopo yote ambayo inaletwa kwenye nchi hii tumeona matunda yake, tunaona *UDOM* imesimama na tunaona watu wanasoma, tunaona barabara za lami zinajengwa, tunaona miradi ya maji inaenda, tunaona Majiji yanakua kila siku. Hatujajengewa na mtu, tumejenga sisi wenyewe kwa nguvu yetu kama nchi na lazima tuwe kipaumbele lazima tujivunie Serikali yetu, hususan Chama Cha Mapinduzi ambacho kinaiongoza Serikali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama Mbunge ninatamani nichangie mambo machache. Jambo la kwanza ninataka kuchangia kwenye uwezeshaji wa wafanyabiashara. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, ukiangalia kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, Dkt. Kitila Mkumbo tunakupongeza. Maandalizi ya Ilani hii, ukurasa namba 95 wanazungumza uwezeshaji wa vijana na watu kwenye sekta ya uchumi, ninampongeza sana Waziri kwamba wameona kwamba kuna nia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge ni lazima tulizungumze hili kwamba, tumeshaanza kuona nia thabiti ya Serikali kuwezesha wafanyabiashara kwenye nchi hii wadogowadogo. Kwenye mazingira ya uwezeshaji wa

wafanyabiashara kuna mambo mengi yamefanyika. Katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukisoma kwenye aya namba 168, amesema marekebisho ya utoaji wa leseni za biashara, hili ni jambo zuri sana sisi kama vijana tunakushukuru kwa sababu, katika Taifa kama hili hatutegemei Watanzania wote kuajiriwa na Serikali, lakini tunategemea Serikali ilee sekta binafsi, ilee mazingira mazuri, itengeneze mazuri kwa ajili ya sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya mazingira Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni haya ya kuweka mazingira mazuri ya wafanyabiashara wetu kwenye Taifa letu. Kuweka mazingira mazuri ya upatikanaji wa leseni za biashara, lakini pili kwenye ukurasa wa 158 wa Hotuba, Waziri anasema, shughuli zitakazofanywa na wazawa zijulikane na shughuli zinazofanywa na watu wageni zijulikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimekuwa ni kilio kikubwa sana cha wafanyabiashara pale Kariakoo kwamba tumekuwa tukiingiliwa na watu wa kutoka mataifa mengine wanafanya biashara ndogo ambazo zilikuwa zinafanywa na Watanzania. Hasa kwa hiki ambacho amekisemea kwenye hotuba hii ni dhahiri na ni wazi kwamba Serikali imekusudia kupambana na hiyo sekta, kuhakikisha wafanyabiashara wetu wanakuwa na mazingira salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunahitaji mwekezaji akija awe na uwekezaji wenye tija ambao Tanzania haupatikani, lakini siyo kazi za Watanzania ambazo zimekuwa zikifanywa. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa mazingira haya ambayo ameyafanya lakini pia nimpongeze kwa sababu amesema juzi *BOT* wamezindua mfumo, kulikuwa na kilio na Azimio la Bunge lilipita hapa kuhusu mikopo chechefu ambayo imekuwa ikiwaumiza Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Gavana wa *BOT,* Bwana Tutuba, lakini pamoja na Waziri kwa sababu yeye ndiye aliye humu ndani, alichukua mawazo haya. Wameanzisha huu mfumo wa kidijiti unaosema "Sema na Benki Kuu," ninampongeza sana.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimpe taarifa kaka yangu kipenzi Festo Sanga ambaye anachangia kwa uzalendo mkubwa sana Mbunge makini wa Makete, yaani ni kijana makini kwa kweli tunamwitaji tena; lakini niseme tu, nimpongeze kaka yetu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye kupitia mikopo ya kausha damu wameweza kufuta taasisi 16 ambazo zilikuwa zinaumiza wananchi na sasa wananchi wapo salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nilifikiri kaka yako kipenzi ni Mheshimiwa Profesa Ndakidemi. Mheshimiwa Festo endelea. *(Makofi)*

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, huyu ni baba.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na niseme wazi ninapokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwa sababu moja kati ya Wabunge ambao wamekuwa mstari mbele kupigania kuhusu mikopo hii chechefu ni pamoja na Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, ninamuunga mkono sana na niipongeze Serikali kwamba kilikuwa ni kilio cha Watanzania kuhakikisha kwamba tunapambana na mikopo hii chechefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *BOT* imekuja na kitu kinaitwa "Sema na Benki Kuu," haya ni mafanikio makubwa kwa Serikali yetu kuhakikisha kwamba inapambana. Kwa Watanzania wengi kuna changamoto ya elimu ya kiuchumi waliyonayo, wengi hawana elimu ya kiuchumi wamekuwa wakikopa kwenye mikopo ambayo inawaumiza lakini Benki Kuu wametafuta suluhisho hili, niwapongeze sana Wizara ya Fedha kwa kazi ambayo wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru pia kwamba Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti hii wameshusha leseni za

bodaboda kutoka 300,000 hadi shilingi 70,000 ni kitu kikubwa sana kwenye kusaidia vijana. Hivyo ndivyo sekta binafsi inavyolelewa, kuwasaidia na kuwatengenezea mazingira mazuri sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanapata huduma nzuri na kwa wakati na kwa unafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna eneo la bodaboda Mheshimiwa Waziri, ushauri wangu tu wa baadaye ambao ninatamani ni kwamba Wizara ya Mambo ya Ndani na Wizara ya Fedha waangalie na Wizara ya Afya, licha ya kwamba tumewashushia bodaboda upatikanaji wa leseni kutoka hiyo shilingi 300,000 hadi shilingi 70,000 hadi 30,000 Mheshimiwa Waziri tuombe kwamba, kwa sababu kwa takwimu na ripoti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ilipotoa, vifo vya takribani 1,400 vimejitokeza vya bodaboda.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tutazame jinsi gani ya kukaa na bodaboda kuwaunganishia bima ya afya pamoja na leseni yao iwe inasomeka katika mfumo mmoja ili wanapopata leseni hapo hapo ndani yake kuwepo na bima ya afya kwa sababu ni moja kati ya maeneo ambayo vijana wanapata sana ajali. Vilevile, hii itatusaidia kuhakikisha hata wale ambao wamekuwa na changamoto ya matibabu kwa sababu wengi bodaboda hizi wanachukua za matajiri wao, wao wanakuwa hawana uwezo; tuweze kuichukuwa hii hoja ya kwamba bima ya afya iwe na *package* ndani yake ya kuhakikisha kwamba anapata leseni humo humo na ndani yake anapata bima ya afya ili tusaidie bodaboda wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, niwashukuru kwa niaba ya wafanyabiashara wa hoteli na wafanyabiashara wadogowadogo kushusha *service levy* kutoka 0.3 hadi 0.25, lakini kutoka 10% hadi asilimia mbili, kwa kweli mmefanya jambo kubwa sana Wizara ya Fedha. Sisi tunawapongeza na kilikua ni kilio cha sisi Wabunge, tunatumwa kutoka maeneo mbalimbali kwamba wakatupiganie na tunaona kabisa nia ya Serikali ya dhati kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama kijana ninaondoka katika Bunge hili kwa hii miaka mitano, nitarejea mwezi wa

Novemba, kuna vitu ambavyo tulivifanya; kuna vitu ambavyo nilivifanya ndani ya Bunge hili, *in a records* ninatamani watu wafahamu kwamba tulifanya, ukiangalia kama Mbunge nilitoa michango hapa Serikali imeifanyia kazi. Nilitoa mchango wa bodaboda kutoa faini kutoka 30,000 hadi 10,000, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi ililifanyia kazi. Mheshimiwa Waziri nilitoa hoja ya kwamba lazima tushushe kodi kwenye nyasi bandia, Serikali ilifanya kazi na nyasi bandia zikaondolewa kodi na nchi hii sasa inafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza kuhusu *cashless economy* Mheshimiwa Waziri kwenye Taifa letu, nilizungumzia *cashless economy* hapa kwa kina na *BOT* wametoa tamko kuanza kuweka *incentives* kuwapunguza Watanzania kwenye matumizi ya *cash* kwenda kwenye *cashless economy*. Mheshimiwa Waziri, *BOT* wamekuja na mkakati wa miaka mitatu kuhakikisha kwamba wana-*support* Taifa kwenda kwenye *cashless economy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge pia nilikuja kwenye Bunge hili nikaleta hoja ya *unclaimed financial assets* kuhakikisha kwamba nchi yetu tunasimamia vizuri *unclaimed financial assets* ambazo zinaweza zikawa ni tija kwenye utendaji na Wizara ya Fedha wameliona hilo na wamechukua hizo fedha wanaelekea eneo lingine. Kama Mbunge nilizungumza na nikatoa hoja kwamba *betting* ni lazima ichangie kwenye maendeleo ya nchi yetu. Leo *betting* inachangia kwenye Mfuko wa Afya, leo *betting* inaendelea na maeneo ya Mfuko wa Maendeleo. Tumefanya mambo mengi kama Mbunge ninajivunia kwamba katika kazi ya miaka mitano, Serikali imechukua maoni ya Wabunge na wanaenda kuyafanyia kazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hoja ya *cashless economy* ninatamani na ninaomba sana nitie msisitizo kwamba hii itatusaidia, kama nchi kuongeza *tax base*. Hapa lazima tutafute tuiongeze kwa sababu Watanzania wengi wanalalamika na kodi hawalipi. Ni vyema tukaongeza wigo wa watu kulipa kodi, ni kupitia *cashless economy*. Kama Taifa ni lazima tuachane na watu kutembea na maburungutu ya hela mfukoni watu walipe kwa kutumia simu; watu walipie kupitia *cheque*; watu walipie

kupitia kadi za benki tuachane na kutembea na fedha ili watu wachangie maendeleo ya nchi yetu. Bila kufanya hivyo hatuwezi kujenga nchi. Mtanzania ajue Taifa hili halili kitu kingine zaidi ya kula kodi, nchi inajengwa kwa kulipa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana pale Simiyu Mheshimiwa Rais alisisitiza kwamba lazima Watanzania walipe kodi na lazima tuwekewe mazingira mazuri ya kulipa kodi. Nitumie nafasi hii kumpongeza Kamishna wa *TRA,* tunaona sasa hivi ulipaji wa kodi wa Mtanzania umekuwa katika mazingira salama, anafanya kazi vizuri, hatujasikia kero wala kelele yoyote, hili ni jambo kubwa sana Mheshimiwa Waziri tunafurahia sana kwa kazi ambayo ameendelea kuifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri nichukue nafasi hii kuwapongeza kwa kuwa na *reserve* ya madini kwenye nchi yetu hususan kwenye Benki Kuu. *Reserve* ya madini Mheshimiwa Waziri jana amesaini mikataba takribani miaka minne, lakini ilikuwa ni hoja ya Bunge kuwa, Taifa kama Taifa lazima tuwe na *gold reserve*. *Gold reserve* ni kitu muhimu kwenye nchi. Ukisoma kwenye ripoti hapa katika nchi 10 Barani Afrika zinazoongoza kwa *reserve* ya madini Tanzania ilikuwa haipo. Mheshimiwa Waziri, ukiangalia Algeria ndiyo walikuwa wanaanza Mheshimiwa Waziri walikuwa na tani 173.

Mheshimiwa Naibu Spika, walikuwa wanakuja kufuatiwa na Mozambique, katika nchi 10 bora za Afrika kwenye *gold reserve* Mozambique walikuwa wana tani tatu. Leo Tanzania ndani ya miezi tisa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tumeingiza na tume-*reserve gold* tani 5.2, ni kitu kikubwa sana katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma kwenye suala la *financial stability*, katika kipindi ambacho kuna *Geopolitics Instability* kama sasa hivi, hii ni kitu kikubwa katika nchi. Kama Waziri, kama mshauri wa Rais, tunakupongeza sana Mheshimiwa Waziri katika kipindi chako hii nchi kuanza kuwa *gold reserve* ambayo sasa hivi ina thamani ya 1,400,000,000. Kama nchi lazima tujivunie. Unapotokea mdororo wa uchumi, unapotokea mtikisiko wa

uchumi nchi sasa angalau sasa kuna eneo ambalo tunaweza tukaji-*balance* na tukajibana.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni jambo kubwa na sisi kama Wabunge lazima tujivunie kwamba nchi yetu sasa imeanza kuwa na *gold reserve* na ni lazima tuendelee kusisitiza na tunaona nia kwa sababu mikataba waliyoingia jana ni kwamba 20% ya *Shanta mining*, 20% ya *GGM*, 20% ya *GGR*, zote zitakuwa zinauzwa kwenye nchi yetu ili nchi yetu iwe na *gold reserve*. Utajiri wa dunia, utajiri wa nchi, *financial stability* ya Taifa ni kuwepo na *gold reserve* na sisi Tanzania sasa tumeanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, niwashukuru sana wote ambao wameendelea kutuunga mkono na niwatakie kila la heri Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini zaidi zaidi nikutakie kila la heri pamoja na Mheshimiwa Spika. Sisi kama vijana kuna mambo ndani ya Bunge tumejifunza kupitia nyie na tumeendelea kukomaa. Tuliingia tukiwa wageni na leo hii tupo humu ndani tunaonekana ni Wabunge tupo imara. Tunaamini tukirejea wakati mwingine tutakuwa imara zaidi ya jana na sisi kama Makete tumeshachagua Mbunge na Mbunge ni Festo Richard Sanga, ahsanteni. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela, wajiandae Mheshimiwa Kakunda na Mheshimiwa Getere.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa nafasi…

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa nishatoa tangazo mwenye pumzi aendelee tu kuchangia. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa nafasi lakini nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenipa afya njema kuchangia bajeti hii. Pia ninaomba niishukuru familia yangu kwa kunivumilia muda mrefu nikiwa ninawajibika kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Lulindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ninaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita kwa jitihada zake kubwa za kuhakikisha kwamba inajenga na kufufua uchumi wa nchi hii. Mambo mengi sana katika nchi hii yamefanyika kuhakikisha kwamba uchumi unakua, lakini unakuwa bora kabisa. Kuna viashiria vingi sana vinaonesha juu ya jambo hili, ushahidi upo waziwazi kabisa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uchumi wa Taifa umeongezeka kwa maana ya kukua kutoka 5.1% na kufika 5.5% lakini pia mauzo ya kilimo nje ya nchi yameongezeka kutoka dola za Kimarekani bilioni 1.2 na kufikia Bilioni 3.54 kutoka mwaka 2023 kwenda 2024. Ongezeko hili ni kubwa sana ni ongezeko la 195%, ni ongezeko lililokuwa kubwa na ni jambo kubwa sana la kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Hassan kwa jitihada zake binafsi ambazo zimefanya mambo haya yakaenda sawa, lakini pia na timu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, tunaweza tukampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake kubwa kujenga uchumi wa nchi hii na ushahidi unaonekana wazi katika kilimo. Licha ya kuwa mauzo ya kilimo yameongezeka, lakini pia kuna utoshelezi wa chakula. Utoshelevu wa chakula umeongezeka kutoka tani milioni 17.14 mwaka 2023 na kufikia tani milioni 23.8 mwaka 2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika ongezeko la mbolea kutoka tani 727,000 kwenda tani 1,213,000 hii inaonesha jinsi kilimo kilivyokua. Hii imeongeza nguvu kazi kwa kiasi kikubwa ambayo ilikuwa haionekani wapi inakofanya kazi; inaonekana kwenye kilimo. Ongezeko la mbolea hii inaonekana moja kwa moja kwamba hii mbolea inatumika katika kuzalishia mazao ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushahidi pia unaoonesha kwamba sasa hivi eneo hili la kilimo limeongeza nguvu kazi kwa maana ya watu walioajiriwa katika eneo hili ni 65%; hivyo, 65% ya nguvu kazi ya nchi hii iko kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kushuka kwa mfumuko wa bei kutoka 3.8% hadi 3.1% kunaonesha kukuwa au kuboreka au kuimarika kwa uchumi katika nchi hii na haya yote

yamefanywa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, yeye na timu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli tunayo mengi zaidi ya kuendelea kupongeza kutokana na yaliyofanyika kwa ajili ya kujenga uchumi wa nchi hii. Akiba kwa mfano ya pesa; kumekuwa na ongezeko la akiba ya pesa ya kigeni kutoka bilioni dola 5.3 na kufika kiasi cha bilioni 5.6 Dola za Kimarekani. Hii ni kutoka mwaka 2023 kuelekea mwaka 2024, lakini hali kadhalika kumekuwa na ongezeko la mauzo ya nje ya huduma kutoka Dola za Kimarekani bilioni 7.2 kwenda dola bilioni 9.1. Hili ni ongezeko kubwa sana la mauzo katika masuala ya bidhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, licha ya ongezeko la mauzo ya bidhaa, pia kumekuwa na ongezeko la mauzo ya huduma. Kumekuwa na ongezeko kama ifuatavyo: Kutoka Dola za Kimarekani bilioni 3.8 mwaka 2023 na kuwa dola bilioni 4.2 mwaka 2022, lakini kitu kilichofurahisha zaidi ni urari. Kumekuwa na ongezeko, urari chanya. Urari maana yake ni *balance of payment.* Kumekuwa na ongezeko la *balance of payment* kutoka dola milioni 41 mpaka kufikia dola milioni 80. Hii ni alama kubwa sana ya kuonesha kwamba uchumi katika nchi hii unakua, tena unakua kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwaeleza ndugu zangu wananchi, wasiwe na hofu kabisa kabisa na ninataka niwaambie kwamba kuna suala la deni linalozungumzwa mara kwa mara, niwahakikishie kwamba hili deni ni himilivu, wala wasiwe na shida wala kuwa na wasiwasi kuhusiana na hili deni na bado tunao uwezo wa kukopa zaidi ya hali ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuzungumzia pia kuhusiana na kodi. Hapa ninaomba kushauri jambo, mazuri mengi kama nilivyoyangumzia; lakini pia ninatamani kushauri kitu kusudi haya mazuri yaendelee kuwa endelevu. Tunazungumzia kuhusiana na suala la kodi; ninashauri wigo wa kodi kuongezeka katika mazingira haya. Kwanza, kumekuwa na idadi chache ya walipakodi; kwa takwimu inaonesha ni milioni 2,467,049 pekee. Hawa ndiyo walipakodi katika nchi hii, lakini ukiangalia nguvu kazi

katika hii nchi ni kubwa mno kiasi kuwa walipakodi wawe kiasi hiki inakuwa siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hapo bado tuna *regular taxpayers* ambao wanalipa mara kwa mara, wapo takribani 687,565 pekee. Hawa ni *regular taxpayers*. Kwa kweli bado tunahitaji kufanya nguvu kubwa kuhakikisha kwamba tunakuwa na *tax base* nzuri ambayo itatuwezesha sisi kuendelea kukua kiuchumi zaidi na sisi kuwa ni watu tunaofahamika kwamba uchumi wetu uko imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema pale mwanzo tusihofu masuala ya kukopa kwa sababu gani? Hizi pesa zinazokopwa hazitumiki katika *recurrent expenditure*, zinatumika moja kwa moja katika *capital expenditure* na tunaona miradi mikubwa mikubwa inayofanyika kama *Standard Gauge*. Tumeona miradi mikubwa ya barabara, tumeona miradi mkubwa ya vyanzo vya maji, *Stiegler's Gorge* kwa mfano. Hali kadhalika tumeona jinsi miradi mikubwa ya umeme inavyotekelezwa katika nchi hii, hali ambayo imewezesha kwamba nchi nzima takribani vijiji vyote vimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule kwangu kwa mfano kwenye jimbo langu takribani vijiji vyote 97 vimepata umeme. Hii inaonesha jinsi uchumi wa nchi hii unavyokua, lakini pia ni uchumi tegemezi, kwamba utatuwezesha kuvuka na sisi kuwa imara sana. Mfano wa ukopaji, kuna watu wana madeni kuliko sisi tulivyokuwa nayo hapa jamani. Kuna watu wanadaiwa mpaka unashangaa hivi hizi pesa kweli hawa watu wanalipa au wanawadhulumu watu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, siwezi kutaja jina la nchi, lakini ni nchi kubwa sana duniani. Yenyewe inadaiwa pesa dola trilioni 32.6*, no,* dola trilioni 36.22, ni pesa nyingi sana hizo watu wanadaiwa, sisi tunadaiwa nini jamani? Hatudaiwi chochote sisi, hasa ukizingatia na uwezo wetu ulivyokuwa mzuri katika kulipa, tunaogopa nini? Ninapenda niwahakikishie kwamba bado tuna nafasi ya kuendelea kukopa zaidi kama inawezekana na wala tusihofu kwa sababu uwezo wa kulipa tunao na tusiwe na shaka, deni letu ni himilivu. Tusiwe na shaka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningetamani sana pia kuonesha mazuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametutendea Wanalulindi. Kwa kweli sisi hatuna cha kumlipa zaidi ya kumuahidi kwamba tutalipa kura 100%. Japo ni jambo gumu, ninataka nitoe *commitment* hapa, huenda tusiweze kupata hiyo 100% ya kura, lakini vyovyote iwavyo, hata 99% tuna uwezo wa kumpigia kura Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyotufanyia ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jimboni kwangu kama nilivyoanza kutangulia, suala la umeme hakuna kijiji sasa hivi ambacho hakijaguswa na umeme. Vijiji vyote 97 vina umeme, lakini jimboni kwangu nikisaidiwa na Mheshimiwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimeweza kupeleka kila kitu alichonituma nikipeleke. Amenituma pesa kwenye shule za sekondari za kata, kulikuwa na maeneo mengi sana tulikuwa hatuna sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda nikuhakikishieni kutokana na ujasiri wa mama huyu na jitihada anazozifanya na kunisikiliza mara zote nilivyokwenda kumwomba, ameniwezesha kuhakikisha kwamba kila kata katika jimbo langu tuna shule za sekondari, kata zote sasa hivi 18 tuna shule za sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hiki hiki kifupi amefanya jitihada kubwa sana kuhakikisha tunajenga shule mpya za *A–level*. Tumekuwa na ongezeko la shule mpya za *A–level* mbili kwa maana ya Shule ya *A–level* ya Mpeta. Hali kadhalika sasa hivi tunajenga *A-level* ya Makong’onda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma pia kulikuwa na ubovu mkubwa au uchakavu mkubwa katika Shule yetu ya Sekondari ya Ndwika. Sasa hivi ninataka niwaambie Shule ya Sekondari ya Ndwika imetumia zaidi ya bilioni moja katika kufanya ukarabati na sasa hivi Ndwika ni shule mpya na ni shule ambayo inategemewa kitaifa, ina-*perform* vizuri sana, sana, sana. Haya ni matunda ya kazi alizozifanya Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan akisaidiana nami Jembe lake aliloniweka kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda niwahakikishie kwamba kuna mambo makubwa yamefanyika kipindi chake. Kulikuwa na barabara ambayo ilikuwa inaonekana kuwa ni barabara ya kuombea kura. Wenyewe wanasema kwamba, "mfupa uliomshinda fisi." Ni kweli mfupa huu ulikuwa umemshinda kwa sababu kwa miaka mingi sana tulikuwa tukitamani sana kupata barabara hii; Barabara ya kutoka Newala kuelekea Masasi. Sasa hivi tunajenga kwa kiwango cha lami, kilometa 60, pesa takribani shilingi bilioni 94. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni pesa nyingi sana; ni pesa nyingi sana na ukiangalia katika mazingira yalivyo katika Jimbo letu la Lulindi tangu mwaka 1995 lilipoanza kuumbwa, ninataka niwahakikishie kwamba, ukikusanya miradi ile ya huko nyuma inazidiwa na mradi huu mmoja tu wa barabara, bilioni 94, ni pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nani anaweza akasema kwamba hatampigia Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ujasiri huo? Kama huko nyuma kuna vitu vya namna hii havijawahi kufanyika, ninataka niwaambie jambo lingine ambalo amewahi kulifanya katika jimbo langu ambalo ni la mfano ambalo nimekuwa nikiomba kumalizia; kuna Daraja la Mbangala, daraja hili ni daraja la mfano katika Mkoa wa Mtwara. Ni daraja ambalo limegharimu takribani 9,800,000,000. Ni daraja ambalo limegharimu pesa nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa eneo la kijijini kwenda kujenga daraja la 9,800,000,000 kwa kweli ni maajabu makubwa sana. Nani kama Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan? Hakuna kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye daraja hili ningemwomba Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba afanye kitu pale. Nimekuja mara kadhaa kuomba *certificate* za yule mkandarasi zilipiwe ziishe kusudi lile daraja likamilike. Pale tunadaiwa *certificate* kama mbili, tatu hivi kusudi kuweza kumalizia lile daraja. Sasa hivi tayari shilingi bilioni tano zimetumika katika daraja lile na zile zilizobakia basi ziende zikamalizie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kama haitoshi, tumekuwa na mradi mkubwa sana katika Mkoa wa Mtwara; Mradi wa Maji ambao tunajenga kutoka kwenye chanzo cha Mitema. Mradi huu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kutupa pesa nyingi takribani bilioni 84 na pale Newala tunajenga *tank* kubwa sana lenye ujazo wa lita 6,000,000. *Tank* hili ninalizungumzia kwa sababu, litasaidia katika eneo langu la Lulindi, Kata ya Makong'onda, Kata ya Namalenga, Kata ya Mitesa na Kata ya Mchauru. Ni kata ambazo zitanufaika na mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunayo mengine mengi zaidi ya kuyazungumza, mengi sana ambayo yamefanyika katika Jimbo la Lulindi. Miongoni mwake ni suala la afya. Wakati ninaingia pale kulikuwa kuna changamoto kubwa sana ya afya, lakini tumeweza kuhakikisha kwamba tunapambana kwa namna moja au nyingine kuhakikisha suala hili linapungua makali yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametuwezesha kupata takribani zaidi ya bilioni tatu kwa ajili ya kujenga Hospitali ya Mbuyuni. Hospitali ambayo imejengwa imekamilika, ni ya kisasa, ina miundombinu ya kutosha, ina vitendea kazi bora kabisa, ina kila aina ya sifa, ikiwemo sasa hivi imekuwa ni hospitali ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo kama haitoshi alituwezesha pia kupata magari ambayo yameweza kutumika kwa ajili ya kufanya huduma za afya. Kwa mfano, kwenye hospitali hiyo kumekuwa na gari hilo la wagonjwa. Hali kadhalika tumepata gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya cha Chiungutwa. Hali kadhalika tumepata gari kwenye Kituo cha Afya cha Chikolopola. Hali kadhalika tuna mpango wa kujenga vitu vya afya takribani viwili kwa kipindi hiki; kipindi hiki tumebahatika kujenga vituo vya afya viwili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma tulikuwa na vituo vya afya viwili tu; Kituo cha Afya cha Nagaga na Kituo cha Afya cha Chiungutwa lakini nikiwa kama Mbunge wa jimbo hili nimebahatika kupata vituo vya afya vinne sasa hivi; Kituo cha Afya cha Chikolopola kimejengwa kimekamilika, lakini kuna Kituo

cha Afya cha Namwanga ambacho tumepata kiasi cha shilingi 457,585,331. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika tumepata pesa katika Kituo cha Afya cha Mkululu, shilingi takribani 250,000,000 kwa kipindi hicho kifupi. Hivi nani kama Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan? Tunaweza tukasema hakuna. Kwa wema wote huu aliotufanyia hivi kwa nini tusimpe kura kwa 100%? Hicho ndiyo tunachoweza kukifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiacha hapo tulikuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano katika Jimbo la Lulindi. Wakati ninaingia maeneo mengi sana kulikuwa hakupatikani mawasiliano. Ninakumbuka pale dada Mheshimiwa Malembeka alitolea mfano, akizungumza kipindi hapo, lakini hiyo ilikuwa ni miaka ya nyuma. Ninaona yeye hakuwa na taarifa sahihi ya hali halisi ilivyo sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mawasiliano katika Jimbo la Lulindi yameimarika sana. Ninapenda nimwambie dada Mheshimiwa Malembeka kwamba, mwaka 2020/2021 mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo La Lulindi nilienda kwa Mheshimiwa Dkt. Ndungulile na kumwomba changamoto niliyokuwa nayo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kumwambia kwamba, kwa bahati njema kwa mara moja aliweza kunipatia minara takribani 13 ambayo ilienda kumaliza changamoto kubwa ya mawasiliano kule, lakini hata hivi sasa ninavyosema bado kuna ujenzi wa minara mingi. Mfano, kuna Mnara wa Mijelejele tumeujenga takribani mwezi uliopita, umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mnara wa Umati, umekamilika, umejengwa hivi karibuni. Kuna Mnara wa *YAS* pia tumeujenga katika Kata ya Mitesa, umekamilika na unatumika. Kuna mnara mwingine tunaujenga Njechele sasa hivi wa *Vodacom* na utakamilika na kuna mnara umejengwa Sindano, hivyo hali kadhalika umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kuwahakikishia kwamba kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hakuna ambacho hakiwezekani. Takribani kila kitu kimefanyika katika jimbo langu. Pamoja na hayo, bado tutaendelea kuomba kwa sababu sisi saa zote mahitaji hayaishi, ni binadamu, lakini ukishaomba haina maana kwamba hakuna kisichofanyika, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tupongeze juhudi kubwa na wananchi wa Tanzania kwa pamoja tunajipongeza, lakini tunampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na kumtumainia kuwa ni kiongozi shupavu ambaye amefanya mambo makubwa. Mambo hayo yanaonekana kila eneo. Hatuna shaka kwenye hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kushauri jambo kwenye suala la kodi kama nilivyosema. Kodi yetu imekuwa na changamoto hususan katika eneo la mamlaka za udhibiti. Mamlaka za udhibiti zimekuwa nyingi sana. Mamlaka hizi zimekuwa zikitishia hata amani ya ile sekta isiyo rasmi kubadilika kuwa rasmi. Kinachotokea mpaka sasa hivi kumekuwa na changamoto kwamba sekta isiyo rasmi imekuwa ni kubwa. Ni 54% kitu ambacho kinafanya sasa hata sekta hii kukua, kubadilika kuwa walipakodi inashindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wamekuwa wanaogopa kujitambulisha kuwa rasmi kwa kuhofia ada kutoka kwenye sekta hii...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mengine mwandikie Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli...

**NAIBU SPIKA:** Nimekupa takribani dakika ishirini.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nikushukuru na ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Kuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Wageni 21 wa Mheshimiwa Cosato David Chumi, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ambao ni Vijana wafanyakazi wa *Catholic,* Viwawa kutoka Parokia ya Mtakatifu Paulo wa Msalaba Kanisa Kuu Jijini Dodoma. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa *Captain* Abbas Ali Mwinyi. Mashekhe kutoka Jimbo la Fuoni Zanzibar. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa Abbas Gulam Tarimba amba oni Walimu wa Shule ya Msingi Mapambano Sinza, Jijini Dar es Salaam. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni Tisa wa Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Taasisi ya Bega kwa Bega na Tanzania kutoka Mkoani Pwani na Singida. Karibuni. *(Makofi)*

Wageni 10 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ambao ni *Kingdom Leadership Network* Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Mheshimiwa Kakunda, wajiandae Mheshimiwa Getere na Mheshimiwa Dkt. Kalemani.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru sana nipate fursa hii ya kuchangia maoni yangu kwenye hotuba mbili. Kwanza, nimpongeze sana Ndugu yangu Profesa Kitila Mkumbo pamoja na Naibu Waziri wake na timu

nzima ya wataalam wa Wizara hii ya Mipango na Uwekezaji kwa hotuba nzuri sana iliyoonesha hali ya uchumi kwamba tuko vizuri, hongera sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, pongezi za pili, nimpe Mheshimiwa mwanafamilia mwenzangu katika sekta ya Uchumi Ndugu yangu Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, pamoja na Naibu Waziri wa Fedha na timu yao yote ya Wizara ya Fedha kwa kutupatia taarifa nzuri ya utekelezaji wa bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na mapendekezo mazuri ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Hongera sana pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wote hawa pamoja na Mawaziri wote akiwemo Waziri Mkuu wanatekeleza kazi zao za kila siku kwa kuongozwa na maelekezo ya Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, nimpongeze sana yeye kama Kiongozi Mkuu wa Nchi, kwa sababu haya matokeo yote mazuri ambayo yameelezwa na Mawaziri wetu hawa wa Mipango na Fedha yote haya, kama yasingekuwa maelekezo yake basi tusingepata mafanikio ambayo tumeyapata. Kwa hiyo, ninampongeza sana Rais kwa mafanikio yote haya, mipango yote mizuri, utekelezaji mzuri licha ya kuwa tuna changamoto za hapa na pale lakini kwa kweli tuko vizuri. Hongera sana Serikali, hongera sana kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, miongoni mwa mafanikio ambayo yameelezwa kwa ufasaha kabisa kwenye hotuba hizi mbili pamoja na taarifa ya Kamati ni uboreshaji wa ukusanyaji wa mapato ya ndani. Tunawapongeza sana wote, lakini tunawapongeza zaidi *TRA*, vilevile tunawapongeza Halmashauri zote za Majiji, Miji, Halmashauri za Wilaya kwa jinsi ambavyo nao vilevile wameboresha ukusanyaji wa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio mengine ni ongezeko la upatikanaji wa fedha za maendeleo hasa kwa ajili ya miradi mikubwa ya kimkakati. Miradi mikubwa ya kimkakati ni uti wa mgongo wa uchumi wa nchi yetu, miradi katika sekta mbalimbali. Nami nitagusia maeneo muhimu machache ambayo tumeshuhudia kuimarika kwa utekelezaji na matokeo yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili uchumi wa nchi uweze kukua ni lazima sekta binafsi ishiriki katika kujenga uchumi wa nchi. Sekta binafsi inashiriki zaidi kupitia wawekezaji wa ndani na nje. Serikali yetu imekuwa ikifanya juhudi nyingi sana katika kuvutia Wawekezaji wa ndani na nje wawekeze fedha, ili mtu awekeze fedha anategemea apate faida. Bila juhudi za Serikali kuwekeza fedha nyingi kwenye maeneo muhimu bado tungekuwa tuko nyuma katika kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa sekta hizo ni zipi ili tuwavutie zaidi wawekezaji. Kuna maeneo manne muhimu ambayo ni lazima tuyaangalie, tuendelee kuyaangalia kwa kina sana, kwa umakini. Eneo la kwanza, wawekezaji wanahitaji sana usafiri na usafirishaji wenye gharama nafuu. Usafiri na usafirishaji, usafiri wa watu na usafirishaji wa bidhaa wenye gharama nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunazo sekta nyingi ambazo zinachangia kwenye kuchangia gharama nafuu za usafiri na usafirishaji. Kwanza kuboresha barabara, barabara za lami, barabara za changarawe, madaraja, vivuko, kuboresha ujenzi wa reli, kuboresha viwanja vya ndege na kuboresha bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, keshokutwa Mheshimwia Rais atakwenda kuzindua Daraja la Kigongo – Busisi. Ni miongoni mwa madaraja makubwa ambayo yanahitajika kwenye sekta hii ili kuendelea kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji. Serikali imefanya makubwa sana, imefanya makubwa sana katika sekta hizi. Tumeona jinsi ambavyo nchi yetu inaendelea kutandazwa kwa barabara za lami na kuimarishwa kwa barabara za changarawe zipitike muda wote wa mwaka; kuimarisha madaraja na kadhalika, maeneo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia ujenzi wa Reli ya Viwango vya Kimataifa unayoendelea nchini na tunaona jinsi ambavyo hata wenzetu katika nchi za nje wakija hapa wanashangaa hiki kipande tu cha *SGR* kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma, wenzetu watu wa nje wanashangaa. Sasa je, tutakapomaliza ifike Tabora, ifike Mwanza, ifike Kigoma, iende mpaka Burundi, iende mpaka mpakani mwa Rwanda, tutakuwa tumepata mafanikio makubwa sana. Ninaomba sana Serikali

iendelee kuwekeza kwenye sekta hizi ili kuendelea kupunguza gharama za usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *interest* yangu hapa kama Mbunge wa Jimbo la Sikonge ni kuona kwamba Kanda ya Kati, Kanda ya Magharibi nayo inaunganishwa na Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa maana ya Barabara ile ya kutoka Mwanza ifike Mbeya, kipande ya Ipole – Rungwa, kipande cha Rungwa – Makongorosi, kipande cha Rungwa – Mkiwa, navyo viwe vya lami ili kuunganisha hizi Kanda zetu za nchi, kuunganisha na nchi jirani, kuunganisha Tanzania na Malawi, kuunganisha Tanzania na Zambia, kuunganisha Tanzania na Burundi, Rwanda, Uganda na kadhalika, kwa kupitia hizi barabara kubwa. Hiyo ni changamoto kwenye eneo langu ambalo ningependa nimkumbushe sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Waziri wa Mipango aendelee kuiangalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa ambazo unaziona kwenye eneo hili ziko mbili. Kwanza ni ile barabara ambayo nimeitaja, lakini ya pili ya Kitaifa, nimesafiri juzi kwenda Dar es Salaam kwa *SGR* nilitumia muda mchache kama masaa manne na nusu, niko Dar es Salaam, kwa hiyo, jambo hili la *SGR* ni jambo la kupongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kurudi nilichagua nisafiri kwa *bus* la kawaida nikaingia kwenye *Bus* linaitwa Kaizirege ambalo linaenda Bukoba. Nimeingia kwenye *bus* Saa Nne Asubuhi nimeteremka kwenye kituo chetu cha *bus* pale Dodoma Saa Nne Usiku, ina maana masaa 12. Maana yake ni nini, maana yake ni kwamba wakati tunaboresha njia nyingine za usafirishaji kama reli, viwanja vya ndege na kadhalika, tunahitaji kuendelea kuboresha barabara zetu. Kwa mfano, kwa mahitaji ya sasa hivi kama nilivyoona juzi, ninadhani tunahitaji kuwa na mipango ya kujenga barabara nne kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma, hiyo itapunguza sana masaa ya kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, wawekezaji wanahitaji nishati ya uhakika. Nishati hapa maana yake ni umeme, gesi asilia, makaa ya mawe mpaka na chuma, hizi zote zinaingia kwenye nishati ya uhakika. Hivi karibuni Serikali yetu

imekamilisha ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere na nchi yetu ni lazima nikumbushe imeichukua miaka 112 kukamilisha bwawa hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 1903 Mhandisi wa Kijerumani ambaye anaitwa *Stigler* ndiye alifika kwenye maporomoko hayo ya *Stigler*, ambayo yalikuwa yanaitwa maporomoko ya *Stigler* ambapo ndiyo sehemu iliyojengwa bwawa, akaandika mradi wake mwaka 1904 akaukamilisha mradi ambao ulikwenda kuwasilishwa kipindi kile cha ukoloni, ulikwenda kuwasilishwa kwenye Bunge la Ujerumani – *Bundestag.* Mwaka 1905 mradi ule ukapitishwa na Bunge la Ujerumani mwaka 1905, ukaanza kujengwa mwaka 1906 mwezi Julai, wakati ambapo wanaanza ujenzi wa tuta, tarehe 12 Julai, 1907 yule bwana *Stigler* ambaye ndiye alikuwa anasimamia ujenzi wa Bwawa akakamatwa na tembo, akapigizwa chini akafariki.

Mheshimiwa Naibu Spika, yeye alifikiri tembo ni sawasawa na tembo wa India ambao watu wanapanda juu ya mgongo wa tembo, alipomsogelea tembo akamkamata, akampigiza kichwa chini akauawa. Kwa hiyo akakosekana Mhandisi mwingine wa kusimamia huo mradi mpaka Ujerumani walipoondolewa kupitia Vita Vikuu vya Kwanza vya Dunia. Waingereza walifanya utafiti wa hapa na pale na kadhalika, lakini hawakuweza kutekeleza ule mradi mpaka tumepata uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uhuru, Mwalimu Nyerere alijaribu hapa na pale kutaka kujenga mradi huo, lakini ilishindikana. Akaja Mzee Mwinyi napo ikashindikana, akaja Mzee Mkapa napo ikashindikana, akaja Mzee Kikwete napo ikashindikana, juhudi mbalimbali zilifanyika mpaka Mzee Magufuli, marehemu akaamua sasa liwalo na liwe akafanya maamuzi magumu ya kuanza kujenga bwawa hilo mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ninawapongeza sana Marais wetu. Wakati anafariki marehemu Magufuli tulikuwa bwawa lile liko chini ya 60%, lakini Mama Samia Suluhu Hassan ameendeleza ujenzi huo, amehakikisha bwawa hilo limekamilika, hiyo ni sifa kubwa sana kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumechukua miaka 112 kuweza kujenga na kukamilisha bwawa hilo, ni jambo muhimu sana. Huu ni mradi wa kipekee ambao utazalisha megawati 2,115, ni mradi wa pekee ambao unakwenda kuiokoa nchi hii katika upungufu wa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa changamoto ambazo bado zimebaki ambazo ni muhimu sana Serikali iendelee na mpango wake katika kuiangalia. Kwanza ni njia za kusafirisha umeme huo lazima ziimarishwe. Pili, vipoozeo, vituo vya kupooza umeme lazima vijengwe vikamilike na viimarishwe. Mwisho ni njia za kusambaza umeme kwa wananchi lazima nazo ziimarishwe.

Mheshimiwa Naibu Spik, tunashuhudia kwamba tumepeleka umeme kila kijiji lakini kila kijiji *transformer* iliyopo kule mara nyingi wameanza na *50KV*. *Transformer* ya *50KV* ambayo ndani ya muda mfupi inakwisha uwezo wake. Kwa hiyo, ni lazima Serikali iendelee kuwekeza ili kwanza kwenye vijiji ambavyo vina umeme tuviongezee kutoka *KV*50, *transformer* iwe *KV*100 au 200 ili wananchi waweze kupata umeme wa uhakika. Nyaya zile za kusafirisha umeme, vituo vya kupooza umeme na kadhalika. Kwa hiyo hizo ni changamoto ambazo zinatakiwa tuendelee kuzifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna uwekezaji kwenye Sekta ya Gesi Asilia. Mipango ipo mizuri sana, ninaomba Serikali iendelee kama ambavyo imeahidiwa kwenye huduma iendelee siyo kutamka maneno tu iendelee kwa vitendo kuhakikisha kwamba ndani ya miaka michache ijayo tunakuwa na miradi ya gesi asilia ambayo itaingia kusaidia uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mradi wa makaa ya mawe na mradi wa chuma wa Mchuchuma na Liganga vilevile ni muhimu sana kwa nchi hii kama tunataka kweli maendeleo, ni lazima Serikali iendelee na mipango yake kuhakikisha kwamba hiyo miradi inatekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu, wawekezaji wanahitaji nguvu kazi yenye ujuzi inayopatikana kwa urahisi ndani ya nchi. Kuna baadhi ya maeneo ya ujuzi mpaka leo ni lazima

tuagize watu kutoka nje ya nchi au tupeleke watu nje ya nchi. Kwa hiyo, ninapongeza sana juhudi za Serikali za uwekezaji kwenye Vyuo Vikuu, uwekezaji kwenye *VETA* kila Wilaya, uwekezaji kwenye Vyuo vya Kati hasa Mikopo ya Elimu ya Juu kwenye Vyuo vya Kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo ninaiona mimi ni mitaala. Mitaala yetu mingine ina matatizo, inatoa wahitimu ambao hawawezi kusaidia, hawahitajiki kwenye sekta hizi ambazo zinahitaji nguvu kazi yenye ujuzi. Kwa hiyo, ninaomba Serikali wakae, watafakari kwa kina hii mitaala ambayo inatolewa na vyuo vyetu ni muhimu sana kuiangalia. Kweli kwa mfano, tunahitaji Maafisa Utumishi, lakini Maafisa Utumishi wa ngazi gani ambao tunawahitaji. Je, Maafisa Utumishi wa Cheti wapo ambao wanahitajika ambao wanaweza wakaajiriwa, kwa nini tunapeleka watoto wakasome cheti kwenye vyuo na tunahitaji wangapi? Kama tunahitaji Maafisa Utumishi wenye cheti kwa mwaka 400, basi tusisomeshe Maafisa Utumishi 10,000 somesha tu hao 400 ambao wanahitajika, vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwangu nimeanza kuwakataza wazazi, anayekuja kuomba ushauri kwangu ninamwambia ahaaha, anakwenda kusoma nini, anakwenda kusoma umeme, ninamwambia hapo sawa, ufundi umeme sawa. Anakwenda kusoma nini, anakwenda kusoma ufundi gereji, ninamwambia sawa, anakwenda kusoma nini, anakwenda kusoma, hii bwana anakwenda kusomea Cheti cha Biashara, ahaaha sasa mambo tunashauriana katika hayo. Kwa hiyo, mitaala ni lazima kuipitia ichangie upatikanaji wa nguvu kazi inayohitajika kwenye sekta za uzalishaji mali kama za kilimo, viwanda na biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitaji la nne ni wawekezaji hasa wa viwanda. Wawekezaji hasa wa viwanda wanahitaji malighafi inayopatikana kwa mwaka mzima. Malighafi inayopatikana kwa mwaka mzima, changamoto bado zipo. Viwanda vingi vinapata malighafi miezi minne, miezi mitatu, miezi mitano kwa mwaka, miezi mingine wanafunga uzalishaji kwa sababu hakuna malighafi. Hiyo ni mpaka sekta hizi za kilimo kwa mfano mpunga, viwanda vya kuchakata mpunga vinafunga miezi sita, vinafunga miezi, kwa sababu ya malighafi kutopatikana. Hata viwanda vya

kukamua mafuta ya alizeti navyo vinafungwa miezi mitatu, miezi sita vinafunga kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo sekta hii ya kilimo inatakiwa kuendelea kui-*support* ili itoe malighafi kusaidia viwanda vya ndani vipate malighafi kwa mwaka mzima ili kutunza ajira za watu wetu. Ajira katika sekta ya uzalishaji viwandani ni jambo la muhimu sana na kwenye ilani ya uchaguzi imeshawekwa muda mrefu tangu mwaka 2005, kwamba katika utekelezaji wa mipango yetu ya kupambana na umaskini tutaimarisha au tutaongeza ajira kwenya sekta za uzalishaji viwandani *(industrial manufacturing)* angalau ifike 80% ya ajira zote nchini, sasa hapo sijui tutafika lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo la kufunga viwanda kwa kukosa malighafi ni jambo ambalo linatakiwa tulifanyie kazi hasahasa miaka hii mitatu, minne ijayo katika kuchangia ile *vision* ambayo tunaipitisha chini ya Profesa Kitila Mkumbo, ni muhimu sana tuweke *base* ili kuhakikisha kwamba hii malighafi ikipatikana itasaidia sana ajira za viwandani na itasaidia sana viwanda vyetu vifanye kazi kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kupongeza sana jihudi zinazofanyika katika kuboresha sekta ya kilimo kwa ujumla. Kuna mabwawa mengi yanaanzishwa ya umwagiliaji, lakini kuna visima 67,000 Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameshatutangazia hapa ni muhimu sana, pia utafiti wa mbegu na masoko, mipango hiyo ikitekelezwa itasaidia sana kuboresha hali ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nimshukuru sana Rais Samia ametuangalia sana Sikonge. Huwa ninasema kila siku kuwaambia watu wangu wa Sikonge, hakuna mradi wowote ambao tulipeleka kwake kupitia kwa Mawaziri hawa ambao ulikataliwa, miradi karibu yote iliungwa mkono, labda tu sehemu ambapo tunaambiwa kwamba kidogo tusubiri upatikanaji wa fedha, hapo tunasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuna deni na Mama Samia kwenye sekta ya miundombinu, kwenye sekta za huduma za jamii, elimu, afya, maji na sekta za uchumi. Changamoto ni kama

tu ambazo nimezieleza hapo mwanzo, kwa kweli tunasubiri ku-*tick* Oktoba ikifika, basi. Tunamuunga mkono Rais Samia, tunaunga mkono CCM na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Getere, jiandae Dkt. Kalemani, Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla jiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara, hizi Wizara mbili ya Fedha na Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wengi tumezungumza humu ndani na kiukweli tumeitendea haki Serikali hii ya Chama Cha Mapinduzi na tunaendelea kuitendea haki katika hii Wizara iliyobaki. Nimpongeze sana Mheshimiwa Mwigulu kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka wakati ameteuliwa ilikuwa 31 Machi, 2021 hiyo tarehe ninaikumbuka sana, kwa sababu kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha kwa nchi mbalimbali duniani maana yake ni kamtihani kako hapo, sasa ni miaka minne jamaa yetu bado anadunda yupo, anaendelea vizuri amefanya kazi kubwa sana ya kumsaidia Rais, ametafuta mikopo, amesimamia fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiwa Waziri wa Fedha wewe ndiyo unaangalia kila kitu kilichopo hapa kinachoendelea. Miradi inayoendelea vizuri, miradi mikubwa, miradi ya kimkakati na kila eneo yeye ndiye anayemsaidia Rais kwenye jambo hilo, tunampongeza sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Getere, hiyo sauti ya juu unapongeza au unalalamika? Hapa siyo Tarime, zungumza. *(Kicheko)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru kwa kuniambia nipunguze, lakini hii sauti siyo ya Dar es Salaam ni ya Mara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha (Mheshimiwa Chande) kwani anafanya kazi vizuri sana na Mheshimiwa Waziri wake. Pia, Waziri wa Mipango, Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo amebahatika kuwa na akili nyingi (ana akili za kitaalam na akili za kisiasa). Pia, ni *political analyst,* anachambua kila kitu kinachoonekana cha kiuchumi na cha kisiasa; anafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru Mheshimiwa Nyongo, Naibu Waziri, kwani anafanya kazi vizuri na Mheshimiwa Waziri. Wanafanya kazi ya kuangalia mipango yetu na dira, lakini pia wanamsaidia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kwenye suala la kutengeneza bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Fedha; wanafanya kazi nzuri sana. Pia, ninamshukuru Kamishna Mkuu wa *TRA*, ametumika vizuri kukusanya hela zetu na ndiyo zinakuja kwenye miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kipekee pia niwashukuru sana watumishi wote wa Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge. Tumekaa nao kwa muda mrefu, wamefanya kazi nzuri ya kufungamana na sisi hapa pamoja na kuhudumia maeneo mbalimbali yanayohitajika; ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Nilikuwa ninaangalia wakati fulani Waheshimiwa Wabunge na watu wengi walikuwa wanazungumza kwamba sisi katika nchi yetu ya Tanzania hatuna *consistency* (kila Rais anayeingia ana mipango yake), lakini Mama Samia ameingia akasema ngoja nifuate yale ambayo wataalam wanasema.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nikajiuliza huyu Mama naye mchumi au nini? Nikaangalia kumbe Mama ametumia uchumi wake wa Chuo cha Manchester – Uingereza vizuri sana. Pia, umahiri wa *degree* yake ya maendeleo ameitumia vizuri sana. Miradi yote aliyoikuta ameimaliza na mingine imebaki kidogo anamalizia. Kwa hiyo, hana namna; amefanya kazi ya kushauriwa vizuri na amefuata vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, duniani hapa mambo ni mawili tu; *good advice or bad advice* (ushauri mzuri au ushauri mbaya). Ukishauriwa vizuri ukafuata utafanikiwa, ukishauriwa vibaya ukafuata utakwenda zako. Kwa mfano wewe kama kuna genge la wavuta bangi wanakwambia toka kwenye hilo genge, wewe ukaendelea nalo na wewe utakuwa mvuta bangi. Kwa hiyo, mama ameshauriwa vizuri na yeye amejiongeza kwenye elimu yake ya *degree* alizozipata ametumikia vizuri na miradi yote inaenda kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi Mara kikubwa kabisa ambacho kilikuwa kinatusumbua kwa Mkoa wa Mara ni Hospitali yetu ya Kwangwa ambayo imekaa muda mrefu sana. Sasa inaenda kumalizika; Mama ametoa hela imebaki maeneo machache sana. Kwa hiyo, tunaenda kuyamalizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa kingine ambacho tulikuwanacho ni Uwanja wa Ndege wa Musoma ambao sasa na wenyewe umekaribia kidogo kumalizika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine ambacho tunaomba sasa ni Bandari yetu ya Musoma ambayo imekwama kwa muda mrefu. Ikiwezekana huko wanakokwenda Mheshimiwa Dkt. Mwigulu na Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo tafadhali, kama tulikuwa na mradi ambao bandari ilikuwepo imekufa mpaka leo haijafufuliwa na maeneo mengine tumeyafufua; tunaomba eneo hili nalo mje waliangalie liweze kutusaidia kwenye maisha yetu katika Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mengine ambayo nitazungumza leo ni kuhusu miradi iliyopo kwenye Jimbo la Bunda. Nikiwa Mbunge 2015 – 2020, sasa hivi tunaenda 2025 kulikuwa na tatizo kubwa la Barabara ya lami ya kutoka Nyamuswa kwenda Bunda; imekamilika ambayo inatoka Nyamuswa – Bunda – Buramba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetumia shilingi bilioni 52 na *point* ambayo Mama Samia katoa. Hiyo barabara imekamilika inapitika vizuri na pale Nyamuswa taa zimewekwa; kwa hiyo mji umependeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na Barabara nyingine ambayo inatoka Makutano inakuja Butiama – Sanzati. Barabara imekamilika kwa shilingi bilioni 52 na *point* na yenyewe. Sasa tatizo tulilonalo kwenye hiyo barabara ni suala la kutoka Sanzati kwenda Nata. Sasa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu kuna siku moja nimekaa na wewe hapa na Mheshimiwa Naibu Waziri ukaagiza shilingi bilioni mbili ziende pale kumaliza hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tafadhali, ninaomba sana hili tamko ambalo alilitoa Mheshimiwa Waziri liendelee kuwepo. Ile barabara imekuwa kero kwani imetengenezwa kwa 65%, bado 35%. Tunaomba shilingi bilioni mbili ziende zimalizie hiyo barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kwa Jimbo la Bunda tumepokea shilingi bilioni 4.6 za ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bukama ambayo inaenda kumalizika. Sasa hivi tumepelekewa shilingi milioni 980, tunaenda kusubiri kama hospitali itamalizika na itaendelea vizuri. Pia, tuna vituo vya afya; tuna Kituo cha Afya Mugeta kimejengwa kwa shilingi milioni 480, kimekamilika na kinatoa huduma, lakini bado uzio. Ninadhani tutamalizia kwani tumeomba hela za kwenda kumalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya cha Hunyari tumejenga kwa shilingi milioni 500 ambazo Mama Samia ametoa, lakini bado *theatre* (jengo la upasuaji) halijakamilika. Tunaomba Serikali sasa; tumeshaomba shilingi milioni 200 ya kumalizia jengo lile liweze kumalizika na fedha zimetoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kituo kipya cha Mihingo, kimetolewa shilingi milioni 250. Sasa hapa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ninaomba hapo anisikilize vizuri ndugu yangu. Mama Samia ameamua kutoa fedha za vituo vya afya vya kimkakati na fedha zimeingia halmashauri. Halmashauri inahamisha zile fedha kutoka halmashauri kwenda kwenye maeneo ya *site* kama kule za kwangu za Mihingo zinatakiwa ziende Zahanati ya Mekomariro.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo ni wiki ya tatu wanaenda wanasema mifumo, mifumo, mifumo. Ninaomba fedha za Mheshimiwa Rais zimetoka zipo Halmashauri ya Bunda.

Kwa nini sasa hiyo mifumo haziendi kwenye *site*? Ninaomba kama mifumo hiyo inahusika na Wizara waitatue zile fedha ziende *site*. Wananchi wanasubiri kituo kipya; wamepeleka viashiria, hela hazionekani. Ninaomba sasa katika hilo tuone kwamba fedha hizo zinaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo tunalo katika Jimbo la Bunda ni sekondari tano. Tumejenga sekondari tano mpya; kuna Sekondari ya Tingirima tumetoa shilingi milioni 470 lakini kuna majengo ya *biology*, fizikia na kemia hayajakamilika. Tunaomba Serikali imalizie na tumeshaomba fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna shule mpya ya Sanzati na hapa ninaomba Mheshimiwa Waziri wa Elimu na wa TAMISEMI tuelewane vizuri. Wananchi waliamua kujenga shule, wakachanga shilingi milioni 80 na Serikali ikawapa shilingi milioni 140. Sekondari imejengwa lakini sasa madarasa kuongezwa inakuwa shida na jengo la utawala halipo. Tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, wataalam wake wafike kwenye Sekondari ya Sanzati waisaidie kujenga madarasa yaliyobaki kwa sababu ni shule ya wananchi na jengo la utawala liwepo na vyumba vya madarasa viongezeke.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Sekondari ya Mariwanda tumepewa shilingi milioni 580, inamalizika. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupa hiyo fedha. Kuna Sekondari ya Nyaburundu tumepewa shilingi milioni 580, inaenda kukamilika. Pia, tuna Sekondari ya Matimwelo tumepewa shilingi milioni 580 ambayo na yenyewe inaenda kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaanzisha pia *high school* mpya. Tuna *high school* ya Makongoro tumepewa shilingi milioni 580 inaenda kukamilika pamoja na *high school* ya Hunyari ambayo tumepewa shilingi milioni 270 ambako wanajenga mabweni na inaenda kukamilika. *High School* ya Makongoro tumejenga bwalo la wanafunzi pamoja na mabweni hivyo inaenda kukamilika ambapo tumetumia shilingi milioni 580. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa upande wa Jimbo la Bunda kwa maana ya elimu tunaendelea kufanya kazi. Suala

ambalo tunalo kubwa ni suala la maboma ya shule za msingi. Shule za msingi Mradi wa *BOOST,* sasa tunafikiri kwamba kwa nini Mheshimiwa Dkt. Mwigulu aangalie sana hii miradi ya kimkakati. Kuna Shule za Msingi Masaba, Chamtikiti, Salakwa, Salama A na Salama B, pamoja na Songambele hali ni mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo shule za msingi maeneo mengi tumemwandikia Mheshimiwa Waziri. Tunaomba fedha zile za *boost* ziende ziwasaidie kama zipo kwa sababu tuliambiwa zinaenda mwezi Machi lakini hazijaenda; mwezi Aprili pia hazijaenda, na mwezi Mei pia hazijaenda. Kwa hiyo, ninafikiri kwamba zitaenda lakini zikienda zitasaidia sana kwenye maeneo hayo ziweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwetu sisi Mara na hasa Jimbo la Bunda tulikuwa tunajiuliza; kwa nini maji yatoke Ziwa Victoria yasafiri kilometa karibu 1,000 yaende Tabora, yaje Dodoma na sisi kilometa 20 tu maji hamna? Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Mradi wa Maji wa Kutoa Maji ya Ziwa Victoria kutoka Butiama kuja Nyamuswa (shilingi bilioni 21). Kusema ukweli hatuna cha kusema ilikuwa ni kama aibu fulani hivi. Sasa hivi hiyo aibu tumeiondoa, mradi unaendelea vizuri. Tunajua utakamilika na ukikamilika utasambaa vijiji vyote vya Jimbo la Bunda na watu wa Bunda watakuwa wamefaidi maji ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi midogo midogo ya maji. Tuna mradi wa shilingi milioni 450 Mariwanda unafanya vizuri; mradi wa shilingi milioni 830 - Hunyari unaendelea kufanya vizuri lakini pia tumepelekewa tena shilingi milioni 270 kumalizia ule mradi. Pia, mradi wa shilingi milioni 450 wa Kiroreni na Kambubu unaendelea vizuri na miradi mingine ambayo tumepeleka Sanzati ya shilingi milioni 500 imekamilika na wananchi wanakunywa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kwa Jimbo la Bunda Mama Samia amefanya kazi kubwa sana. Sasa kwangu mimi ninaona kama mtu mtaalam wa kisiasa maana yake sisi tumefanya siasa muda mrefu; utakuta watu wana vimaneno maneno kwa Mheshimiwa Rais, mara wanachonga maneno maneno; wamechelewa sana. Kifupi wataalam wanasema hili limeshatiki; wamechelewa mno. Mama ameshashinda muda

mrefu, ni kura ngapi ameshinda ndiyo hatuelewi, lakini suala la kushinda alishashinda; wamechelewa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kisiasa mtu akishapeleka nguvu kubwa ya utendaji kiasi hiki hakuna namna ya kumzuia. Kwa hiyo suala halipo, Chama Cha Mapinduzi tunaamini mwezi Oktoba bendera ya Chama Cha Mapinduzi itapepea vizuri. Waheshimiwa Wabunge wote Mungu atujalie turudi wote kwa maana Mama yeye alisharudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ninakuombea uendelee vizuri, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Kalemani, wajiandae Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla na Mheshimiwa Tarimo.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ninaunga mkono hoja na bajeti kwa asilimia zote. Pia, ninaomba nitoe shukrani nyingi sana kwa chama changu (Chama Cha Mapinduzi) kwa kumchagua na kumpitisha Mwenyekiti wa Chama chetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa Kiti cha Urais. Hongereni Chama Cha Mapinduzi, wamefanya kazi kubwa na tumefanya mapema bila kuchelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na kuaminika kupitia Chama chetu kupeperusha tena bendera mwaka huu kama Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninamtakia kila la kheri na mafanikio makubwa kwenye harakati hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza *comrade* Balozi Dkt. Nchimbi kwa kuaminika na Chama chetu kuwa mgombea mwenza wa Kiti cha Urais. Tumpigie makofi sana

na tunamtakia kila la kheri. Amefanya kazi kubwa kwenye utendaji wa Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajadili bajeti kubwa ya shilingi trilioni 57 hivi. Nimepitia majalada ya wawasilishaji wa bajeti zote na nimepitia kwenye mtandao pia bajeti za nchi za Afrika Mashariki. Ukipitia bajeti yetu utaona bajeti yetu kwa nchi za Afrika Mashariki inaongoza kwa ukubwa na inaongoza kuwa na *reflection* nzuri za bajeti ya wananchi. Kwa hiyo, kwanza sisi wenyewe tujipongeze kwa kupitisha bajeti hii kubwa nono inayokwenda kutatua kero za Watanzania wa kawaida. Sababu za kupongeza na kuunga mkono ni kama zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kwa utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuvunja rekodi ya utekelezaji wa miradi kabambe na ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi almaarufu Daraja la Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alieleza Mheshimiwa Waziri na yeye ninampongeza sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa pamoja na Naibu wake na watendaji. Daraja hili limesemwa ni refu ambalo ni kilometa 3.2 hivi. Siyo urefu tu, ni zuri pia. Mimi nimepita kule juzi; ni zuri na ni imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Daraja hili litarahisisha sana shughuli za kiuchumi kwa Watanzania na hasa wa Kanda ya Ziwa. Ilikuwa ni changamoto kubwa sana wananchi kutoka Mwanza kuvuka kwenda Kagera na kutoka Geita na maeneo mengine kwenda Mara, lakini leo wananchi wanapita kirahisi sana. Pia, bahati nzuri sana hata Wakenya waliokuwa wanakwama wanakwenda kupita kufanya biashara zao kwenda Mwanza na maeneo mengine mpaka Kagera na *DRC* kwa urahisi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kulikamilisha Daraja hili la Kigongo – Busisi. Ninataka niungane na wananchi wengine kwa kumpongeza. Jana nilipita kule na akinamama tunafuatana pale

wamebeba mchicha wanauza wakawa wanasema, kwa nini tusiruhusiwe kuuzia kwenye Daraja hili kwa sababu ni zuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona mafanikio ya mapema sana na wengine wanasema, kwa nini tusiwe tunatembeaga kwa miguu bila hata kiatu wakati mwingine? Wakaendelea kusema, si turuhusiwe hata kuwa tunajisugulia hapa kwa sababu ni zuri sana? Kwa hiyo, unaweza ukaona mafanikio ya haraka haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ukamilishaji wa Daraja la Kigongo – Busisi unakwenda kufungua fursa za kiuchumi. Nirudie tena kumpongeza Mheshimiwa Rais na tumuunge mkono sana kwani keshokutwa analizindua kwa kukamilika. Nitumie nafasi hii kama Mbunge wa kawaida kuwaalika wananchi wenye uwezo wa kufika pale washuhudie uzuri wa Daraja hili na kumuunga mkono Mheshimiwa Rais katika juhudi zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa *SGR*. Mradi huu ni mkubwa sana na nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha kwa utoaji wa fedha. Ujenzi wa mradi wa reli ya umeme kutoka Dar es Salaam mpaka Dodoma umeshakamilika na mafanikio yake tumeambiwa na nimesafiri mara mbili, mara tatu. Pia, ninafahamu wananchi wengi wanasafiri zaidi, lakini mpaka sasa limeshaleta mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa ninapitia taarifa za Mheshimiwa Waziri kwamba zaidi ya watu milioni mbili wameshasafiri kwa sasa na hapo ni umbali mfupi tu wa kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninafahamu pia Mheshimiwa Rais na Serikali wanaendelea kujenga mradi huu. Hivi karibuni watakamilisha kujenga tena Makutupora kuelekea Tabora kama kilometa 368 hivi. Hiyo ni juhudi kubwa ya Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha ili pia *SGR* ijengwe mpaka ukanda ule. Pia, itajengwa kutoka Tabora mpaka Kigoma kilometa 506 hivi. Ni parefu kweli kweli siyo mchezo na itajengwa kutoka Tabora mpaka Mwanza kilometa 341. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii ikishapita maana yake nini? Maana yake ni kwamba *SGR* inakwenda kukamilika kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na itajengwa kutoka Mwanza mpaka Isaka kilometa 165. Pia, itakwenda kutoka Tabora mpaka Uvinza na Uvinza mpaka Msongati – Burundi. Ninaomba tupigie makofi sana bajeti hii kwani itakuwa na manufaa makubwa sana kwa Watanzania na wananchi wengine na mpaka nchi za jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa sasa hakuna uzembe wa kuyasemea mazuri ambayo Serikali imeyafanya. Ninawashukuru wananchi na Waheshimiwa Wabunge. Bajeti hii ni ya wananchi, maana yake tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa kuileta bajeti hii, lakini tujipongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kuipitisha kwa sababu tukishapita (na tunakwenda kuvuka Waheshimiwa Wabunge wengi humu) tunakwenda kuisimamia sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ni matarajio yetu kwamba bajeti hii ambayo ni ya wananchi itakuwa mkombozi mkubwa sana kwa maendeleo ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *SGR* ambao unaendelea sasa na mafanikio yake na bado upo katika hatua ya awali kabisa, nina matumaini makubwa kwamba utakapokamilika mradi huu ambao pia kuna ujenzi wa kutoka Tabora kwenda Kaliua mpaka Mtwara – Mbamba Bay; nchi yetu itakuwa imeungana katika *network* ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi nimepata taarifa kwamba Mheshimiwa Rais ameshaleta mabehewa 89 ya abiria; hata makofi hatupigi kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mabehewa mengine 1,430 ya mizigo pia yanakwenda kutua Tanzania; ni jambo la kheri sana. Nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri na wote walioshiriki katika ujenzi na matayarisho ya mradi huu kwa kazi kubwa waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ujenzi wa *SGR,* lakini ninafahamu kwamba uwepo wa umeme wa uhakika ni matarajio makubwa kwamba *SGR* itafanya kazi kwa ufanisi zaidi. Mpaka sasa kwa nchi ambazo zimejenga mtandao mrefu wa *SGR* ya aina yetu kwa sasa kwa nchi za Afrika Mashariki ni Tanzania peke yake. Ni jambo la kujipongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzetu wa Kenya wana umbali wa kilometa 780 tu ambao ndiyo walikuwa wametangulia kabla yetu. Kwa hiyo, tujipongeze sana Watanzania kwani tumevunja rekodi na Mama Samia amevunja rekodi kwa kujenga mtandao mrefu wa reli ya *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la umeme; umeme ni usalama. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa Mradi mkubwa wa Bwawa la Mwalimu Nyerere. Mradi huu wengi wameeleza (mimi ninarejelea kidogo tu) umetuzalishia umeme wa *megawatt* 2,115. Pia, umeme huu unachangia kwa kiwango kikubwa sana kukuza uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya uwepo wa umeme huu tulikuwa na takribani *megawatt* 2,000 na Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati (Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko) alileta taarifa yake humu. Ninampongeza sana pia Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na usimamizi mzuri wa mradi huu. Mradi huu sasa umekamilika, lakini yapo mambo ya kujipongeza kama Watanzania kwa kukamilisha mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza; tumeujenga mradi huu kwa kutumia rasilimali yetu wenyewe (rasilimali ya maji yetu wenyewe). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kutumia fedha zetu wenyewe, la tatu ni kutumia watalaam wetu wenyewe na la nne ni tunakwenda kuusafirisha sisi wenyewe, kuutumia sisi wenyewe na kuutumia, kama ulinzi na usalama sisi, wenyewe. Hapa ninaweza kusema, CCM oye! Ila kwa sababu ni mchana niache tu, ni kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Mwalimu Nyerere ambao ni *megawatt* 2,115 unatufanya Watanzania leo kuongoza kwa kuwa na umeme mwingi kuliko nchi zote za Afrika Mashariki. Kabla ya umeme huu Kenya walikuwa wanaongoza kwa kuwa na *megawatt* 2,722 leo hii sisi tuna umeme wa *megawatt* 4,031. Wenzetu Uganda walikuwa na *megawatt* 1,722 tumewapita, Rwanda wana *megawatt* 230, Burundi wana *megawatt* 89, hata makofi hatupigiani ndugu zangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo ukweli kazi kubwa imefanyika. Sasa maana yake nini? Kwa taarifa ya juzi ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati ni kwamba, mahitaji yetu ya umeme kwa sasa hivi ni takribani *megawatt* 2000. Sasa swali la kujiuliza ni hizo *megawatt* 2,030 zilizobaki tunazitumiaje? Maana yake ni zinakwenda kuingiza pesa za kigeni, tunaweza tukawauzia majirani zetu bila sisi kutetereka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zambia wana upungufu wa *megawatt* 82 tutawauzia, Malawi wana upungufu wa *megawatt* 89 tutawauzia, Rwanda wana upungufu wa *megawatt* 42 tutawauzia, Kenya wana upungufu wa *megawatt* 1,700 tutawauzia. Naomba tujipigie makofi Wabunge kwa kazi kubwa tuliyoifanya na hii bajeti kwa sababu ni yetu ni matarajio yetu kwamba, mafanikio yote yaliyoletwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na nguvu za Wabunge ni *reflection* ya kuunga mkono kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na uwepo wa umeme huu, lakini kazi kubwa aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kama ifuatavyo: Moja, amejenga miundombinu ya kusafirisha huo umeme mkubwa wa *kilovolt* 400. Ninaomba tuelewane Watanzania, *kilovolt* 400 maana yake ni umeme mkubwa sana wa viwanda na umeshasafirishwa kutoka Bwawa la Mwalimu Nyerere, kilomita 160, kwenda Chalinze. Umeanza kusafirishwa kutoka Chalinze kuja Morogoro na Dodoma na unatoka Iringa kwenda Mbeya, Tunduma na Sumbawanga, kilomita 620. Hata makofi hatuwezi kupiga ndugu zangu? *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma M. Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. DKT. MEDARD M. KALEMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, Mheshimiwa Rais kafanya kazi kubwa na umeme huo huo unasafiri kutoka Mpanda mpaka Kigoma. Sasa hivi wamejenga kutoka Kigoma mpaka Nyakanazi, kilomita 280, *kilovolt* 400, umeme mkubwa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amevunja rekodi, ninaomba tumpigie makofi amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu tumejenga umbali wa kilomita 414 kutoka Singida kupita Remguru kwenda Namanga mpaka Kenya na umekamilika. Waheshimiwa Wabunge suala la umeme nimesema ni usalama, kazi ambazo zimefanyika kuhakikisha kwamba, nchi yetu inabaki salama pamoja na kuusambaza kuwapalekea wananchi pia, ni kichocheo cha kuhakikisha kwamba, nchi yetu inabaki salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huu, ninashukuru sana kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri nimeona kwamba, 67.4% ni wa maji. Ameeleza Mheshimiwa Kakunda sasa hivi kwamba, tulichelewa kidogo, lakini kuchelewa kulikuwa na manufaa kwa sababu, umekuja wakati tunaouhitaji. Ukiwa na umeme wa maji maana yake ni una umeme unaotabirika, wa uhakika, ambao pia ni wa kutosheleza na wa gharama nafuu kwa hiyo, Watanzania wanakwenda kunufaika na uwepo wa umeme huu kwa kuwa na gharama nafuu, hasa utakapokamilika kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo kwa umeme wa maji maana yake ni kwanza gharama za kuujenga wenyewe kwa *unit* moja ni shilingi 36 tu. Kwa hiyo, sehemu kubwa inakwenda kwa wananchi. Ninatoa shukrani sana kwa Mheshimiwa Rais kwa kuwa na uhakika wa umeme wa kutosha, unaotabirika, wa gharama nafuu. Maana yake nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Mheshimiwa Rais, ukimtazama usoni ni kwamba, umeme huu utakwenda kijiji kwa kijiji, kitongoji kwa kitongoji, kaya kwa kaya na nyumba kwa nyumba na hayo ndiyo matarajio makubwa ya Watanzania. Ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Waziri

wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu kwa kukamilisha mradi huu, tuliusubiri kwa hamu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kwa sababu, niliwahi kusimama hapo kidogo, umeme huu ni muhimu sana kwa Watanzania. Ninawaomba tumuunge mkono Mheshimiwa Rais katika jitihada zake za kuhakikisha wananchi wanapata umeme nchi nzima na hasa kuhakikisha kwamba, miundombinu iliyojengwa inalindwa na kuimarishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kupeleka umeme vijijini. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, amevunja rekodi kuwa Rais wa kwanza kwa Afrika Mashariki na inawezekana hata kwa dunia nzima, kwa kupeleka umeme katika vijiji vyote ndani ya muda mfupi. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi inayofanyika sasa hivi ni usambazaji tu, kazi ambayo inaweza ikawa endelevu kufanywa na Shirika letu la *TANESCO*. Kwa hiyo, nasema tu kwamba, bajeti hii ya shilingi trilioni 57, ambayo ni ya wananchi, inaelekezwa kwa wananchi wa kawaida. Inakwenda kuonesha umuhimu wake kwa sababu, inakwenda kujibu kero za Watanzania wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sasa niombe kidogo, katika bajeti hii, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mwigulu Nchemba kwa kutoa fedha. Katika Mawaziri waliotoa fedha kwa wakati kwa miradi mikubwa na amevunja rekodi. Ninamfahamu, watu wanaweza wakazungumza mengine, lakini kwenye kutoa fedha kaka yangu amevunja rekodi, hongera sana. Sasa namwomba akatoe hela za ujenzi wa barabara ya kilomita 51 kutoka Nyamirembe huko Chato na Wanachato wanamsikia hapa Mheshimiwa Mwigulu, kilomita 51.01 kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa hela shilingi bilioni 129 na ametoa shilingi bilioni tano ujenzi wa kilomita moja umeanza. Sasa toa hela ujenzi wa Barabara, kilomita 51.01 ya kutoka Nyamirembe – Kazunguti – Karerwezo – Nyamirembe kwenda Nyambiti mpaka Iryamchele, ipite mpaka huko na izunguke iende Nyambogo ili wananchi wa maeneo hayo waweze kufaidika na lami kwa haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana, Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, wajiandae.

Mheshimiwa Hamisi Kigwangalla hayupo, tuendelee na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti kuu kwa mara nyingine tena. Kipekee kabisa ninachukua nafasi kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mwigulu Nchemba, Profesa Kitila, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Chande pamoja na Mheshimiwa Nyongo, Katibu Mkuu, pamoja na wote walioshiriki katika maandalizi haya mazuri, ambayo yametufikisha kupata bajeti nzuri sana ya kihistoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua pia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya bajeti zilizopita na bajeti hii kwa sababu, zote kwa 100% zimekwenda kujibu yale yote ambayo tuliyaleta, kama vipaumbele vya Wanamoshi, ambavyo tulipitanavyo kwenye kampeni. Vyote vimepata hela na viko kwenye *stage* mbalimbali za utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninagusia maeneo kadhaa; tunayo Barabara ya *TACTIC* kwenye mradi wa *TACTIC, Tier II.* Walitoa tenda ikaenda kwenye *awarding,* lakini ikashindikana kwa sababu, bado ilikuwa inaonekana iko juu, sasa wametangaza tena awamu ya pili. Ninawaomba Wizara waweze kuingilia kuona uhalisia ili kazi hii iende ikaanze mapema kwa sababu, inasubiriwa sana na Wanamoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni ya muhimu sana. Ni ya kufungua kata za pembezoni kuanzia Kata ile ya Ng'ambo kuja ya Msalanga, kuja ya Mji Mpya, Miembeni, Njoro, Kaloleni, Shirimatunda mpaka Karanga, ni barabara ya muhimu sana.

Ninaomba basi watusaidie. Imetangazwa tenda kwa siku nyingine 14 na itakwisha karibuni, watusaidie kulisimamia ili sasa tuweze kupata wakandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Barabara ya Moshi – Arusha inajengwa pale. *TANROADS* wako kwenye hatua za mwisho za kupata mkandarasi, lakini kuna mkanganyiko ambao ninaomba sasa watusaidie kuharakisha kuupatia majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nime-*engage* mara kadhaa wenzetu wa *TARURA* na *TANROADS,* lakini bado hawajaweza kuja na *concept* ya mara moja. Barabara hii kwenye *round about* ya *YMCA, double road* hii ya Moshi – Arusha inakwenda kukutana na *double road* nyingine mbili; kuna inayotoka *keep left* ya *NBC* kuja *keep left* ya *YMCA* na *double road* nyingine, ambayo Rais ameshakubali kuipatia fedha, ni ya kutoka *YMCA* kwenda *KCMC*. Sasa pale kwenye *keep left* ya *YMCA* patakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Kitila kwa sababu, iko kwenye mpango na bahati nzuri kule ni kwenu, wakati unaelekea Rombo utapita pale, sasa ninadhani kwa uhalisia kabisa, hata Mheshimiwa Nchemba ukiwa unataka kwenda kule Old Moshi lazima upite pale *YMCA,* sasa ninadhani lile eneo linastahili kabisa hata kuwekewa *flyover* kwa sababu, kutakuwa na *double road* nne. Hii ya kutoka mjini, kwa maana ya *NBC* kuja *YMCA,* tayari fedha zipo, sasa wenzetu wa *TARURA* wanapata shida kwamba, wakitengeneza pale *YMCA* waiwekeje? Kwa hiyo, ninaomba sana, waliingilie hili, ili ikiwezekana tuweke *flyover* pale. Ile barabara ni kubwa, ni Barabara ya Afrika Mashariki, inapitisha magari mengi na ni hitaji halisia, siyo *exaggeration*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbushia fedha za Kituo cha Afya Kiboroloni, nimeahidiwa hapa zitatoka kabla ya tarehe 30. Ninaomba sana, ni kituo cha afya cha kimkakati, fedha zake ziweze kwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumshukuru Mheshimiwa Rais, tarehe 25 kesho kutwa atakuja kuzindua kituo cha matibabu ya kansa kwa mionzi, *KCMC*. Kituo kile ni muhimu

sana kwa Kanda ya Kaskazini na kitakwenda kubadilisha kabisa maisha ya watu wa Kanda nzima ya Kaskazini na hasa Moshi Mjini kwa sababu, sasa matibabu ya kansa kwa mionzi yatapatikana *KCMC*, Bugando na *Ocean Roads.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ombi langu la siku zote. Kwenye *salary scale* ya Watumishi wa *KCMC,* hasa hawa madaktari bingwa na watumishi kwa ujumla, iweze kuangaliwa ifanane na hospitali nyingine hizi kubwa za kikanda, ili tuondoe ile haso ya hawa madaktari kuwa wanakimbiakimbia kwenda kujitafutia nyongeza maeneo mengine, hususan Arusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Uwanja wa Ndege wa Moshi. Nimepata uhakika kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, watamlipa mkandarasi muda wowote kuanzia sasa, ili akamilishe kurekebisha uwanja ule. Naomba sasa, tafadhali sana, angalieni suala la fidia kwa zile nyumba kadhaa pale, ili ku-*extend* ile *runway* tumalize hili suala kwa mara moja ile *airport* ziweze kutua zile ndege kubwa, kama *ATR70* na ziweze kuongeza tija kwa uwanja huu pale Moshi Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuishukuru Wizara ya Fedha kwa sababu, kwa kuungana na Wizara ya Michezo, wametuhakikishia Moshi Mjini, pale *Memorial,* watatuletea uwanja mmojawapo wa mazoezi, kwa ajili ya timu zinazokuja kwa michezo ya *AFCON*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa unyenyekevu na wenye shukrani sana ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa tukio ambalo linaenda kufanyika Moshi Mjini kesho. Mheshimiwa Rais amekubali na tayari ametoa fedha shilingi bilioni 12.1, kwa ajili ya kukamilisha Stendi ya Nganga, Mfumuni, ambayo ilisimama kwa muda mrefu sana, hii kwetu ina umuhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi bilioni 12.1 inayoenda kumalizia, ambayo kesho tunategemea pale Halmashauri ya Moshi watie saini na mkandarasi *CRJE,* nimepiga kelele sana hapa, nimeshirikiana na Ofisi ya *AG* kuhakikisha mkataba huu unahuishwa. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ninashukuru

Mawaziri pamoja na Serikali nzima kwa kukubali kutuondolea huu mkwamo wa Stendi ya Nganga, Mfumuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Manyema lilikubalika na Serikali kutengewa shilingi milioni 600, kwa ajili tu ya paa na *floor*. Ninamwomba Waziri atusaidie hela hii, shilingi milioni 600 siyo kitu kwake, itoke kipindi hiki tukaweke paa, kwa ajili ya wafanyabiashara zaidi ya 1,000 ambao wako Soko la Manyema. Ni paa na sakafu tu na hatua zote tumeshapitisha; suala hilo liko kwako Mheshimiwa Mwigulu, ninaomba aamue na atusaidie, apeleke hiyo shilingi milioni 600 tukamilishe hili suala. Sisi Moshi Mjini baada ya hili na hayo mengine yote yaliyopita, ninataka niwahakikishie kura za Chama Cha Mapinduzi, kura za Mheshimiwa Rais, sisi tunasema Oktoba tunatiki, halafu tunatiki tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hiki kitabu cha bajeti yapo maeneo ambayo ninataka nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais. Maeneo makubwa sana ambayo ametufanyia mengi tulishayasema na mimi hapa nitasema kwa kushukuru, lakini na kuongeza hapo nakshi nakshi kidogo ili yakae vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuongeza kipato cha chini cha mshahara kwa watumishi wa umma kutoka shilingi 370,000 mpaka shilingi 500,000. Ninamshukuru sana amewajali watu ambao wanatufanyia kazi, katika hali ya kawaida mara nyingi hawapati namna ya kuweza kuonekana na kupewa maua yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba, kuna mfanyabiashara mmoja Arusha wakati wanaangalia mabadiliko ya kodi alitoa wazo lake na ninafikiri ni zuri sana. Hawa watu wa kima cha chini, kama ikiwezekana, ile kodi ya moja kwa moja ya *PAYEE,* hawa wa laki tano hawa, tuangalie namna ya kuiondoa kule kwao, watalipa kodi kwenye vitu vingine hivi wanavyotumia, waondolewe *PAYEE* hawa wa kima cha chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile wazo la yule mfanyabiashara, *Sapbil wa Hanspoul,* ninadhani ni zuri sana. Mheshimiwa Waziri

aangalie namna ya kufanya, tutapata maeneo mengine ya kufidia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwenye bajeti hii, kwenye ukurasa wa 65, kwa kuongeza kiwango cha chini cha pensheni kwa 149.8% kutoka shilingi 100,000 mpaka shilingi 250,000. Hawa watu waliostaafu nao waliipigania nchi hii, kama hawa walioko kazini sasa, Mheshimiwa Rais amewaona na amefanya jambo jema sana. Ninaomba kanyongeza kadogo na hawako wengi sana hawa kwa sababu, *life expectancy* ya Tanzania mpaka sasa ni miaka 68. Hebu tuangalie namna ya kuondoa makato yote hata kwa kuongea na benki, hata yale makato ya *withdraw* yaondolewe kwa wastaafu, kama wanavyofanya wenzetu kwenye nchi zilizoendelea, mpaka maeneo ya *parking* wanaweka ya *special.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie pia namna ya kuongeza hii pensheni mpaka ifike sawa na mtu, ambaye anastaafu sasa. Yaani mtu anayestaafu sasa awe sawa na mtu wa kada yake aliyestaafu miaka mingine, ili waweze kujikimu. Ninadhani tunaweza tukafikia huko kwa jinsi ambavyo uchumi wetu unaendelea kupanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwenye ukurasa wa 90, wamefuta kabisa ile kodi kwa bodaboda na bajaji, wale ambao wanafanya kazi ya kusafirisha abiria. Wameifuta kabisa ile shilingi 65,000 ya bodaboda na ile shilingi 120,000. Sasa ninaendelea hapohapo, nilileta kilio chao kwenye leseni; kwenye leseni kilio chao kikubwa siyo ile gharama ya kulipia leseni, ni gharama ya ule mlolongo wa shule, kama kule *VETA* shilingi 340,000 na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, kama inawezekana, *VETA;* sasa hivi Moshi Mjini, wiki hii wanawachukua wale bodaboda na bajaji ambao hawana leseni wanawapa shule pale kwa shilingi 35,000, wanawapa vyeti wakachukue leseni. Hebu tuangalie namna ya kufanya hivyo kwa sababu, shilingi 340,000 ni kubwa sana kwao, wengi hawana leseni na wanaendelea kupata shida pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaungana na wazo la Mheshimiwa Festo Sanga la bima ya afya kwa wote ipitishwe hapahapa kwenye leseni kwa wale watu wa bodaboda, lakini ikionekana huo ni mzigo sana tuangalie namna ya kucharge *WCF* kwa sababu, mara nyingi wanapata ajali wakiwa kwenye pikipiki zao na ile ni wamepata ajali wakiwa kazini. Tuangalie *WCF* namna ambavyo wanaweza wakawa sehemu ya kuwatibu wakati wanapopata matatizo. Ninaomba sana hilo tuliangalie kwa karibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 91, kuna ile kodi ya 10% *(Withholding Tax)* kwa *profit* ambayo haijagawanywa. Imeongelewa na watu wengi, wapo waliotoa mawazo tofauti, kama Mheshimiwa Lugangira kwamba, waangalie namna ya kuifanya ili isionekane kwamba, ni mwanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwa roho nyeupe kabisa, hii inaonekana kama ni *double taxation,* hebu tuangalie kwanza. Mheshimiwa Lugangira amesema angalau huo mwaka mmoja uongezwe, lakini mimi ninasema pamoja na huo mwaka mmoja, lakini baadhi ya zile taasisi ndogo kwa sababu, wanavyo-*retain* hii *profit* ni, kwa ajili ya kukua. Sasa unaweza kukuta anatafuta hela ya kujazia ili wa *reinvest*. Waangalie namna ya kuzisaidia hizi taasisi ndogo, hii kodi kwa kweli, isiende kuwaumiza na ikiwezekana ifutwe kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kilio ambacho tulikileta mara nyingi hasa kwa sisi ambao tunatoka maeneo haya yenye utalii. Ukurasa wa 21 ameangazia ile Sheria ya Wanyamapori Namba 282(9). Kwenye ukurasa wa 124 amekwenda kwenye sheria ile ya eneo la uhifadhi la Ngorongoro Namba 284(12)(B) katika kuhakikisha kwamba kuna ile *retention* kwa ajili ya kuhakikisha sasa wanaweza kurekebisha barabara, kuwekeza kwenye maeneo ya maendeleo, kuwekeza kwenye sehemu ambazo zinahitaji uwekezaji wa haraka na baadaye kuboresha utalii wetu na baadaye nchi yetu kusonga mbele kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya mchango huu nikushukuru sana na wewe mwenyewe na nikutakie kila la heri

unaporudi maeneo yako hayo wakakuchague urudi tena, Mheshimiwa Spika arudi na Mheshimiwa Naibu Spika naye arudi; na Wabunge wote niwatakie kila la heri maeneo yao Mungu atubariki sote, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu kazi iliyobaki ni ya muda mchache ninaongeza muda hadi tumalize; na sasa ninawatangaza wageni ambao wapo muda huu.

Tuna wageni 25 wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, ambayo ni Timu ya Kuombea Uchaguzi kutoka Mikoa mbalimbali Nchini Tanzania, wakiongozwa na Mkurugenzi Ndugu Tumaini Wakawaka. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, atafuatia Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga na Mheshimiwa Jaqueline Ngonyani Msongozi ajiandae.

**MHE. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili kuchangia kwenye hoja hii iliyokuwa mezani. Kabla ya kuendelea moja kwa moja nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya na kuweza leo kusimama tena kwenye Bunge hili Tukufu kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru wananchi wa jimbo langu la Korogwe Mjini kwa kuwa na imani na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuwa Mbunge na kuwawakilisha kwa hiki kipindi cha miaka mitano. Ninafahamu kazi tulizozifanya kwa pamoja na kushirikiana na wao pamoja na *support* kubwa ambayo imetolewa na Serikali yetu ya Awamu ya Sitta ya mama Samia Suluhu Hassan. Kimsingi bado wana matumaini na wana imani kubwa na mimi na ninaamini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwenye Bunge ambalo litaanza tena mwezi Novemba, nitakuwa miongoni mwa Wabunge hao kwa kuwa kazi kubwa tumeifanya. Wana imani kubwa sana na mimi na pia wana imani kubwa sana na Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kifupi nitaeleza mambo ambayo wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini wanasema; kwamba Oktoba watakwenda kupiga tiki kwa mama Samia Suluhu Hassa. Hizi ni sababu ambazo wanazo; kwa hiyo nitaongea hayo mambo kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo ninapenda kushauri mambo machache. Kwanza niwapongeze viongozi wa Wizara hizi mbili ambazo leo tunachangia, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Profesa pamoja na wasaidizi wao kwa kazi kubwa ambazo wanaendelea kuzifanya kulisaidia Taifa hili. Sehemu ambazo ninataka nishauri moja ni kwenye sekta ya afya. Kwanza, tunaishukuru Serikali yetu kwa namna ambavyo wameboresha sekta ya afya kwa kujenga miundombinu kwenye hospitali za wilaya, za rufaa, vituo vya afya pamoja na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo ninashauri mambo machache. Cha kwanza nipongeze kwa hatua kubwa hasa ya kuongeza wataalam. Ukiona taarifa zetu ni kwamba tulikuwa tuna wataalam wachache, lakini sasa hivi wapo madaktari wabobezi zaidi ya 2,000. Ninatamani tuendelee kuweka mkazo mkubwa kwenye kutafuta wataalam, ku-*sponsor* wananchi wa Tanzania, vijana wetu waende kupata elimu nzuri ya udaktari ili waweze kurudi kuwahudumia watu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo tuna makundi maalumu. Ninataka nizungumzie akinamama wajawazito pamoja na wazee. Kimsingi tunazo *facilities* nzuri lakini bado hawa watu wa makundi maalum wana changamoto kubwa katika kupatiwa huduma. Tunaomba Serikali itumie namna ambayo inaona ni sahihi. Kama *policy* yetu inavyosema, kwamba watahudumiwa bure basi iwe bure kweli kweli. Sasa hivi mama mjamzito akienda hospitali anaambiwa achangie vitu kadha wa kadha kwa kuwa hospitali wakati huo hivyo vitu havipo. Kwa hali ngumu ya wananchi wetu huwa wanapata changamoto kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba Serikali ijipange kuhakikisha kwamba, kama tulivyosema kwamba matibabu ya wazee na akinamama wajawazito ni bure basi ikawe bure kweli kweli. Ninaamini kuwa Serikali ya mama Samia

Suluhu Hassan haina jambo inashindwa, ninajua itakwenda kufanyia kazi kwenye sekta hii ili kweli akinamama wajawazito na wazee wapatiwe matibabu bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninataka kushauri ni sekta ya elimu. Vilevile tunaipongeza na kuishukuru Serikali kwa namna kubwa ilivyowekeza kwenye miundombinu ya elimu. Kwenye shule zetu imejenga madarasa, maabara na miundombinu mingi na hasa kwenye hiki kipindi cha Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikwisha kuchangia hapo awali. Sikumbuki ni mwaka gani, lakini nilikwisha kuchangia na leo ninataka nikumbushe tena. Ninatamani siku moja elimu ya nchi hii isiwe ya ubaguzi. Kwa maoni yangu na nilikwishaambiwa mara nyingi na wataalam, wanasema hata siku moja tusidharau umuhimu wa Kiingereza kwenye elimu yetu. Elimu yetu hasa ya msingi, kuna shule za *private* ambazo zinafundisha kwa mtaala wa Kiingereza, lakini pia kuna shule za Serikali ambazo zinafundisha kwa mtaala wa Kiswahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kabisa kwamba watoto kutoka familia maskini ndio wanaokwenda kwenye hizi shule ambazo zinatumia mitaala ya Kiswahili; lakini watoto ambao wazazi wao wana kipato kikubwa wanakwenda kwenye hizi shule za Kingereza. Ombi langu na ushauri wangu, siku moja kwenye nchi hii mtu asiamue anampeleka mtoto wake kwenye shule ya Kingereza au ya Kiswahili kutokana na uwezo wake wa kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kuwa nchi yetu bado uchumi wake si mkubwa kihivyo, lakini ninatamani Serikali ifanye *investment* ili kuwe na shule za msingi za kutosha ambazo zinafundisha mitaala ya Kingereza ili mwananchi awe ana *option* mwenyewe, *whether* kumpeleka mtoto kwenye shule ya Kingereza au shule ya Kiswahili. Huo ndio ulikuwa mchango wangu kwenye sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona Serikali ilivyopiga hatua kubwa kwenye kukusanya kodi; lakini changamoto kubwa ni wigo wa walipakodi kwenye nchi hii. Nchi hii watu wanaolipa kodi ni

wachache sana. Wengi wameshauri, lakini sehemu moja ambayo baadhi ya watu wameshauri ni kwenye *informal economy.* Kati ya changamoto kubwa kwenye nchi hii ni sekta ambayo haiko rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kukusanya kodi vizuri ni lazima tuhakikishe kuwa tuna-*formalise* biashara nyingi ili kuwe na urahisi wa kukusanya kodi. Sehemu mojawapo ambayo watu wamezungumzia ni kwenye kupunguza *cash economy.* Ni ngumu sana kuweza kukusanya kodi endapo tunatumia *cash economy.* Nchi yetu inaweza kupunguza au kuondoa kabisa *cash economy;* hili linawezekana. Nchi yetu ni kati ya nchi ambazo zinatumia sana teknolojia hasa simu. Ukiona kwenye mitandao watu wana-*smartphone* na wana simu nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, mtu yeyote ambaye anasajili biashara, iwe duka kwa *level* gani, sehemu ya kusajili biashara ni lazima aambiwe anatakiwa kununua *card reader* ambayo inaweza kusoma kadi za kifedha; na wananchi wetu kila mwananchi atengenezewe kadi ambayo inaweza kuhamisha fedha kwenye simu kwenda kwenye hiyo kadi ili akifika dukani badala ya kutumia *cash* anatumia ile kadi ambayo anaweza kuhamisha hela kutoka kwenye simu yake kupeleka kwenye kadi. Kwa hiyo, hizi kadi zinawezekana zikatolewa bure kwa wananchi wote. Inawekana. Kama tulivyoweza kutoa *NIDA,* na kitambulisho cha mpigakura. Hatushindwi kutengeneza kadi ambayo inaweza kusomwa na *card reader* ambazo ziko kwenye maduka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kila mwananchi anakuwa na hiyo kadi ambayo mtu anaweza ku-*transfer* hela kutoka Mpesa, Tigo, *whatever* kwenda kwenye hiyo kadi; na kila mfanyabiashara anayefanya biashara yoyote alazimishwe kuwa na hiyo *card reader* ili mwananchi akifika aweze kutumia hiyo kadi kufanya *transaction.* Hii itapunguza kwa kiasi kikubwa *cash economy* na itasaidia watu kuweza kulipa kodi kwa ajili kwa kuwa *TRA* wanaweza ku-*track movement* za *transaction* za kila mwananchi na kila mfanyabiashara. Hizo ni sehemu ambazo nilitaka kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nilitaka kuongelea mambo machache. Kama nilivyoongea hapo awali, matumaini makubwa ya Watanzania, hasa waliyonayo watu wa Korogwe kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; wanasema kwa kupitia mambo hayo Oktoba, 2025 wanakwenda kumpigia kura Rais wao; lakini wanasema watampitisha Rais na watampitisha Mbunge wao kwa haya mambo ambayo Mama Samia amekwenda kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru Mama Samia kwenye Jimbo letu la Korogwe Mjini. Wakati ninaingia kwenye nafasi hii ya Ubunge mwaka 2020 nilikuta tuna kituo kimoja tu cha afya. Sasa hivi tunaongea tunamaliza miaka yetu mitano Mama Samia amekwisha kutujengea vituo vipya viwili vya afya. Haya ni mapinduzi makubwa kwenye jimbo ambalo lina nusu tarafa siyo tarafa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Korogwe Mjini lina nusu tarafa lakini kwenye hiyo nusu tarafa tuna vituo vya afya vitatu; na sasa hivi tumepatiwa fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha afya cha nne. Hayo ni mapinduzi makubwa kwenye sekta ya afya na wananchi wa Korogwe Mjini wanamwambia mama Samia Suluhu Hassan mwaka huu wako na yeye wanakwenda kumlipa kwenye kutiki Oktoba mwaa huu. Isitoshe, kwenye sekta ya afya ametujengea *emergency medical department* mpya kabisa, na sasa hivi wananchi wanaitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya sehemu ambayo ilikuwa ni changamoto kubwa kwenye mji wetu ni sekta ya maji. Mama Samia kwa kipindi cha miaka minne mimi nikiwa Mbunge ametuletea miradi mingi ya maji kwenye Jimbo la Korogwe Mjini. Sasa hivi ninajua changamoto haijakwisha kabisa, lakini imepungua kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ambayo ina takribani zaidi ya shilingi bilioni 30 za Kitanzania imejengwa kwenye mji wetu; na sasa kuna mradi mkubwa wa miji 28 ambao uko zaidi ya 50% na kabla ya Oktoba mwaka huu unaenda kukamilika na huo ndio unaenda kuwa suluhisho. Changamoto ya maji itakuwa historia kabisa kwenye Mji wa Korogwe. Hayo ni mapinduzi makubwa

ambayo Mama Samia ameyafanya na wanasema Oktoba wanaenda kutiki kumrudisha kuwa Rais wa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hilo, kwenye sekta ya barabara mji wetu ulikuwa una changamoto nyingi sana za barabara hasa katikati ya mji. Tumejengewa vipande vingi vya Barabara, zaidi ya vitano katikati ya mji wetu pale. Sasa hivi tuna Mradi wa *TACTIC,* hivi punde unakwenda kuanza kutengenezwa. Utajenga barabara yetu ya katikati ya mji kutoka Benki ya *NMB* mpaka kwenye Hospitali yetu ya Magunga. Tutakwenda kutoa barabara hiyo kutoka kwenye Kata ya Bagamoyo kwenda kwenye Kata ya Mgombezi. Kwa hayo watu wa Korogwe Mjini wamejiandaa kwenda kumpigia Mama Samia kura za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hivyo barabara zetu usiku ulikuwa huwezi kutembea, kuna giza; lakini tumeletewa taa za barabarani. Mtu wakati wowote unaweza kupita. Mji umependeza, mji umenoga. Hayo ni matunda makubwa na kazi kubwa ya Serikali yetu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mama Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa sekta ya elimu, wakati ninaingia madarakani nilikuta sekondari tisa kwenye mji wetu, lakini hivi tunavyoongea tumekwishajenga sekondari mpya tatu. Haijawahi kutokea kwa kipindi kimoja kwa Mbunge mmoja na kwa Serikali miaka mitano pekee kujenga sekondari nyingi kama hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wanasema watakwenda na Mbunge wao, hawabadilishi na vilevile watakwenda na Rais wao Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa hasa kwenye sekta ya elimu. Nimekwisha kuwaambia, kwamba endapo nikirudi tena mwakani, kuna kata moja tu sasa hivi haina sekondari, lakini kwa ajili iko katikati ya mji na imebanwa sana, nikirudi Oktoba nitamwomba Mama Samia na tutajenga sekondari kwenye Kata ya Masuguru, sekondari ya ghorofa. Ndiyo kata pekee ambayo haina sekondari na tutakwenda kuwawekea sekondari ya ghorofa pale kwenye Kata ya Masuguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesha kuongea na Mheshimiwa Waziri amesema, wewe pambana tu urudi; na wananchi watanirudisha. Tukirudi tu tunakwenda kujenga sekondari ya ghorofa kwenye Kata ya Masuguru na inawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hivyo Mama Samia amejenga shule za msingi tatu kwenye mji wetu. Hiki kitu siyo kidogo. Shule za msingi tatu mpya kabisa zimejengwa na wanafunzi hawasumbuki siku hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya kilimo, tulikuwa na changamoto kubwa sana ya wakulima wetu hasa wa mpunga; wanalima kwenye mabonde. Wakikaribia kuvuna maji yanakuja yanazoa mashamba. Tunaishukuru Serikali imetuletea shilingi bilioni moja na milioni mia nane kwenye Bonde la Mahenge na sasa hivi tunakwenda kuletewa shilingi bilioni tisa kwenye Bonde la kwa Msisi. Hayo ni mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kilimo na wananchi wa Korogwe wanasema wanakwenda kumpigia Mama Samia kura za kishindo Oktoba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha hivyo tuna barabara yetu kubwa ambayo inaunganisha Jimbo la Korogwe Mjini, Korogwe Vijijini na Jimbo la Kaka yangu Dunstan Kitandula kule. Barabara ile tuliiomba siku nyingi; barabara inayotoka *Old* Korogwe, Kwa Mndolwa, Magoma, Mashewa hadi Mabokweni. Serikali imeshatoa fedha upembuzi yakinifu umeshafanyika na mwaka huu wa fedha unaokuja kwenye bajeti hii hapa tumetengewa fedha tunakwenda kujengewa barabara ya lami ambayo inaenda kuunganisha majimbo yetu hayo matatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini pamoja na majimbo ya Korogwe Vijijini na Mkinga kule wanasema wanakwenda kumchagua Mama Samia Suluhu Hassan kwa sababu hiyo ni barabara yao ambayo walikuwa wanaitarajia na wanaitamani siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi letu pia kuhusu *SGR;* tunamshukuru Mama Samia, hii miradi ambayo Rais Magufuli aliiacha ameifanyia kazi; mfano *SGR*. Mimi ni mdau mkubwa ambaye ninatumia sana *SGR*. Wananchi wa Kanda ya Kaskazini

kule Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro nao tunatamani kuwa na *SGR*. Kwa hiyo, tunamwomba Mama Samia, vile anavyopambana na *SGR* kule kwa kuwa tuna reli tayari, basi atufikirie ili na sisi tuwe na *SGR* ambayo itakuwa inatoka Dar es Salaam, Tanga Mjini, Korogwe, Moshi na Kilimanjaro. Kwanza kule kuna abiria wengi na vilevile kule kuna mizigo mingi ya kutosha. Kwa hiyo, tunamwomba mama yetu kwenye hiki kipindi cha miaka mitano inayokuja basi atujengee *SGR* katika Kanda yetu ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana. Ninajua umenivumilia sana; nimeongea sana, lakini kama Naibu Spika alivyosema, hiki ndicho kipindi cha mavuno. Tunaongea yale mambo makubwa ambayo Serikali yetu imeyafanya. Mama Samia amefanya mambo makubwa sana. Nikitaka kuendelea kuongea hapa nitatumia nusu saa nyingine, lakini niishie hapa. *Commitment* yangu mimi kama Mbunge wa Jimbo la Korogwe Mjini na wananchi wangu wa Korogwe Mjini tunamwambia Mama Samia a-*relax* asiache kukosa usingizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wanasema sijui *no reforms, no election;* sisi tunasema Oktoba tunaenda kutiki kura nyingi za kishindo kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili tunayo sababu ya kufanya hivyo; hatuongei tu. ingekuwa Mama Samia Suluhu Hassan, hata kama ni Mwenyekiti wangu wa chama, niko *serious,* angekuwa hajafanya nisingesimama kwa ujasiri kusema tunaenda kumpigia kura, lakini ninasimama kwa ujasiri kwa kuwa amefanya mambo makubwa. Ndiyo maana tunasema Oktoba tunaenda kumlipa kwa yale mambo makubwa ambayo ameyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawashukuru sana, tena sana wananchi wa Korogwe Mjini kwa miaka mitano. Ninawashukuru kwa imani kubwa waliyokuwa nayo, na ninashukuru kwa imani kubwa ambayo wanaendelea kuwa nayo. Kila siku ninasoma *massages* zao, wakisema kuwa, Mheshimiwa Mbunge tuko pamoja na wewe, pambana, nenda kachukue fomu na sisi tutakupitisha kwa mara nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninakushukuru sana Mungu akubariki kwa kunipa nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea. Tunamalizia na Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii kwa mwaka ujao wa fedha. Nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri sana na kubwa sana ambayo ameifanya kwenye Taifa letu. Kule Ludewa ziko ambzo ningeweza kuzitaja. Wakati anakuja kuomba kura alivuka Mto Ruhuhu alikutana na vilio vya wananchi walikuwa wakiliwa sana na mamba kutokana na kuvuka ule mto. Alivyochaguliwa baadaye ameweza kujenga daraja pale la Mto Ruhuhu. Kwa hiyo, kwa hili ninamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kule Mwambao kuna vijiji ambavyo vilikuwa havifikiki kabisa kwa barabara, kwa mfano, Makonde na Lumbila ameweza kututengenezea barabara. Tuliweka maombi maalum, Serikali ilitoa na wananchi kule leo wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais na wanamuahidi kwamba mwezi Oktoba watatiki na kura zitakuwa nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hayo tu lakini vilevile, kipande cha Barabara inayoanzia Njombe kwenda Manda sehemu ile ya Itoni mpaka Lusitu nilivyoingia ilikuwa imejengwa kilometa tisa kwa kiwango cha zege, lakini leo tuna kilometa 50 zimetimia kwa kiwango cha zege na kiasi kikubwa kimejengwa wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ile kwa kweli ni zege ya kiwango cha kimataifa kwa nchi hii ninafikiri sisi ndiyo tumependelewa kule Ludewa labda kidogo wale wa mwendokasi Dar es Salaam wanaweza wakawa wananukianukia kufanana na sisi. Vilevile, barabara hii imetumia kiasi cha shilingi bilioni 179, tungekuwa tunajenga barabara za kawaida zilikuwa

zinatosha kuanza Njombe mpaka Manda kwa kiwango cha lami na sehemu ya kutoka Mkiu – Liganga – Madaba ingeweza kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliungana vilevile na Mbunge mwenzangu jirani Mheshimiwa Deo Mwanyika, Serikali ikatafuta mkandarasi kuanzia pale Lusitu mpaka Njombe na kiasi cha shilingi bilioni 114. Kwa hiyo ni mradi mkubwa sana, ehee natambua kwamba hapa katikati kuna changamoto ilitokea ila nishukuru Serikali imeweza kumlipa mkandarasi kiasi cha shilingi bilioni 4.7 ila tu huyu mkandarasi ameomba sana kwa kuwa mradi huu ni mkubwa wa bilioni 114 angeongezewa kidogo fedha ninashukuru kuona Mheshimiwa Mwigulu anaandika pale, angeongezewa fedha ili aweze kurudi kazini kwa kasi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Ulega aliweza kutafuta fedha nyingine kwa ajili ya kuiboresha ile barabara iweze kupitika vizuri. Ilikua ni kero kubwa sana kwa wananchi hasa wanaotegemea Hospitali ya Ikonda, wasafirishaji walitaka kuweka mgomo. Mimi na Mheshimiwa Mwanyika tuliweza kuwatuliza wakaendelea. Kwa hiyo kitendo cha kuiranda vizuri kumeleta matumaini makubwa, lakini wananchi watafurahi zaidi wakiona mkandarasi ameongezewa malipo ili aweze kurejea kazini na kuiboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi barabara za kwenda Ludewa hasa maeneo ya Liganga na Mchuchuma ni barabara ambazo zimeshika uchumi mkubwa sana wa nchi hii. Nilikuwa ninaangalia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo nimeona ametenga fedha kwa ajili ya pale kwenye makaa ya mawe Mradi wa Umeme *megawatt* 600 pale Mchuchuma, nimeona pale Mheshimiwa Profesa Kitila, ninashukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ule Mgodi wa Liganga, nimeona pale kwenye bajeti. Kwa hiyo, ni ishara kwamba miradi hii sasa inakwenda kuanza, nilikuwa ninaangalia takwimu mwaka 2022 Serikali ilitumia Dola za Kimarekani milioni 753 kuagiza chuma nje ya nchi na mwaka 2023 ilitumia Dola za Kimarekani 775.11 kuagiza chuma. Kwa hiyo, fedha nyingi ambayo ingeweza

kufanya mambo makubwa sana hapa nchini ilikwenda Afrika Kusini kununua chuma ambacho kimetumika kujenga reli, Bwawa la Mwalimu Nyerere na mahitaji mbalimbali ya chuma. Vilevile, nchi kama China nayo imenufaika sana na mapato haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, bado tunaiona dhamira ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ya miradi hii kuanza, ndiyo maana ninasema hapa nimepitia bajeti nimeona fedha zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo tunaendelea kumshukuru sana ni kulipa fidia wale wananchi wa Liganga na wa Mchuchuma. Kwa sababu kule miradi, mradi mmoja uko *termed* kama Mradi wa Kitaifa ambao unaitwa Maganga Matitu na Ketewaka ndiyo hili sasa watu wa *NDC* wanakwenda wiki ijayo kwenda kulipa fidia. Kwa hiyo, ninawashukuru sana watu wa *NDC* kwa jitihada na ninatambua saa hizi wamekwenda kumkagua huyo mwekezaji mkubwa Mheshimiwa Jafo sijamwona hapa nilivyomtafuta, nimeambiwa yuko China kwa mwekezaji yule wa Liganga na Mchuchuma. Kwa hiyo nimpongeze sana na yeye kwa kumsaidia vizuri sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina taarifa kwamba huyo Shudao ambaye sasa ndiye anachukua ile Liganga kubwa ana mtaji mkubwa sana. Mtaji wake unafika trilioni 99 nimeambiwa kwa hiyo ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana. Kwa hiyo, niombe sana Serikali iharakishe maamuzi baada ya fidia zile kulipwa twende sasa viwanja vikajengwe kule Ludewa na ile sasa itafungua sana uchumi wa Nyanda za Juu Kusini na uchumi wa nchi yetu. Watanzania wengi sana watakwenda kupata ajira kwenye ile miradi kwa hiyo ni miradi muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ndiyo huu Ketewaka ambao tayari *MMI Steel* wameshajadiliana na Serikali ndiyo wanakwenda kulipa fidia nao wataanza. Kwa hiyo, hii miradi inahitaji barabara zile ziweze kuboreshwa vizuri kama ambavyo nimeeleza kwa sababu itachangia kwa kiwango kikubwa sana kuongeza pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wilaya hii sasa inakwenda kuwa ya uwekezaji mkubwa naomba sana Tume ya Mipango iweze kuangalia zile barabara za kimkakati na madaraja ili wananchi waweze kulima kwa wingi zaidi, kuzalisha chakula cha kuweza kulisha wageni wote ambao watakwenda kuhamia kufuata uwekezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara vilevile iweze kupita kutoa elimu kwa wananchi juu ya fursa ambazo zitakuwepo kutokana na miradi hii, namna ya kukabiliana na athari za kimazingira, namna ya kutunza ardhi yao na katika hili nimpongeze sana Mheshimiwa Ndejembi, Waziri wa Ardhi. Wizara ya Ardhi kule imepeleka fedha nyingi sana na maeneo mengi tayari yameshaanza kupimwa. Kijiji cha Amani na Mavanga tayari viwanja zaidi ya 10,000 vimeshapimwa, maeneo yamepangwa kimji bado tu kufungua barabara. Kwa hiyo, miradi itakavyokwenda itakuta mambo yameshakaa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu Wizara ya Ardhi iliweza kutoa shilingi milioni 100 kwa ajili ya kupima miji mingine kama Mji wa Lugarawa kwa ajili ya maandalizi ya ugeni huu mkubwa mbao utakuwepo kule Ludewa kwetu. Vilevile, Makao Makuu ya Wilaya napo yamepangwa na kupimwa vizuri na kupitia Mradi wa *World Bank,* Serikali ilitoa fedha kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji karibu vyote vya Ludewa. Sasa hatua itakayofuata ni kuwapimia wananchi na kuwapa hati za haki miliki za kimila ili wananchi wale waweze kuwa na usalama kwenye milki zao, lakini vilevile waweze kutumia kama nyenzo za kujiongezea vipato kwenye taasisi za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesoma ukurasa wa 39 wa Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba nimeona amezungumza pale kwamba Serikali inaendelea na maandalizi ya kutekeleza Mradi wa Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa kimiminika kwa maana ya *LNG* na kutekeleza shughuli za utafiti wa mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2022/2023 Tanzania iliagiza mafuta kwa ajili ya magari na mitambo mingine yenye thamani ya Dola za Kimarekani 3.19 bilioni na mwaka wa

fedha 2023/2024 Tanzania iliagiza kutoka nje lita bilioni 4.3 za *petrol*. Sasa na hizi nimesoma kwenye Gazeti la *Daily News* la tarehe 28 Aprili, 2025. Kwa hiyo hoja yangu hapa ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba hili alililoliandika Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye ukurasa wa 39 wa Hotuba yake ni jambo kubwa na muhimu sana, kwa sababu ile gesi kama itaendelea kusindikwa inamaana itatumika majumbani. Bei ya kuongeza gesi kwenye mitungi kwa ajili ya matumizi ya majumbani itashuka. Kwa hiyo sasa hivi tumegawa sana mitungi hata Ludewa kule wamepata, lakini ile gharama ya kwenda kujaza gesi bado wananchi hawana uwezo. Kwa hiyo, jambo hili linaleta madhara makubwa sana kwenye mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Tanzania inakadiriwa kuwa na gesi ya asilia ipatayo trilioni 57 *cubic feet*. Kwa hiyo, tuna gesi kwa kiwango kikubwa sana ambayo inaweza ikatumika kuokoa mazingira yetu ambayo ukataji wa miti umekithiri. Ukiangali takwimu za uharibifu wa mazingira nilikuwa ninaisoma, inaonekana ukataji wa miti hekta milioni 3.5 kuanzia mwaka 2001 hadi 2023 kwa mujibu wa *Global Forest Watch* ziliweza kuteketea kutokana na ukataji wa kuni na mkaa kwa ajili ya matumizi ya majumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa hii maliasili ambayo Mwenyezi Mungu ametujalia (gesi asilia) ni vizuri tukaharakisha tukaweza kumaliza majadiliano ya ule mkataba mkubwa ili tuweze kupata gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani, lakini vilevile gesi kwa ajili ya kuendeshea mitambo, kwa maana hiyo gesi kwa ajili ya kuweka mbadala wa kiwango kikubwa cha *petrol* ambacho Serikali yetu imekuwa ikiagiza nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia takwimu ninaona karibia 40% ya bajeti yetu inatumika kwa ajili ya kuagiza mafuta. Kwa hiyo, tukianza kutumia hii gesi katika kuendeshea magari yetu hasa ya Serikali tutaokoa fedha nyingi sana hiyo 40% ya bajeti inayotumika kuagiza mafuta kwa ajili ya kuendesha magari ni kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo, tuharakishe uwekezaji kwenye gesi katika nchi yetu ili tuweze kutumia kuendeshea mitambo, kuokoa mazingira kama nilivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi vilevile inaweza kusaidia kama malighafi kwenye viwanda vya kuzalisha mbolea. Ukiangalia nishati ambayo inatumika kwa kiwango kikubwa hasa mbolea aina ya *ammonia* na *nitrogen* kwa kiwango kikubwa gesi ndiyo inahitajika. Tanzania 26% ya bajeti yetu tunategemea kutokana na sekta ya kilimo na Watanzania zaidi ya hiyo 70% wako kwenye kilimo. Kwa hiyo, tukifikia wakati tunazalisha mbolea zetu wenyewe hapa nchini kwa sababu malighafi zote zipo kule Ludewa pia tuna makaa ya mawe. Ukiangalia nchi nyingine kama China makaa ya mawe yana gesi za *nitrogen* na *methane* wanachanganya tu na samadi na vitu vichache vichache tayari wanaenda kuvitumia kwenye kilimo. Kwa hiyo, malighafi zote ambazo zinaweza kutumika katika kuzalisha mbolea tunazo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa sana kuishauri Serikali eneo hili la gesi tulifanyie kazi haraka na inaonekana gesi yetu ilianza kugundulika mwaka 1974 Songosongo na mwaka 1982 *Mnazi bay*. Ninatambua kwamba tangu mwaka 2004 tulianza kuzalisha gesi hapa nchini kwa ajili ya matumizi ya majumbani mpaka leo tuna kilometa zinakaribia 800 ya *line* ambayo tumesambaza gesi kwa watumiaji na kilometa 58 ambayo inahudumia wenye viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo eneo lingine ambalo kuangalia ni kwenye chuma. Chuma nayo na makaa ya mawe yana zile *clinker* ambazo zinaweza kutumika katika viwanda vya saruji na tuna *limestone* ya kutosha sana. Kwa hiyo, tunaweza tukaanzisha pia viwanda vya saruji kwa sababu mahitaji yake kwa nchi hii ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ningependa tuweze kutumia hizi maliasili zetu na sasa hivi tunaona kwamba kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri kutokana na misukosuko mbalimbali duniani kuna njia mbadala nyingi ambazo zinaweza zikachukuliwa na Serikali kama hatua za kunusuru uchumi wetu usiweze kupata madhara, kama hiyo ya kuongeza thamani ya maliasili mbalimbali ambazo tunazo kwenye viwanda, lakini vilevile kwenye sekta ya kilimo. Kuanzisha viwanda vya kuzalisha chakula cha samaki hii itakuwa ni kwanza kumwinua mkulima yule

ambaye analima mazao ambayo yanatumika kama malighafi ya kutengeneza vyakula vya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Wizara ya Mifugo na Uvuvi imejitahidi sana kuanzisha hoja ya ufugaji wa samaki kwa vizimba ingawa sisi kule Ziwa Nyasa wametuahidi kwamba watakuja kufanya utafiti kwa sababu Ziwa letu lina mawimbi makali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tulijaribu kuweka kizimba kimoja tulishirikiana na watu wa *TAFIRI* matokeo yake yalikuwa mazuri sana. Ziwa Nyasa lina *oxygen* kwa wingi kwa hiyo samaki wana uwezo wa kukiona chakula vizuri kwa sababu maji yake ni masafi na yale mawimbi yanavyopiga yanasambaza hewa ya *oxygen* vizuri. Kwa hiyo, Ziwa Nyasa linafaa sana kwa ufugaji wa samaki kwa vizimba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyosema kuwe na viwanda vya kuzalisha chakula cha samaki kwa sababu kwa kiwango kikubwa sasa hivi wafugaji wa samaki wanategemea chakula cha samaki kutoka nje ya nchi. Kwa hiyo, tunaomba na sisi kule Ludewa tuna kata nane, Kata ya Lumbila, Kata ya Kilondo, Kata ya Lifuma, Kata ya Lupingu, Kata ya Iwela, Kata ya Manda na Kata ya Ruhuhu wananchi hawa wote wapo kando kando ya Ziwa Nyasa shughuli zao ni uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale samaki wa asili wameanza kama kupungua kutokana na mabadiliko ya tabianchi na sababu mbalimbali. Hata hivyo, hii ya ufugaji wa samaki kwa vizimba itakwenda kutoa ajira kubwa sana kwa wananchi wale wa Tarafa ya Mwambao na Tarafa ya Masasi, kwa sababu tulishafanya jaribio na tumeona kwamba matokeo ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali na niishukuru kwenye eneo la umeme kazi kubwa sana imefanyika nchini na Jimboni kwangu pia wamefanya kazi kubwa sana, bado mambo machache machache tu. Ludewa tulikuwa na wazalishaji binafsi wa umeme, kulikuwa na MADOPE tunawashukuru walitusaidia sana, lakini pale ambapo walikutana na changamoto Serikali iliweza kutusaidia, wale wananchi wanaotegemea umeme kule Mawengi na Milo umeme wa

JUHUMA walikaa giza karibu miezi tisa, lakini baadaye Serikali ikaweza kutusaidia. Walinisikiliza mimi Mbunge niliyeomba Serikali itafute fedha za dharura kwa ajili ya kurekebisha hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuliweza kuwatoa gizani wale wananchi kwa hili nishukuru sana Serikali; lakini kwa kuwa walikuwa kwenye wazalishaji binafsi bado vitongoji vingine vya Mawengi havijafikishiwa umeme. Kwa hiyo, ninatambua kuna jitihada zinaendelea kule *REA* na *TANESCO* walitutengea bilioni sita na niliambiwa mwezi huu ndiyo kulikuwa na kikao cha Bodi kuweza kuidhinisha zile bilioni sita kwa ajili ya kupelekwa kwenda kuboresha umeme kule Kata ya Lupanga, Kata ya Lubonde, Kata ya Lugarawa, Kata ya Mlangali, Madilu kule na pale Madilu Sekondari. Kwa hiyo, ninatambua kwamba kuna hizo fedha, lakini ninaomba Serikali iongeze kasi ya kusimamia eneo hilo ili wale wananchi hasa vitongoji vile ambavyo havijafikishiwa umeme kule Madilu, Lubonde na Lupanga ili waweze kufikishiwa umeme na maeneo yale niliyoyasema mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vile vijiji vya Tarafa ya Mwambao. Kuna Kata ya Lumbila mkandarasi alishapatikana muda mrefu na Serikali, lakini baadaye ikaonekana anabadilishwa, kuna watu wa Suma JKT walikwenda kufanya *survey* wakaainisha gharama na kila kitu. Kwa hiyo, tunaomba na wenyewe waweze kwenda mapema wananchi wa Lumbila pale Nkanda wanavyoona wenzao wa Ikombe wanalala kwenye umeme wana mwanga, wao kidogo wanajisikia unyonge kidogo. Kwa hiyo, ninaomba taratibu za huyu mkandarasi zikamilike haraka ili wale wananchi wa Kata ya Lumbila na Kilondo waweze kuwekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mkurugenzi Mkuu wa *REA* kwa kuamua yale maeneo ambayo yalikuwa yana changamoto za kijiografia kule kando kando ya Ziwa Nyasa kwenda kuwapelekea umeme wa *solar* wakati maandalizi ya kuwapelekea umeme huu wa gridi yanaendelea. Hii nayo tunashukuru sana, hofu ya wananchi tu ilikuwa kwamba kule mawimbi yale makali muda mwingi sana kunakuwa na Dhoruba, kwa hiyo kukiwa hakuna jua umeme ule wa jua utakuwa unasumbua. Kwa hiyo na yenyewe ni hatua kubwa, tunaomba tu

watu wa *REA* ikiwezekana kabla Bunge halijavunjwa tuweze kujua mkandarasi ni nani aliyepatikana ili tuweze kwenda kuwaeleza wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa nilisemee kidogo ni eneo la sekta ya afya. Tunashukuru sana Serikali kwa kweli miaka hii mitano hospitali ya wilaya pale zimeingia karibia bilioni tatu, Makao Makuu ya Wilaya. Kwa hiyo, miundombinu na vifaatiba vimeboreshwa, kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali; na maeneo ya zahanati, kuna zahanati mpya zinakaribia 21 sasa na wiki iliyopita tunashukuru kwa fedha tumeona kwa ajili ya kukamilisha boma la wananchi wa Nindi milioni 60, lakini Zahanati ya Kijiji cha Limfuma ilichakaa sana. Kwa hiyo, wale wananchi wameweza kupewa milioni 60 kwa hiyo wana uwezo wakichanganya na nguvu zao wakajenga zahanati mpya ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kimata kupitia mradi ule wa *TASAF* wamepelekewa zaidi ya milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati. Tunaishukuru sana Serikali sambamba na wale Wananchi wa Mbongo, Mbugani, Sagalu, Kimelembe, Lifua na maeneo mengine. Tunashukuru pia kwa ajili ya wale wananchi wa Kisaula nao wamepelekewa milioni 30 waweze kumalizia boma lao, haya ninayoyasema ndiyo ambayo yatajaza kura nyingi sana kwa Chama Cha Mapinduzi mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu fedha imeonekana hadi kwenye vitongoji, hii Kisaula ninayoisema ni kitongoji kina wananchi zaidi ya 700 wana shule ya msingi, walianza boma lao na sasa Serikali imewaongezea milioni 30 ili waweze kumalizia zahanati yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe tu lile swali nililouliza asubuhi kuhusu maji Kisaula wale wananchi kwa sababu Mheshimiwa Rais amenunua mitambo ni kutafuta mafuta kupeleka mtambo eneo lile ambalo wanataka kujenga zahanati ili wasisumbuke sana kujenga zahanati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la afya kuna wananchi walianza maboma mengi. Kwa hiyo, ninaomba Tume

ya Mipango iweze kutusaidia kuweka kwenye mipango. Tunashukuru awamu hii ya miaka mitano tumepata fedha kwa ajili ya vituo vya afya vitatu. Kituo cha Mundindi na Kituo cha Afya cha Madilu milioni 669, kwa hiyo niishukuru sana Serikali. Mawengi pia na wenyewe wamepata kwa ajili ya kukamilisha kituo cha afya, awamu ya kwanza tumezikuta katika *deposit account* milioni 250. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaishukuru sana Serikali, nikitembea Ludewa kwa wananchi *off course* ninatembea kwa heshima, naheshimika sana kutoka na Serikali kupeleka miradi hii mingi. Hili linaonesha kwamba yajayo yanafurahishwa sana, wananchi wa Ludewa wamekuwa na imani kubwa sana na mimi Mbunge wao, lakini jeuri yote hii nimeipata kutokana na Serikali kupeleka fedha kwa wingi na kufufua miradi ambayo kwa miaka mingi sana ilikuwa kama imekufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mawasiliano ya simu; ninamshukuru vilevile Mheshimiwa Jerry Silaa alituma wataalam pale Makonde na leo nimepigiwa simu na watu wa *TTCL* kwamba vifaa na ujenzi utaanza wiki ya kwanza ya mwezi Julai. Tena kwa pamoja ujenzi pale Nsisi, Lupingu pamoja na Makonde wiki ya kwanza ya mwezi Julai ujenzi utaanza, lakini minara mingine zaidi ya tisa ujenzi unaendelea. Kwa miaka hii mitano jumla ya minara ya simu 26 kazi hii siyo ndogo ni kazi kubwa na mawasiliano ya simu siyo anasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi leo wanaweza kuuliza bei ya viazi wanavyolima kwenye kipalila wale wananchi wa Mangalanyene anapiga simu Kariakoo yeye mwenyewe, anapiga simu Dodoma, anapiga simu popote kutoka kijijini, lakini hata watumishi waliokuwa wanatembea mwendo mrefu kwenda kusajili wanafunzi kwenye mifumo mawasiliano ya simu au wale wa sekta ya afya ule mfumo unaitwa *GoT-HoMIS* na wenyewe umewapunguzia mwendo, walikuwa wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamoga, ninaona fursa aliyoitoa Mheshimiwa Naibu Spika, umeitumia kuliko wote.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, huyo ndiye mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo na kwa vile shughuli zote za leo zimekamilika, basi niwatakieni kila la heri na ninawatakia mchana mwema.

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 7.42 Mchana Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 18 Juni, 2025, Saa Tatu Asubuhi)*